

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Nane – Tarehe 11 Aprili, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma M. Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 62

Kuangalia Upya Suala la Utoaji wa Ruzuku za Maendeleo

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

Mabadiliko ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 yameleta nafuu sana kwa wakulima, lakini wakati huo huo Halmashauri za Wilaya zenyе wakulima wadogo zimeathirika kimapato na kusababisha kushindwa kutatua kero za wananchi kwa wakati.

(a) Je, Serikali inaweza kuangalia upya suala la utaoji ruzuku za maendeleo?

(b) Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imeathirika kwa kiwango kikubwa: Je, Serikali ipo tayari kuipatia ruzuku ili kutoa huduma za elimu na afya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 imefanyiwa marekebisho na Bunge Mwezi Juni, 2017 kwa kupunguza kiwango cha ushuru wa mazao kutoka asilimia tano hadi asilimia tatu kwa mazao ya chakula na biashara. Hata hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kubuni vyanzo vipyta vyatapato na kuimarisha makusanyo katika vyanzo vilivyopo ili kuongeza mapato na kuboresha utaoji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mikakati hiyo, mapato ya ndani ya Halmashauri yameendelea kuongezeka kila mwaka. Mfano, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 687 na zilikusanya shilingi bilioni 553.39 sawa na asilimia 81. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri zimeidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 735.58 hadi Februari, 2019 zimekusanya shilingi bilioni 401 sawa na asilimia 55. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri zimekadiria kukusanya shilingi bilioni 765.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi kwa ujumla inaonyesha makusanyo ya Halmashauri yameendelea kuongezeka pamoja na kupungua kwa ushuru wa mazao kutokana na Halmashauri kubuni vyanzo mbalimbali vyatapato na vyanzo mbadala. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kuzisimamia Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuimarisha makusanyo na kupunguza utegemezi kutoka Serikali kuu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwaka 2019, Serikali imepeleka kiasi cha shilingi milioni 416 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwa ajili ya kugharamia Elimu Msingi

Bila Malipo, shilingi milioni 250 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 20 ya shule za sekondari na shilingi 411 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba. Serikali itaendelea kuongeza utoaji wa ruzuku kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Richard Mbogo, swalii la nyongeza.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu ya Serikali, tunajua ongezeko la mapato. Tuna Halmashauri 185 lakini zinatofautiana kati ya Halmashauri na Halmashauri. Kwa hiyo, pamoja na ongezeko la kibajeti, bado Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imeathirika na mabadiliko ya Sheria hii. Sasa je, Serikali iko tayari kuongeza ruzuku toka hii ambayo tumeipata ya shilingi milioni 250 ambapo tumeweza kumalizia maboma ya shule mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; tuna changamoto pia upande wa huduma za kiafya. Kata ya Itenka pamoja na Kata ya Ugara ziko mbali sana na upatikanaji wa huduma: Je, Serikali iko tayari kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata hizi mbili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali iko tayari kuendelea kukamilisha maboma ya afya na elimu na ndiyo maana Mwezi wa Pili tumepeleka fedha zaidi ya shilingi bilioni 29.9 katika Majimbo mbalimbali likiwepo na hili la Nsimbo kukamilisha maboma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimesema, Serikali itaendelea kupeleka fedha ya ruzuku ya

miradi ya maendeleo mbalimbali kadri ambavyo fedha itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili anaulizia kuwa na vituo vya afya. Ni nia njema ya Serikali kuendelea kuimarisha huduma za afya na tumefanya hivyo, vimejengwa vituo 352. Kwenye bajeti hii ambayo tunaendelea na mjadala kwenye Bunge lako Tukufu tunavyo vituo 52 vingine, hospitali 27, ukiongeza zile 67 zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtie moyo Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufanya kazi hii ya kutoa huduma ya afya kwa wananchi wake kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Pamoja na Halmashauri zetu kufanya vizuri, kuna baadhi ya vyanzo hawafanyi vizuri. Mfano, chanzo cha Kodi ya Ardhi, mwanzoni walikuwa wakikusanya wanapata *retention* ya 30 percent lakini sasa hawapati *retention* hiyo ambayo ilikuwa inawasaidia kujaza gari mafuta waweze kufuatilia wale ambaao hawalipi Kodi ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu: Je, Serikali iko tayari kuangalia upya chanzo hili ili kisaidie kukusanya kodi hii ya ardhi kwa asilimia 100?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalii hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Gekul kwa kazi nzuri anayoifanya kule Babati kuwasemea watu wa Babati, lakini pili, naomba nilipokee suala hili kama sehemu ya changamoto, tuwasiliane na Halmashauri ya

Babati Mjini, Wizara ya Ardhi na TAMISEMI tuone changamoto zilizopo tuweze kuziimarisha.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge.

Na. 63

Chanzo cha Maji Mto Kagera

MHE. BALOZI. DKT. DIODORUS B. KAMALA aliuliza:-

Mto Kagera ni chanzo muhimu kinachoweza kusaidia upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wanaopakana nao:-

Je, kwanini Serikali isifanye utaratibu wa kuvuta maji hayo ili yawasaidie wakazi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza mipango ya kutumia Mto Kagera kama chanzo cha maji katika maeneo mbalimbali yanayopakana na Mto huo. Kwa sasa Serikali kuititia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA) imepanga kuutumia Mto Kagera kama chanzo cha maji kwa Miji ya Kyaka na Bunazi pamoja na vijiji mbalimbali vinavyozungukwa na mto huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi kwenda Miji ya Kyaka na Bunazi kwa kutumia chanzo cha mto huo, BUWASA imemwajiri mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni na matarajio ya usanifu huo utakamilika mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya ujenzi wa mradi huo utaanza katika mwaka wa fedha 2020/2021.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kamala.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na ninashukuru pia kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Waziri wake na Katibu Mkuu wake. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba alituma wataalam kule Kata ya Kanigo, Kata ya Kashenye, Kata ya Ishaizi na Kata ya Ishunju kwa ajili ya maandalizi ya awali ya kutumia maji ya Ziwa Victoria. Je, yuko tayari kuharakisha jitihada hizo ili maji hayo yaanze kutumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalidogo la pili. Kwa kuwa Wilaya ya Misenyi tumebarikiwa kuwa na mito mingi; tunao Mto Kagera pamoja na Mto Nkenge na mingine: Je, mradi kama huu ambao uko mbioni kuanza kama Mheshimiwa alivyojibu katika maeneo ya Kyaka na Bunazi, atakuwa tayari kubuni mradi kama huo katika maeneo yaliyo karibu na Mto Nkenge?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya. Nilifika katika Jimbo lake, nimeona kazi kubwa zinazofanyika katika eneo lile. Kubwa ambalo ninalotaka nimhakikishie, sisi kama Wizara ya Maji ambayo siyo Wizara ya ukame, tumeona haja kwamba haina budi na kwamba haiwezekani tuone kabisa vijiji ama Miji ambayo iko karibu na mito mikubwa ama maziwa wakose maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna vyanzo vyaa uhakika, ndiyo maana tumewatuma wataalam wetu

waweze kwenda katika eneo lile ili tuweze kubuni mradi na wananchi wake waweze kupata majisafi na salama na yenye kuwatoshaleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la *ku-design* katika Mto Nkenge; uwepo wa chanzo unatupa nafasi kama Wizara ya Maji katika kuhakikisha tunabuni miradi mikubwa ili tuweze kuwapatia wananchi wake maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kuanzisha mradi katika Mto Nkenge ili wananchi wake waweze kupata majisafi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa upo mradi wa maji ambao tunautegemea sana katika Wilaya ya Ngara, mradi ambao tayari umeshapata kibali cha Serikali; na mwaka huu unaoishia kwenye bajeti zilikuwa zimetengwa shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza usanifu wa mradi huu.

Ni lini Mhandisi Mshauri atakuwepo *s/ite* tayari kwa ajili ya kuanza usanifu wa mradi huu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, binafsi nilipata nafasi ya katika Jimbo lake la Ngara na tumeona chanzo cha Mto Ruvubu ni chanzo cha uhakika na kina maji mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama viongozi wa Wizara ndio maana tukamtuma mtaalam wetu. Kwa hiyo, kubwa tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha Mhandisi Mshauri anapatikana kwa haraka ili kazi iweze kuanza mara moja na wananchi wake waweze kupata mradi huo.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Nicolaus Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini.

Na. 64

Tatizo la Maji Safi na Salama Mji wa Tarime

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kukamilisha mradi wa visima 23 ambavyo vingesaidia kama suluhisho la muda mfupi la tatizo la maji safi na salama katika Mji wa Tarime hususan kwenye maeneo ya Kata za pembezoni kama Nyandoto (Masurula), Nkende, Ketare, Kenyamanyori, Nyamisangura na Turwa?

(b) Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Jimbo la Tarime Mjini Julai, 2018 aliwaeleza wananchi kuwa Serikali imetenga takriban shilingi bilioni 14 kwa ajili ya maji kutoka Ziwa Victoria ambayo itaondoa kabisa tatizo la maji katika Mji wa Tarime. Je, ni hatua gani imefikiwa kwenye ahadi hiyo hasa ikizingatiwa kuwa mradi huo upo kwenye mchakato kwa miaka mingi sasa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicolas Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) imeingia mkataba na Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) kwa ajili ya uchimbaji wa visima 23 katika Mji wa Tarime kwa gharama ya shilingi milioni 536.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa *DDCA* wanaendelea na utafiti wa maji chini ya ardhi (*hydrological survey*) na matarajio ya kazi ya uchimbaji wa visima hivyo itakamilika mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa ahadi ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa wananchi wa Tarime, Serikali imeshapata fedha kutoka Serikali ya India kiasi cha dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji kwa miji 28 ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar ambapo Mji wa Tarime ni miongoni mwa Miji itakayopata maji kupitia fedha hizo. Kwa sasa taratibu za kuwapata wataalam washauri watakaofanya usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni unaendelea. Matarajio ya ujenzi wa miradi hiyo itaanza katika mwaka wa fedha 2019/2020. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko, swalii la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa majibu yanayotia matumaini kama yatakelezeka, kwa sababu mradi wa Ziwa Victoria kuanzia wakati wa Mheshimiwa Eng. Kamwelwe alisema mnafanya upembizi yakinifu na mradi ungeenda kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mji wa Tarime ndiyo Makao Makuu ya Wilaya Tarime na umekuwa na matatizo ya maji kwa muda mrefu na kusababisha wananchi wasifanye shughuli zao za maendeleo; na kwa kuwa vyanzo vikuu katika Mji wa Tarime ni Bwawa la Nyanduruma na lile la Tagota ambalo halitoi majisafi na salama na Wizara tuliowaomba hata angalau wajenge *treatment plant* wakasema wanategema mradi mkubwa wa Ziwa Victoria:

Ni lini sasa mtahakikisha kwamba ule mradi ambao tumeuanzisha Gamasara ambao tumesha-*rise certificate*, Mkandarasi amesimama kuanzia Novemba tumeleta Wizarani mpaka leo hajalipwa, ni lini yule Mkandarasi atalipwa ili angalau ajenge lile tenki la lita 100,000 kuweza kusaidia wananchi wa Gamasara na Kata ya Nyandoto na Kata za pembezoni kwa kipindi hiki tukisubiria huu mradi wa Ziwa Victoria ambao mmesema unakwenda kuanza mwaka 2019/2020?

La pili, hawa *DDCA* wameshakamilisha na walileta *certificate* na hata Mheshimiwa Eng. Kamwelwe mimi mwenyewe nilimpa *document*, lakini mpaka leo inavyosemekana, hawajalipwa fedha na ndio maana hata hawajaanza kufanya huo utafiti wa maji ya chini ya ardhi kama mlivyo-*report* hapa. Napenda sasa nihakikishiwe leo kwamba hawa *DDCA* watalipwa fedha ili wananchi wa Tarime hasa zile Kata za pembezoni waweze kuchimba visima na wapate majisafi na salama. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimtoe hofu dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko, Serikali ya Awamu ya Tano ikiahidi inatekeleza na ikichelewa kutekeleza, basi kunakuwa na sababu maalum ya kueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ninalotaka kusema, pamoja na mradi mkubwa huo wa Ziwa Victoria katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji Tarime, lakini tuna mradi pale Gamasara wa asilimia 25, lakini tunatambua kabisa utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri, tulikuwa na madeni ya Wakandarasi zaidi ya shilingi bilioni 88, lakini tunamshukuru Mheshimiwa Rais amewaagiza watu Wizara ya Fedha kutupa zaidi ya shilingi bilioni 44 kwa ajili ya kuwalipa Wakandarasi na tumeshazipata na tumeshazigawa. Tuna shilingi bilioni 44 nyingine tutakazopewa mwezi huu wa Nne. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie, katika maeneo yote ambayo Wakandarasi wanadai, tutawalipa ili miradi iendelee kutekelezeka na ahadi ya kumtua mwana mama ndoo kichwani iweze kitimilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la *DDCA*, sisi pale tumeona haja ya uchimbaji wa visima. Sasa katika mgao huo wa shilingi bilioni 44, watu ambao wamelipwa ni

watu wa *DDCA*. Tunawaagiza waende Tarime haraka katika kuhakikisha hii kazi inafanyika ili ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mwana mama ndoo kichwani inatimilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba endeleeni kutuunga mkono bajeti yetu katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, halafu Mheshimiwa Zungu.

MHE. JOHN. W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Swali hili limekuja wakati mzuri kwa sababu ni swali linalohusu Tarime na ilikuwa Wilaya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais amekuja Tarime Mwezi Julai, alisimama kwenye Mji wa Nyamongo kwenye Kijiji cha Kewanja na akaahidi kwamba Mwezi wa Tatu mwaka huu, watu wa Nyamongo ambao ni zaidi ya 35,000 wakazi wa pale na wakazi wa Sirari watakuwa wamepata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje kuhusu hilo likiendana sana hasa na swali hili ambalo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Mwezi Julai?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu tu kwa ufupi Mheshimiwa Mbunge. Ahadi ni deni; na Mheshimiwa Rais anapoahidi sisi hatuna kikwazo cha kushindwa kutekeleza. Kwa hiyo, tumejipanga katika kuhakikisha tunalitekeleza hilo jambo ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge tunachimba visima kwenye maeneo yetu. Kisima cha mita 100 kina-*cost* takribani shilingi milioni saba, lakini ukienda Halmashauri kisima cha mita 100, għarama zinazolipwa ni zaidi ya shilingi milioni 35 kwa kisima kimoja. Visima hivi 23 ambavyo vinataka kuchimbwa Tarime vitagħarimu siyo chini ya shilingi milioni 900 kwa bei za Wakandarasi na bei za hao wanaokwenda huko kwenye Halmashauri zao.

Je, Serikali sasa lini ita-*revisit* bei hizi na kutoa bei elekezi kuhakikisha pesa za Serikali zinaokolewa na ubadhirifu ili wananchi wapate maji kwa bei nafuu ambapo yanaweza kupatikana kwa shilingi milioni saba tu kwa kisima cha mita 100? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Zungu kwa swali lake zuri sana lakini kubwa tukiri kwamba kulikuwa kuna ubadhirifu mkubwa sana hasa katika miradi ya maji. Sisi tumeona hilo na ndiyo maana tukaanzisha Wakala wa Maji Vijjjini na tuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutupitishai Muswada wetu na sisi tumejipanga katika kuhakikisha tunasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na għarama nafuu, sisi tunataka tuuongezee uwezo kwa Wakala wa Maji wa Uchimbaji Visima (*DDCA*) katika kuhakikisha tunawapa vifaa vyā kutosha ili uchimbaji wake uwe nafuu uweze kuendana na watu binafsi. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 65

Mradi wa Umeme wa Msongo wa KVA 400

MHE. SILYVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Mradi wa Umeme mkubwa wa msongo wa KVA 400 toka Kinyerezi kuititia Pwani, Morogoro, Singida na Arusha umechukua maeneo ya wananchi kwa muda mrefu bila kuwalipa fidia:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kulipa fidia hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia *TANESCO* inatekeleza mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovolts 400 kutoa Kinyerezi - Dar es salaam na Rufiji - Pwani kuititia Chalinze hadi Dodoma. Malengo ya mradi huo ni kuongeza upatikanaji wa umeme katika ukanda wa Mashariki, Kati na kaskazini mwa nchi kutoka kwenye mitambo ya kuzalisha umeme (Kinyerezi) na mradi wa Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya upimaji njia na kutathmini mali za wananchi watakaopisha mradi kutoka Kibaha hadi Chalinze ilikamilika Mwezi Desemba, 2017 na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali Mwezi Novemba, 2018. Serikali kuititia *TANESCO* Mwezi Januari, 2019 itatangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mtaalam mshauri wa kufanya upembusi yakinifu wa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Rufiji hadi Chalinze na kuhuisha upembusi yakinifu wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi hadi Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shilingi bilioni 21 na milioni 600 zinatakiwa kulipwa kama fidia kwa wananchi katika maeneo ya Halmashauri za Kisarawe, Kibaha Mjini, Kibaha Vijiji na Chalinze na eneo la Kiluvya na taratibu zote za uandaaji taarifa na majedwali ya malipo ya fidia zimekamilika. Serikali inatarajia kutenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 34 kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wa maeneo hayo baada ya kukamilika kazi ya kuhuisha upembuzi yakinifu ikiwa ni pamoja na gharama za mradi wa kipande cha Kinyerezi Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wananchi waendelee kuvuta subira wakati Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za malipo yao ya fidia. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Koka, swali la nyongeza.

MHE. SILYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kazi kubwa anayoifanya katika miradi ya umeme na hususan mradi mkubwa wa *Stiegler's gorge* ambao unakwenda katuondolea gharama kubwa ya umeme hakika ni neema. Nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri ameshatutembelea zaidi ya mara tatu katika Jimbo langu, anachapa kazi na kwa pamoja Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, pamoja na kuchukua muda mrefu katika fidia hii, lakini wananchi wa Kibaha wana taarifa kwamba wenzao wa Arusha na Singida walikwishakupata malipo, kama hivi ndivyo, je, wanapata malipo kwa ubaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika miradi ya ujazilishaji katika Mji wa Kibaha yaani *densification* Mitaa ya Muheza, Mbwate, Lumumba, Sagale, Mkombozi, Mbwawa Hekani, Kumba na Mtakuja miradi hii bado haijaanza utekelezaji kama ilivyokuwa imeahaidiwa. Je, Serikali ina

mpango gani wa kukamilisha miradi hii ambayo wananchi wanaisubiri kwa hamu ili waweze kupata umeme na kukidhi mahitaji yao ya kiuchumi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali haya ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Silvestry Koka, ndugu yangu kutoka Jimbo la Kibaha Mjini kuwa kwanza tumepokea pongezi na nichukue fursa hii kumpongeza yeye binafsi Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzake wa Mkoa wa Pwani amba o wanapitiwa na mradi huu akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha Vijijiini, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze pamoja na dada yangu Mheshimiwa Bonnah, Mbunge wa Jimbo la Segerea kwa kazi ya kuwasemea wananchi wao na kufuatilia masuala ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyo sema nimefanya ziara katika maeneo yao mbalimbali, lakini nataka niseme moja ya jambo ambalo limejitokeza baada tu ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuja na mapinduzi ya kutaka kutekeleza mradi wa *Rufiji Hydro Power Stiegler's*, njia hii ya msongo wa kilovoti 400 ilikuwa inaitwa Kinyerezi – Chalinze - Tanga. Kwa hiyo baada ya kuja na ule mradi ilikuwa lazima sasa kuwe na *line* ya kilovoti 400 kutoka Rufiji mpaka Chalinze ambayo inaunganishwa na Dodoma na kimsingi kwa ajili pia ya kuwezesha treni yetu ya umeme ambayo kama maelezo yalitolewa inatarajia kuanza kazi Novemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na wananchi, nami mwenyewe pia ni muhanga kwa sababu nawakilisha wanawake wa Mkoa wa Pwani. Nataka niseme kwa kweli kwa kuwa mradi huu wa ujenzi wa njia hii ya msongo wa kilovoti 400 unaanza kutekelezwa Januari, 2020, hatuwezi kuanza mradi huu bila kuwalipa wananchi fidia. Kwa hiyo

kiwango kilichotajwa kwenye jibu langu la msingi cha bilioni 36 na kwamba ndio wakati wake muafaka sasa wa kulipa kwa sababu hata fidia inayolipwa maeneo ya Singida, maeneo ya Mkoa wa Manyara kwa ajili ya njia ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida mpaka Namanga ni kwa sababu mradi umeanza kutekelezwa na ndio maana lazima ulipe fidia maana yake ni moja ya masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa maeneo haya niliyoyataja, tunawashukuru na tunawaomba radhi kwamba wamechukua muda mrefu lakini wamekuwa na subira, waendelee na kwamba sasa kwa kweli mchakato wa malipo upo mbioni kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ametaja maeneo ya Muheza, Lumumba, Madina, Mtakuja, Mbwawa kote huku mimi na Mheshimiwa Mbunge tulifanya ziara pamoja, nataka niwathibitishie wananchi kwa kazi ambayo Mheshimiwa Mbunge alikuwa anafanya kwamba maeneo haya tuliahidi kuyapelekea umeme kwa mradi wa *Peri-urban* na huo mradi wa *Peri-urban* pia unagusa Jimbo ya Ukonga kwa ndugu yangu Mheshimiwa Waitara pia kwa ndugu yangu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya maeneo ya Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwa hatua iliyofikiwa, mradi huu unaanza mwezi wa Nne kwa sababu taratibu zote za manunuzi zimekamilika na kwa sasa wakandarasi wale au wale ambao wametenda ipo hatua *ya post qualification*. Kwa hiyo Serikali imedhamiria kwa dhati kabisa maeneo ambayo yanakua kwa kasi kupelekea mradi wa *Peri-urban*. Naomba tu waendelee kuvumilia mwezi wa Nne mwishoni utaanza huu mradi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suzan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona swali hili la Mheshimiwa Koka, tena hili la juzi, lakini katika Jimbo la Mlimba kuna mradi mkubwa

wa umeme mkubwa ulikuwa unapelekwa kutoka Kihansi Jimboni Mlimba kwenda Wilaya ya Malinyi, katika mwaka 2014 na mpaka 2016 *TANESCO* ikakubali kwamba wale watu wanatakiwa walipwe, lakini mpaka leo unavyozungumza wengine wameshakufa, wengine wameshazeeka hawajalipwa hata senti tano. Je, ni lini sasa Serikali itawalipa hawa wananchi au kwa vile wako mbali sanahakuna barabara jamani kosa, letu nini wananchi wa Mlimba? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan, Mbunge wa Jimbo la Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nipokee hii changamoto ambayo ameielezea Mheshimiwa Suzana na nikitambua kwamba kwa kipindi cha Bunge hili la Kumi na Moja, awamu ya kwanza alihudumu Kamati ya Nishati na Madini na nimwahidi kwamba tutaenda kufuatilia kwa sababu maeneo haya anayoyataja na kwa kuwa mradi mkubwa wa Kihansi unaozalisha umeme zaidi ya megawati 180 ni ya wananchi wa maeneo hayo, hivyo tunawategemea sana na wamekuwa watunzaji wazuri wa mazingira na mpaka sasa hivi hatujawahi kupata changamoto yoyote ya kusema labda maji yamepungua katika uzalishaji wa umeme. Kwa hiyo nimwahidi Mheshimiwa Mbunge baada tu ya hapa naomba tufuutilie, kwa sababu hata jana aliniambiakuhusu hili suala ili kuona fidia imefikia wapi, lakini nihakikishe kwamba kama haki hiyo ipo na tahmini ilifanyika Serikali ya Awamu ya Tano inalipa fidia. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salma Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kuuliza kuhusu suala la fidia; wananchi wa Mkuranga, Kibiti na Rufiji wanadai fidia zaidi ya miaka mitatu kutoka *TANESCO*. Sasa kutokana na mradi huu wa

umeme wa Kinyerezi, je, ni lini wananchi hawa watalipwa
hizo fidia? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mama yetu Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, Mbunge wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, lakini anahudumu Mikoa ya Pwani na Lindi kama ambavyo ameuliza masuala ya fidia ya mradi wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Somangafungu Kinyerezi. Kimsingi mradi huu fidia yake inalipwa na *TANESCO* na maeneo ambayo yalipitiwa na mradi huu kuanzia Kilwa, Kibiti, Rufiji, Mkuranga na maeneo ya Mbagala na Ilala Dar es Salaam, nataka nikiri kwamba kutokana na mradi huu takribani gharama yake kama isiyopungua billioni 50 hilvi, lakini *TANESCO* mpaka sasa hilvi wamelipa zaidi ya billioni 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba zipo changamoto za baadhi ya wananchi wachache na hata hivi karibuni tulipanga na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mkuranga kufanya kikao na Menejimenti ya *TANESCO* ili kuweza kutambua mpango wao mkakati wa kumalizia malipo ambayo yamesalia. Kwa hiyo, nimshukuru kwamba na tunamwalika Mheshimiwa Mbunge, Mama yetu Mama Salma Kikwete na Mheshimiwa Mbunge wa Rufiji na Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa katika kikao hiko ili kutambua akina nani wamelipwa, akina nani hawajalipwa kwa sababu zipo changamoto pia katika suala zima la wanaojitokeza. Hata hivyo, nimwahidi kabisa kwamba *TANESCO* kwa kweli wamejipanga kulipa kwa sababu mradi huu ni lazima utajengwa kutokana na uwekezaji unataka kufanyika Mkoa wa Mtwara wa ujenzi wa mtambo wa kuzalisha megawati 300 na Somangafungu yenywewe wa ujenzi wa mtambo wa kuzalisha megawati 330. Kwa hiyo nimshukuru na kumpongeza kwa swali lake zuri hili. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 66

Hitaji la Chuo cha Mafunzo ya Gesi na Mafuta Kanda ya Kusini

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA aliuliza:-

Gesi ambayo imegunduliwa katika Mkao wa Mtwara itanufaisha wananchi wote nchini na Taifa kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kujenga Chuo kitakachotoa mafunzo ya gesi na mafuta katika Kanda ya Kusini ili vijana wa Lindi na Mtwara na maeneo mengine waweze kupata taaluma na kuweza kushiriki kwenye sekta hii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuvitumia vyuo vilivyopo nchini kuwajengea uwezo wa kitaaluma wananchi katika masuala ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia. Kwa mfano, kwa mwaka 2010 Kampuni ya *Petrobras* ilitumia Dola za Marekani 350,000 sawa na shillingi milioni 780 kufundisha na kukipatia Chuo cha *VETA* Mtwara vifaa vya mafunzo. Aidha, kuititia mpango huo wanafunzi 50 na wakufunzi wawili walifundishwa kwenye fani ya umeme na makanika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Statoil* imekuwa ikifadhili mafunzo mbalimbali kwa ngazi za vyuo kwa mfano mwaka 2013 ilifadhili wananchi tisa kusoma shule ya biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, masuala ya fedha na

uchumi wamafuta na gesi asilia. Aidha, Kampuni ya *BG* waliendesha mafunzo na VETA Mtwara kwenye fani za *English Language, Food preparation, Plumbing, Welding, Carpentry, Motor Vehicle Maintenance, Electrical Installation and Maintenance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2013 ilitoa ufadhilli kwa wanafunzi 50 kusoma Chuo cha VETA Mtwara. Aidha, Serikali kupitia *TPDC* imefungua klubu 32 za mafuta na gesi katika shule za sekondari za mikoa ya Lindi na Mtwara kwa lengo la kutoa elimu inayohusu tasnia ya mafuta na gesi asilia pamoja namna inavyoweza kuwanufaisha kupitia fursa zinazotengenezwa na tasnia hii katika maeneo yao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shamsia, swalı la nyongeza halafu Mheshimiwa Mama Kahligi.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa nini Serikali haitaki kuwapa gesi wawekezaji wa kiwanda cha mbolea ambao wako tayari kujenga Msangamkuu, Mkoani Mtwara vijijini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı langu la pili, mionganı mwa manufaa ya gesi kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara ni pamoja na kupelekewa umeme lakini mpaka sasa baadhi ya maeneo hakuna umeme Mkoani Mtwara. Naomba kujua kwa nini Serikali haipeleki umeme maeneo mengi ya Mkoa wa Mtwara? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Mbunge Shamsia, wifi yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuna mwekezaji, ni kweli wapo wawekezaji kampuni ya *WD capital* ya *Egypt* pamoja na *Oman Petra*

Chemical ya Oman na *LMG* ya Ujerumani ambayo iliingia makubalino na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani kuwekeza kiwanda cha mbolea katika Mji wa Msangamkuu ambayo itatumia malighafi ya gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme sio sahihi sana kwamba walikataliwa kupewa gesi, lakini kikwazo kilikuwa bei ya gesi ambao wawekezaji wetu walikuwa wanaitaka. Kwa mfano, sambamba na huyo pia kuna mradi wa Kampuni ya *Ferresta*/ambayo waliingia ubia na Kampuni yetu *TPDC* lakini wote hao walikuwa bei yao ya awali ambayo walikuwa wanaitaka ni iwe *USD* 2.26 ambako gharama za uzalishaji wa gesi hizi kwa mujibu wa EWURA ni *USD* 5.6. Kwa hiyo utaona *gape* yake lakini Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayovutia wawekezaji ili kuititia maagizo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli iliridhia tuanze mchakato wa mazungumzo. Kuititia mchakato wa mazungumzo ambao ulihusisha *T/C* ambayo yalifanyika mwezi Machi mwaka huu 2019, tumefikia bei ambayo wenzetu wawekezaji hawa wamerejea ili kuitafakari na baada ya wiki mbili walisema watarejea tena na bei hiyo ni kama *USD* 3.36 ambayo tunaamini pengine hiyo inaweza sasa ikafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwathibitishie wakazi wa maeneo ya Kilwa ambako *Ferresta* na *TPDC* watajenga kiwanda hicho na wakazi wa maeneo ya Msangamkuu Mkoani Mtwara kwamba, fursa ya ujenzi wa viwanda vya mbolea ambao faida kubwa itatoa ajira na mapato bado ipo na Serikali hii ya Awamu ya Tano kuititia hata Ofisi ya Waziri Mkuu Uwezeshaji na hata Taasisi ya *T/C* na taasisi zingine tutahakikisha kwamba fursa hii itafanyika kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ameulizia kwa nini Mkoa wa Mtwara kwa kuwa unatoa gesi haujapelekewa umeme kwa kiwango ambacho Mheshimiwa Mbunge ameulizia. Nataka niseme ni kweli Mkoa wetu wa Mtwara tunautegemea sana kwa gesi megawati 1,600, zinazozalishwa sasa asilimia 52 inatokana na gesi. Pia Mkoa wa Mtwara kwa *REA* awamu ya tatu inaendelea ina viji 167,

Iakini Manispaa ya Mtwara Mikindani baadhi ya maeneo hata mimi niliyatemebelea Mkangaula, Mkanalebi na pale maeneo ya mjini na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo tulikuwa naye pamoja na amekuwa wakiliulizia mara kadhaa hapa ndani ya Bunge kwa kazi nzuri ya kufuatilia miradi hii nimhakikishie tu ujazilizi awamu ya pili unaendelea na utaugusa Manispaa ya Mtwara Mikindani na maeneo mengine na hata Mkoa wa Lindi kwa sababu bado tunatarajia gesi kutoa mchango mkubwa katika kuzalisha umeme ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alfredina Kahigi.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuulizia swali la nyongeza. Je, ni vigezo gani ambavyo vimepelekea kupeleka gesi ya bei nafuu majumbani Mkoani Dar es Salaam, sehemu za Mikocheni badala ya kuipeleka Mtwara mahali ambako gesi inaanzia. Ahsante? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri umemwelewa, haya majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kahigi, kwanza nimpongeze kwa kutambua utanzania uliopo kwa sababu ye ye anatokea Mkoa wa Kagera, Iakini ameuliza swali linalohusiana na masuala ya gesi, kwa nini kwa watu wa Mtwara hawakuunganishiwa hii gesi ya majumbani. Nataka nimthibitishie kuititia Serikali yetu na *TPDC* kwa sasa na Mheshimiwa Waziri wetu wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani alizindua mradi wa usambazaji gesi majumbani Mkoa wa Mtwara na Dar es Salaam na ni kweli kwamba Dar es Salaam tuna takribani viwanda zaidi ya 20 ambavyo vimeunganishiwa, tuna nyumba nyingi Iakini ndio utaratibu za kuunganisha zaidi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimthibitishie Mheshimiwa Kahigi kwamba hata sasa hivi tunasubiri tu vifaa na kuanzia mwezi wa Nne wakazi wa Mkoa wa Mtwara

kwenye nyumba za maeneo ya *railway* pale wataunganishiwa gesi, Chuo cha ufundi Mtwara *Technical* kitaunganishiwa gesi, pia na maeneo ya Mkuranga viwanda vyaa *Gypsum* nao wote wataunganishiwa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme, miradi hii ya kusambaza gesi asilia majumbani ni mradi ambao unahitaji mtaji mkubwa. Tunaishukuru sana Wizara ya Fedha kwa kuridhia kwamba *TPDC* waendelee na mchakato wa kuhuisha sekta binafsi katika uwekezaji wa mradi huu ambao unatarajia kutumia takriban bilioni 200 katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Dodoma na Tanga na pia kuna mpango wa kujenga bomba la gesi kuelekea Uganda, zote ni kutumia hizo fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nithibitishe kwamba kwa kweli Serikali yetu ya Awamu ya Tano inatambua matumizi ya gesi asilia ukiacha kuzalisha umeme lakini kwa viwandani na majumbani ili kulinda mazingira yetu kwa wananchi kuacha kukata miti, watumie gesi mbadala. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimemkiliza vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri, dada yangu akijibu hili swalii, nami naliona ni jambo la muhimu sana kwa sababu uharibifu wa mazingira katika nchi hii umekuwa mkubwa sana na kwa sababu nchi yetu inatumia pesa nyngi sana za kigeni kuagiza mafuta kwa ajili ya magari na mitambo. Je, ni lini Serikali italeta hapa Bungeni mpango mkakati wa namna gesi yetu itakavyotumika majumbani na kwenye magari na mitambo mingine ili kuweza kuokoa pesa nyngi za kigeni ambazo zinatumika kwa ajili ya kuagiza mafuta kutoka nje? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Selasini,

kaka yangu na Mbunge wa Jimbo la Rombo ambalo ameuliza ni lini Serikali italeta mpango mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme Serikali kupitia *TPDC* ina mpango mkakati wa matumizi ya gesi, tangu gesi ilivyogunduliwa na kwa kuwa tuna gesi nyingi zaidi ya trilioni 55 *Cubic feet*, gesi hii imepangiwa mkakati wa matumizi yake. Kuna gesi ya kutumia kwenye masuala ya uzalishaji wa umeme, kuna kiwango cha gesi cha kutumia kwa ajili ya viwanda, kuna kiwango cha gesi cha kutumia kwa ajili ya majumbani, kuna gesi ya kiwango cha kutumia kwa ajili ya magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali lake aliloliuliza ni kwamba huo mkakati tunaowasilisha upo wa kimaandishi kabisa, *Gas System Master Plan* ambayo imeainisha matumizi yake na kiwango kimepangwa kabisa hadi 2035. Nachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ndio maana nimesema mchakato wa matumizi yote haya hata sasa hivi kipo kituo Dar es Salaam pale Ubungo, unaweza ukabadilisha gari lako kutoka matumizi ya mafuta ya kawaida *diesel* kwenda kwenye matumizi ya gesi. Tunachofanya sasa ni kutaka kuongeza vituo vingi zaidi ili huduma hiyo ipanuke, kwa hiyo, jambo hilo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimesema hapa kwenye swali la nyongeza la mama yangu Mheshimiwa Mama Kahigi kwamba mipango yote inahitaji uwekezaji wa kutosha. Tunafurahi kwamba Serikali yetu kwa kuungwa mkono, Serikali ya Oman ilikuja hapa na kulikuwa na *MoU* tumeshaisaini lakini zaidi inataka kuisaidia sekta hii ya gesi hasa usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua hilo na umuhimu wa utunzaji wa mazingira pia. Ndiyo maana sasa hivi hii gesi ya *LPG* inayotoka nje ya nchi tumeona tuipangie mkakati kwa muda kwamba lazima nayo iingie kwenye *bulk procurement* kusudi iingie kwa wingi kwa madhumuni ya kushusha bei na kutumika kwa wingi wakati tunasubiri

utekelezaji wa mkakati wa muda mrefu wa kuhakikisha gesi hii yetu ya asilia tunaisambaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie hata mradi wa *LNG* wa Lindi wa kusindika gesi ili kurahisisha usafirishaji wake, sasa hivi mazungumzo yameanza tunatarajia utaanza 2024. Mradi huu ukishaanza tutakuwa na uwezo wa *ku-export* gesi zaidi na kusambaza ndani ya nchi na kujenga miundombinu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira Mgusu, kwa niaba ya Waziri wa Nishati. Tunamalizia swali letu la mwisho kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini aulize swali lake.

Na. 67

Ukosefu wa Mawasiliano katika Baadhi ya Mikoa Nchini

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA aliuliza:-

Maeneo mengi katika Jimbo la Tabora Mjini na Iramba Mashariki hayana mawasiliano ya simu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu katika maeneo hayo ili wananchi wa maeneo hayo wapate mawasiliano?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote inasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 inayoelekeza kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo yote, yakiwemo maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara. Mpaka sasa hivi jumla ya kata 703 katika mikoa yote Tanzania zimefikiwa na huduma za mawasiliano kwa jitihada za Mfuko, ambapo Watanzania zaidi ya milioni nne wanapata huduma za mawasiliano. Tabora Mjini zaidi ya wakazi 12,992 wamefikishiwa huduma za mawasiliano katika Kata za Kabilia na Kampuni ya *Halotel*, Kalunde na Kampuni ya *Vodacom* na Uyui na Kampuni ya *Vodacom* vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali zinazoleta mafanikio hayo bado kuna maeneo nchini yakiwemo baadhi ya maeneo ya Jimbo la Tabora Mjini ambayo hayajafikiwa na huduma za mawasiliano. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itafanya tathmini kamili ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika vijiji vyote vyta kata za majimbo ya Tabora Mjini na vijiji vitakavyobainika kukosa mawasiliano au kuwa na mawasiliano hafifu vitaingizwa katika orodha ya vijiji vitakavyojumuishwa katika zabuni zitakazotangazwa hivi karibuni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa, hili swali limekuwa la muda mrefu na maeneo mengi ya Tabora Mjini zikiwemo Kata za Itetemya maeneo ya Kipalapala, lakini pia maeneo ya Ndevelwa, Ikomwa, Kakola, Uyui na mengine bado yana matatizo mengi sana ya mawasiliano ya simu. Namuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa hili Bunge lina muda mrefu na tutakuwa na siku za katikati za mapumziko ya wiki,

ni lini atakuwa tayari kuongozana na mimi angalau tukakague pamoja miradi hii aweze kuona shida ya wananchi wa sehemu hizo kwenye mambo ya mawasiliano?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali haya ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Adam Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwakasaka kwa juhudii nyingi sana anazozifanya katika kushughulikia kero za wananchi katika Jimbo la Tabora Mjini. Mwenyewe nilmekwishafika pale, Mheshimiwa Mwakasaka na unakumbuka tulikuwa wote tukazungukia baadhi ya maeneo niliyozungumza yamefungiwa minara na nakuhakikishia kwamba niko tayari wakati wowote twende kutembelea maeneo mengine na nitaambatana na timu ya watalaaam kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika Jimbo la Nkasi Kusini vipo vijiji kadhaa ambavyo havina mawasiliano ya simu na nimefanya juhudii sana kumtembelea Mheshimiwa Waziri, mara tatu hivi na kumuandikia barua, vipo Vijiji vya Kasapa, Msamba, Mlalambo, Ng'undwe na vinginevyo. Je, ni lini sasa vijiji hivi vitapata mawasiliano ya simu ambayo ni muhimu sana? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalii hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba amekwishafika Ofisini kwangu mara tatu, kwa ajili ya kufuatilia changamoto ya mawasiliano katika Jimbo lake la Nkasi Kusini. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari orodha ya vijiji ulivyonandikia kikiwemo Kasapa, Msamba na Mlalambo vimekwishaorodheshwa kwa ajili ya kutangaziwa tenda hivi karibuni kabla ya mwezi Mei ili viweze kuingizwa kwenye mpango wa kupewa minara ya mawasiliano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Haonga.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Urambo haikutokea katika orodha ya kwanza iliyotolewa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa maeneo ambayo hayana usikivu mzuri wa simu, je, kwa kuwa yuko tayari kwenda kwa Mheshimiwa Mwakasaka Tabora Mjini, hawezi pia kupitiliza kuja Urambo ili ajionee mwenyewe maeneo yasiyokuwa na usikivu wa simu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali la mama yangu, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwezi Agosti, 2018 tulitangaza orodha ya kata 273 zinazopelekewa minara kwa ajili ya kusambaza mawasiliano na bahati mbaya Jimbo la

Urambo halikupata. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika vijiji ambavyo aliniletea barua ofisini kwangu, vijiji vya Urambo vitaingizwa kwenye mpango wa mawasiliano kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Namhakikishia nitakapokwenda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mwakasaka basi nitapitia mpaka Urambo kuangalia changamoto za mawasiliano, kama kuna jipya tutaweza kuongeza zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga na mwisho Mheshimiwa Yussuf.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mwaka 2016, Serikali ilitutaka sisi Wabunge kuorodhesha vijiji, vitongoji pamoja na mitaa yote ambayo haina mawasiliano na sisi Wabunge tulifanya hivyo, tukaorodhesha vijiji vyetu vingi sana. Jimbo langu la Mbozi niliorodhesha vijiji vingi sana kikiwepo Kijiji cha *Mbozi Mission* ambacho kina hospitali kubwa na taasisi nydingi kama vyuo, hakina mawasiliano, Kijiji cha Maninga, vijiji vingi sana Jimbo la Mbozi havina mawasiliano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue kwa nini Serikali ilituambia sisi Wabunge tupeleke orodha ya vijiji na maeneo ambayo hayana mawasiliano lakini mpaka sasa maeneo hayo hatujapata mawasiliano. Je, Serikali ilikuwa inadanganya Wabunge?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Haonga, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka 2016 tuliwaomba Waheshimiwa Wabunge waorodheshe maeneo mbalimbali ya majimbo yao ambayo hayana mawasiliano. Kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tulifanya kazi maeneo mengi sana na ndiyo maana mpaka sasa hivi kwa

mawasiliano takwimu zinasema Watanzania tunawasiliana kwa asilimia 94. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yake ya *Mbozi Mission* na mengine aliyoazungumza inawezekana kabisa kwenye orodha ambayo tunategemea kuitangaza mwisho wa mwezi huu au mwanzoni mwa mwezi wa tano yakawemo na hivyo atapata mawasiliano. Hiyo ndiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tatizo lilloko Tabora Mjini kwa watoto wetu ni sawasawa na tatizo lilloko Pemba kwa wazazi wao, tatizo la mawasiliano. Mheshimiwa Waziri swali hili uliulizwa mwaka jana na Wabunge wawili na ukaahidi kuja Pemba na ukaja Pemba wewe mwenyewe ukaona tatizo lillopo, hususan kwa Mheshimiwa Maida na Mheshimiwa Bi. Mgeni lakini hadi leo tatizo liko vilevile halijatatuka hakuna mawasiliano katika maeneo hayo. Sasa nini *impact* ya safari yako kuja Pemba zaidi ya marashi ya karafuu? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Yussuf, rafiki yangu sana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilikwenda Pemba mwezi Januari kwa ajili ya kukagua hali ya mawasiliano ya Kisiwa cha Pemba na ni kweli nilikuta hali si nzuri sana. Nikuhakikishie tu Mheshimiwa Yussuf kwamba *impact* ya safari yangu pamoja na marashi ya Pemba vilevile ni kuhakikisha tunawaaletea mawasiliano ili wananchi wa Pemba wawzeze kuwasiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tulioikuta kule ni kwamba kuna hali ya kijiografia ya mabonde na milima, halafu ina minazi mingi sana. Kwa hiyo, badala ya kuweka

mnara mmoja u-supply radius ya kilometra 15 kama kawaida ina supply radius isiyozidi kilometra 4, kwa hiyo, inahitaji minara mingi sana. Kama unavyojua mnara mmoja ni shilingi milioni 300 mpaka 600, kwa hiyo, ni lazima tuwe na uwekezaji wa kutosha. Nakuhakikisha kwamba tutaweka uwekezaji huo kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili wananchi wa Pemba na hasa kwenye kihoteli kile cha chini ya bahari waweze kupata mawasiliano.

MWENYEKITI: Ahsante sana Waheshimiwa kwa kazi nzuri ya maswali na majibu. Tuna matangazo hapa, kwanza tutaanza na wageni ambaao wapo Bungeni asubuhi hii. Wageni walipo Jukwaa la Mheshimiwa Spika, tuna wageni 60 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaao ni marafiki zake anaoshirikiana nao katika ku-support juhudini zinazofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye shughuli za kimaendeleo, hususan, afya, elimu na utamaduni, wakitokea mikoa 10 ya Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa Marafiki wa Dkt. Tulia Taifa, Ndugu Fransisco Pierre Mwinuka. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ambaye ni mfanyakia shara kutoka Kimara Jijini Dar-es-Salaam, Ndugu Alex Fredrick. Karibu sana katika Bunge letu. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ambaye ni kaka yake kutoka Pangani, Mkoa wa Tanga, Ndugu Halidi Mikidadi. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni 130 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaao ni Wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Manyara, wakiongozwa na Ndugu Nicomedji Josephati. (*Makofi*)

Wengine ni wageni 15 wa Waheshimiwa Wabunge, Kanali Mstaafu Mheshimiwa Masoud Ali Khamis na

Mheshimiwa Machano Othman, ambaao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Jimbo la Mfenesini kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi wakiongozwa na Mwenyekiti, Ndugu Rashid Iddi. Karibuni sana wageni wetu kutoka Mfenesini. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, ambaao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma na Mwanza wakiongozwa na Ndugu Fikiri Marumba. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Wageni wengine ni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ambaao ni wanachuo 70 na viongozi 5 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kilichopo hapa Jijini Dodoma ambaao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi zake. Karibuni sana wanachuo 70 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini. (*Makofi*)

Wengine ni wanachuo 74 na viongozi 5 kutoka Chuo cha Uongozi wa Mahakama kilichopo Lushoto Mkoani Tanga ambaao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi zake. Karibuni sana wanafunzi wetu wa chuo kutoka Lushoto. (*Makofi*)

Katibu, tuendelee.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kwa
Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na tutaanza michango yetu na Mheshimiwa Ally Saleh Ally, atafuatia Mheshimiwa John Heche baadaye

Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Salma Kikwete wajiandae.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nitachangia katika eneo moja tu la utawala bora. Kwanza nataka nianze na msemo usemao, "Mgema akisifiwa tembo hulitia maji". Sitaki kuufafanua nitauacha hivyo hivyo tu uning'inie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuanza kwa kusema kwamba kukosolewa ndiko kunakomjenga mtu. Wanaokusifu hawakusaidii sana, ukikosolewa ndipo unapoonaa makosa yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nafanya *research* ya nini nitasema hapa nikaona kwamba *IMF* imetoa taarifa kwamba uchumi wetu utakua kwa asilimia 4 tu mwaka huu na mwaka ujao utakua kwa asilimia 4.2, kinyume na ambavyo tumeambiwa na bajeti inavyosema kwamba utakua kwa zaidi ya asilimia 6. Humu ndani tunajisifu kwamba uchumi unakua, wa pili Afrika, wa tatu Afrika, wa kwanza Afrika Mashariki, hiyo haisaidii kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwa kusema kwamba katika upande wa utawala bora kuna vitu vingi vya kuiga lakini tukifika kuwaambia viongozi wetu kwamba tuige hili tunaambiwa Tanzania haliigi kila kitu. Nitakuja na mfano mdogo tu mmoja mmoja kutoka Ethiopia, ndani ya miaka miwili Ethiopia imetoka kwenye *dictatorship into democracy and now deep into good governance*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano nitakaoutoa ni wa mwanariadha ambaye anaitwa Feyisa Lilesa ambaye alishinda medali ya *silver* kule Rio De Janeiro. Yule anatoka Kabilia la Oromo ambaa ni wengi lakini kule kwao hawana nafasi ya kiuongozi. Alipokuwa kule *in protest* akafanya alama hii (*hapa Msemaji alionesha alama*) kuonesha kwamba Waoromo hawana uhuru ndani ya nchi yao wenywewe. Matokeo yake akabakia kulekule Brazil kama mkimbizi kwa miaka miwili. Jana amerudi kwao na ameitwa na Waziri Mkuu

ameambiwa njoo nyumbani hata kama uliikosoa nchi yako ukiwa nje, rudi nyumbani uje ujenge Taifa. *On top of that akarudishiwa zawadi yake ya Olimpiki ambayo alikuwa apewe ya dola 17,000, look at that level. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa Profesa Assad amekwenda nje na amesema maoni kuikosoa Serikali, tunasema uzalendo, hautakiwi ukosoe nje ya nchi. Utakosoaje ndani ya nchi wakati hakuna nafasi ya kukosoa? Utakosoaje ndani ya nchi wakati uhuru wa kujieleza na uhuru wa kujikusanya haupo kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukisema utawala bora tutizame na mengine. Utawala bora siyo maneno tu, utawala bora lazima uendane na haki, usawa, uadilifu na imani, lazima uendane na Katiba na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza mifano ya kuonesha kwamba *we still have a lot to do* katika utawala bora. Nianze na uhuru wa kujikusanya, uhuru wa siasa. Kwa mujibu wa Katiba ya nchi hii na sheria, hakuna mwenye uwezo wa kusema kwamba nasimamisha siasa mpaka wakati wa uchaguzi, hakuna kisheria wala kikatiba. Kwa mujibu wa sheria hakuna mwenye uwezo wa kusema kwamba nasimamisha siasa mpaka wakati wa uchaguzi, hakuna kisheria na kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vipo kufanya siasa wakati wowote. Hata kauli ile itoke juu kiasi gani, ni kauli batili, haramu, *mutlaq*. Hata kama imetoka juu kiasi gani, huwezi kuwazuia wananchi wako wasifanye siasa eti kwa sababu wajenge nchi. Nchi ni pamoja na kufanya siasa na kukosoa ndiyo kujenga nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vyama vingine vyaa siasa haviruhusiwi kufanya mikutano na Polisi mpaka sasa wanashindwa hoja. Hoja yao ni *simple* intelijensia. Intelijensia yenye we hainonyeshi kama ya kisayansi ya kisasa. Aah, maana yake Chama cha *CUF* kitazuia vyama vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano uliotolewa, *CUF* watazuia *ACT* wasifanye mikutano. Hivi *CUF* ni chama cha fujo? Hivi huoni kwamba unakiweka pabaya Chama cha *CUF* kwamba ni chama cha fujo kinataka kuzuia mikutano ya vyama vingine? Au mnataka kukifuta na *CUF* vilevile! Kwa sababu kama chama kinafanya fujo kila siku za kuzuia mikutano ya vyama vingine nacho kifutwe? Siamini kama *CUF* wanafanya hivyo. Hawafanyi hivyo kwa sababu ni *their interest* vile vile na wao wakifanya mikutano yao wengine wasitumike kuwazuia. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni jambo ambalo sioni kama linaendana na utawala bora, nalo ni taasisi zetu za Kiulinzi kupokea zawadi. Jana nimeona Polisi wanapokea vifaa gani sijui kutoka *NMB*. Mara utasikia wamejengewa vibanda, mara sijui vitu gani *how can you do that?* Mtu ambaye anakuzawaidia utawezaje kum-counter? Utawezaje kum-check akifanya makosa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Polisi au Jeshi ama wengine wanawekewa *vote*; kwa nini waende wakajidhalilishe kwa kupekewa vibanda viwili, vitatu vya kujengwa barabarani? Huo siyo utawala bora, kwa sababu huyo ambaye amekuzawadia huwezi tena kumkagua. Kwa mujibu wa sheria yetu ya rushwa, anayepokea na anayetoa wote ni rushwa. Kwa hiyo, Polisi nao wanapokea rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Miswada; tunakuja hapa ndani ya Bunge letu, Miswada mingi utaona hata haitoi fursa nyingine za kisheria. Unashangaa wanasheria wetu wanaoleta Miswada Bungeni wanayo dhana ya utawala bora ndani ya akili zao? Kama hawana, kwa nini basi muwaache walete Miswada kila siku. Ndani ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria tunasema mbona hapa hakuna fursa ya rufaa? Mbona hapa hakuna kitu gani? Utawala bora bado haujaingia katika akili zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulisemea ni suala la TAKUKURU. Watu wanashitakiwa kwa

very grievous offences kwa mfano utakatishaji fedha au uhujumu uchumi, lakini wanatangaziwa dunia nzima, wanahukumiwa kabla hawajafika mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimeona kesi moja, mama mmoja anashitakiwa, anapelekwa mahakamani, TAKUKURU wanatoa *Press Conference*. Tayari umeshamhukumu mtu yule katika *public*. Kwa hiyo, huu siyo utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni muundo wa kuhoji watu hadharani. Umekuwa mtindo sana katika nchi yetu ya Tanzania kwamba Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa anaweza kuwaita watu akawahoji katika hadhara na hata mkuu wetu wa nchi anafanya. Kusema kweli taratibu za kumhoji mfanyakazi zipo; taratibu za kumkosoa mfanyakazi zipo, zimewekwa kisheria. Sasa kwa nini umwite hadharani, uende ukamuue kwa *pressure* na kitu gani, unamdhaliisha mbele za watu ajibu maswali papo kwa papo wakati ungeweza kuwa naye ofisini? Huu siyo utawala bora. Siyo utawala bora kabisa kwa sababu humtendei haki mfanyakazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwengine, juzi nimeona, nafikiri Mkuu wa Mkoa wa Iringa, anamwambia mtu wa benki aende akafungue benki aje na nyaraka siku ambayo siyo ya kazi. Aende akafungue achukue nyaraka wakati ambao siyo wa kazi. Anamwambia wewe si ndio Meneja bwana, nenda kafungue lete nyaraka hapa. *This is not utawala bora. Jamani, utawala bora deserves more than that.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwangu mimi, utawala bora ni *financial governance*. Ripoti ya CAG inaonyesha kwamba utawala bora *is far from dream to us*. Madudu ambayo yanaendelea ndani ya Serikali katika upande wa fedha yanatisha. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ally Saleh, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Heche na baadaye Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami leo niweze kuchangia kwenye hizi bajeti mbili za TAMISEMI na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana CAG Prof. Assad, kwa kweli Prof. Assad ameitendea haki na ametendea haki uprofesa wake na ameonyesha ni kwa nini hasa kulikuwa na wingu la kutaka kumchomoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri Serikali yenu ambayo kwa miaka miwili imekuwa ikijitangaza kwamba inapiga vita ufisadi. Mtu ambaye alitakiwa kukumbatiwa na Serikali na kulindwa kwa gharama zote ni huyu Prof. Assad ambaye ameleta taarifa ambayo mpaka mama yangu kule Kijijiini anasema sasa nimejua kwa nini CAGyupo na CAGanafanya kazi gani. Kwa hiyo, ningependa nianze na hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimnukuu kidogo Mwalimu Nyerere kwenye kitabu chetu cha TANU na Watu Wetu. Anasema, "Viongozi wa TANU hawana budi watokane na watu, kwa sababu TANU ni chama cha watu na sababu ya pili ni kwamba kazi ya TANU ni kuwatumikia watu. Sitaki kueleza mambo yanayofanywa na Serikali kama vile kujenga shule, hospitali, barabara na kadhalika. Nataka kusema juu ya shida za watu za kila siku." Mwisho wa kunukuu. Mengine tuendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ambayo Serikali inakutana na shida za watu za kila siku ni kwenye Halmashauri zetu. Halmashauri ndizo zinasozimamia shule ambazo watoto wa wananchi masikini wanasoma; sio watoto wetu hapa. Hakuna Mbunge hata mmoja humu anasimama aseme mtoto wake anasoma kwenye shule za msingi za Serikali, hayupo hata mmoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hospitali, ndiyo kwenye watu wetu, wanakwenda kutafuta madawa kule na kutibiwa...

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Akina mama wanajifungua kule.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Heche

T A A R I F A

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mdogo wangu hapo, asiseme kwamba hakuna Mbunge ambaye anasomesha. Mimi kuna wajukuu zangu wanasoma kwenye hizo shule. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, naomba uendelee.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, unilindie muda wangu ni kidogo nizungumze matatizo ya nchi, tafadhali.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu sina sababu ya kumjibu kwa sababu...

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi na shule za sekondari zipo kwenye Halmashauri, hospitali zinasimamiwa na Halmashauri, matatizo ya kila siku ya watu ambayo Mwalimu Nyerere aliyasema kwenye kitabu cha TANU yapo kwenye Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza na Halmashauri yetu ya Tarime, Kwa masikitiko makubwa; na nimpongeze Mheshimiwa Jafo kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya na aangalie hili. Halmashauri yetu ya Tarime, huu ni mwezi wa Nne vikao vimesimamishwa kinyume cha utaratibu wa kisheria. Hili suala la utawala bora la kudhibiti Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanajifanya vitu vyovyo ambavyo wanaamua, eti kwa kisingizo kwamba kuna ujisadi umefanyika. *Fine!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ujisadi umefanyika, kuna watu waliofanya huo ujisadi. Mkuu wa Mkoa achukue hatua kwa hao watu waliofanya ujisadi. Sasa leo unazuia vikao vya Halmashauri; *Finance Committee* haikai, Baraza la Madiwani halikai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tulikuwa na watoto 1,030 wameshindwa kwenda sekondari tangu mwezi wa Kwanza, hakuna vyumba vya madarasa, tukatenga zaidi ya shilingi milioni 250 kwenda kujenga madarasa. Hizi pesa tunazo, ni pesa za wananchi wa Tarime ambao wamekusanya wenyewe kwenye nyanya na vitunguu, tunazo zipo kwenye akaunti. Mkuu wa Mkoa amezuia kwamba vikao havikai, anataka sisi tuwe tunamwandikia barua yeye kumwomba pesa kinyume cha utaratibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kisheria, watu wenyewe mamlaka ya kugawa pesa ni hili Bunge na Bunge la wananchi ambalo ni la Halmashauri pale Wilayani. Sasa Mkuu wa Mkoa anataka kujigeuza *Pay Master General* wa Mkoa. Yeye ndio anataka sisi tuwe tunamwomba. Nimesema hakuna siku tutamwomba hizo pesa. Mwangalie kama hizi hujuma mnazowafanya wananchi wa Tarime kwa kuwabagua kwa makusudi ni sawa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kama wateule wa Rais; leo hapa Assad amezungumza kuhusu upotetu wa zaidi ya shilingi bilioni 16 kwenye *uniforms* za Askari, mbona hamjazuia Jeshi la Polisi lisifanye kazi? Jana Gilles Muroto alikuwa anasema hapa atapiga watu mpaka wachakae,

mbona hamjawazuia wasifanye kazi kwa sababu kuna ufisadi kwenye Jeshi la Polisi. Amezungumza mambo mengi hapa, mbona hamjazuia hao watu wasifanye kazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi simtetei mwizi na nipo *clear*, na Mwenyekiti wa Halmashauri yangu katika kupigania hili aliwekwa ndani siku 11 kwa sababu ya kupigania ufisadi uliofanywa na wateule walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Jafo naomba atengue agizo batili hili, wananchi wa Tarime wapate haki ya Baraza lao la Madiwani ku-deliberate kwenye *issue* na wafanyiwe maendeleo. Hilo la mwanzo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nije kwenye ajira. Tumeona hapa vijana wetu wako vyuoni wanasoma. Hawa vijana wanahitaji ajira. Kila siku nyie mnazungumza humu. Nyie mmeajiriwa na wananchi, mnalipwa mamilioni ya pesa, wanahitaji ajira hao. Watoke mwatengenezee mazingira mazuri kama ni kujajiri, wajajiri na mikopo iwepo. Kama ni ajira za Serikali, zitoke; kama ni *private sector*, iajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka minne mfululizo Serikali hii inayotudanganya inakusanya kuliko wote hajaajiri wananchi. Juzi mmetangaza ajira 4,000 za Walimu, vijana walio-*apply* ni 11,300. Mnawenza kuona *crisis* iliyopo. Mnatangaza ajira 4,000 wanajitokeza vijana 11,300 na nyie mpo hapa mnasema kila kitu kinaenda sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya. Bajeti iliyopita tulitenga shilingi bilioni 561, pesa ambazo mmepeleka mpaka sasa ni shilingi bilioni 89 peke yake. Hakuna madawa, hakuna *gloves* wala nyazi. Serikali yenu inayokusanya kuliko zote, kwenye madawa mmetoka hapa na *rhetoric* za kisiasa mmepeleka chini ya asilimia 15. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema ninyi ni Serikali ya viwanda; kwenye viwanda mlitenga shilingi bilioni 90, pesa ambazo zimekwenda zimetolewa na Serikali kwa ajili ya

maendeleo ya viwanda ni shilingi bilioni 5.4, asilimia sita peke yake. *No wonder* mnasema cherehani tano ni viwanda, kwa sababu kama shilingi bilioni 90 mmetenga, mnaapeleka shilingi bilioni 5.4 kwa nini msiseme kiwanda cha cherehani ni kiwanda na gongo ni kiwanda. Kwa nini msiseme hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinaajiri Watanzania asilimia 70, kinatoa chakula kwa Watanzania asilimia 100, kinatoa malighafi za viwandani asilimia 80; mmetenga shilingi bilioni 98.1, zimekwenda shilingi bilioni 42. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maji ambayo mmesema mnamtua mama ndoo kichwani, Mfuko wa Maji tulipitisha hapa kwa mbwembwe mkapigiana makofi, shilingi bilioni 299, pesa zilizokwenda kutoka kwenye Mfuko wa Maji ni shillingi bilioni 1.62... (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa...

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Tulia Mheshimiwa Waziri utapata nafasi ya kujibu, subiria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Tulia.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa

Heche, katika bajeti ya mwaka 2018 tulitengewa shilingi bilioni 100,058 katika Mfuko wa Maji. Mpaka mwezi Februari tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 93. Kwa hiyo, namwombe tu ajiridhishe katika kuhakikisha halipotoshi Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche taarifa hiyo.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sources za maji zipo tatu...*

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sizungumzii pesa za wahisani za kutoka India. Mimi nazungumzia...

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. JOHN W. HECHE: Mimi nazungumzia pesa za Mfuko wa Maji na Mheshimiwa Waziri anajua ninachokzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ambayo tunakuja kuitisha hapa kila mwaka, ina maana tuna matatizo ya wananchi tunataka kwenda kuyatatua. Kama tutakuja hapa watu watalipwa pesa, halafu utekelezaji ni zero; *general budget* utekelezaji ni chini ya asilimia 30. Leo tunakwenda kuitisha bajeti nydingine kwa sababu gani? Hapa Mawaziri wamejua kila siku wakisimama... (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: ...ni kutukana CHADEMA mnapiga makofi mnasahau matatizo yaliyowaleta hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu. Tangu kuwepo na elimu bure, *enrollment* kwenye shule ni asilimia 17...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: ...lakini miundombinu ni asilimia moja peke yake mme-*improve*. Matundu ya vyoo zaidi ya asilimia 63. Kwa wasichana hakuna, vyoo wanajisaidia vichakani... (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche muda wako umemalizika.

MHE. JOHN W. HECHE: Matundu ya vyoo kwa wavulana hakuna; hakuna mabweni... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Umemalizika muda wako Mheshimiwa Heche.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Je, mnapaswa kuchaguliwa tena au mwondolewe kwa... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche muda umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo baadaye Mheshimiwa Salma Kikwete ajiandae.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mungu na pia nishukuru Wabunge wote kwa salamu za pole mlizotupatia wakati tulipofiya na mama yetu mzazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo wamefanya na pia Waziri

Mheshimiwa Jafo, unafanya kazi kubwa sana pamoja na mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika, unatumikia vyema chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niguse suala dogo ambalo alikuwa anachangia rafiki yangu Mheshimiwa Heche kuhusiana na Mkuu wa Mkoa kuingilia kati utendaji wa Halmashauri katika Jimbo lake. Ukienda kwenye sheria, wanaotumia Wakuu wa Mikoa, *The Regional Administration Act, 1997* kipengele cha 5(3) naomba ninukuu, “*For the purpose of this section it shall be the duty of the Regional Commissioner to facilitate and assist local government authorities in the region to undertake and discharge their responsibilities by providing and securing the enabling environment for the successful performance by them of their duties and functions.*” (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa ndio mwakilishi wa Rais katika Mkoa na sheria imempa mamlaka ya kuingilia ili kuona kwamba *performance* ya Halmashauri inafanyika. Kwa hiyo, kitendo kilichofanyika ni chema na Halmashauri yake inapata *service levy* kutoka kwenye mgodi *1.5 billion*. Wanapata *corporate social responsibility* shilingi bilioni tano.

Kwa hiyo, kama kuna hali ya kifisadi ambayo imefanyika na tume iliundwa, kwa hiyo, ni sahihi kuhakikisha kwamba anadhibiti matumizi ya fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya suala hilo, naomba niingie kwenye suala letu la Mkoa wa Katavi. Bajeti ya *TARURA...*

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Bajeti ya *TARURA...*

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. RICHARD P. MBOGO: ...tumepangiwa shilingi bilioni 3.6.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe...

MHE. RICHARD P. MBOGO: Tumepangiwa shilingi bilioni 3.6.

MHE. JOHN W. HECHE: Samahani tuvumiliane. Nina haki ya kutoa taarifa.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hiyo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo, tafadhali dakika moja

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Tusikilizane. Mheshimiwa Mbogo, subiri. Sasa nyie mnaongea, huyu mtu anatoa taarifa.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Bado ni ndogo sana bajeti hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo, subiri kidogo.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, umenipa nafasi ya kutoa taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche ongea wewe siyo wenzako. Wewe ndio unatakiwa utoe taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetulia nakusikiliza wewe.

MWENYEKITI: Haya sema hiyo taarifa.

TAARIFA

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hii; na iwe *very clear*. Sisi hatujakataa Mkuu wa Mkoa kuchunguza, kufanya chochote kwenye Halmashauri. Tunachokataa ni kuzuia vikao vya wananchi *vi-deliberate* kwenye *issues* za maendeleo ya wananchi. Ndicho tunachokataa. Hana sheria inayompa mamlaka hayo ya kuingilia na kujigeuza *Pay Master General*, hakuna sheria inasema hivyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo, taarifa hiyo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vikao vinakaa halafu havitendi haki ipasavyo, akizua ni sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, muda wangu naomba uulinde, utanipa na *bonus*.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia kuhusu *TARURA*; kwa Mkoa wa Katavi tumepangiwa bilioni 3.6, ni fedha ambayo haitoshi. Tuna mtandao wa barabara kilometra 2,563 lakini ambazo zilihakikiwa na ile tume ni kwenye 2,400 na kitu, tofauti ni ndogo sana. Hata hivyo, katika mtandao huu kilometra 24 ndiyo ni lami ambayo ni asilimia moja, kilometra 511 ambayo ni asilimia 20 ndiyo barabara ya changarawe na kilometra 2,027 ambayo ni asilimia 79 katika Mkoa mzima wa Katavi ni za udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii ya ufinyu wa bajeti ambayo tunatengewa Mkoa wa

Katavi, naomba sana Mheshimiwa Waziri Jafo na watendaji wa *TARURA* na kama wako humu ndani naomba walichukue hili; randama hii wakaiboreshe watuongezee iwe angalau bilioni tano. Kwa sababu Mkoa wa Katavi tunatunza mazingira, tuna mvua nyingi tunapeleka maji Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa na kadhalika, sasa barabara hizi kipindi cha masika hazipitiki.

Kwa hiyo tunaomba tuongezewe toka bilioni 3.6 ifike angalau bilioni tano. Ilishangaza sana, kuna halmashauri karibuni 11 zinazidi mkoa mzima, kwa hiyo tunaomba suala hili Mheshimiwa Waziri Jafo na timu yake na watendaji wa *TARURA* walifanyie kazi, bajeti sio Biblia, bajeti sio Msahafu inaweza ikaboreshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusiana na mapato kwenye halmashauri zetu. Halmashauri za Mkoa wa Katavi, Halmashauri ya Nsimbo ambayo tunalima tumbaku pamoja na Chunya, kampuni za ununuzi wa tumbaku zimegoma kutulipa tozo kutokana na kudai fedha zao za marejesho ya *VAT* (*VAT refund*). Kwa hiyo, tuombe kama wahusika wa Wizara ya Fedha na wa TAMISEMI watusaidie ili tuweze kupata fedha na tutekeleze miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie suala la utawala bora; hii Sheria ya *Regional Administration Act* ya 1997 imewapa madaraka Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuweza kutoa amri ya kumkamata mtu. Kuna wakati mwengine utekelezaji wake umekuwa hauendani na sheria inavyosema. Niombe Waziri wa Utawala Bora pamoja na Serikali kijumla na tunajua muda mrefu semina zimetolewa, mafunzo na maonyo mbalimbali kwa watendaji wetu watekeleze sheria hii ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mzuri, naomba *ku-declare* kabisa, nina mzee wangu anaitwa Ernest Wamryoma alikamatwa tarehe 24, Machi akiwa anatetea ardhi yake aliyoshinda Mahakama Kuu ya Ardhi na Mahakama Kuu ya Ardhi Kikatiba, Ibara ya 107A(1) ndiyo chombo chenye kutenda haki. Kwa hiyo Mkuu wa Wilaya ya

Kigamboni, Mheshimiwa Sara Msafiri hajamtendea haki mzee Ernest Wamryoma kwa kumyanyasa na ameshinda Mahakama Kuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Lukuvi, katika masuluhihi yake ya matatizo ya ardhi huwa anasema jambo lolote ambalo limeamuliwa na mahakama lisiletwe kwenye ofisi yake. Sasa niombe Waziri, Ofisi ya Rais suala la Utawala Bora, naomba asaidie Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni aache kumsumbuu huyu mzee, kashinda Mahakama Kuu na aliyemshinda alikuwa amemkaribisha tu, aache mahakama ambavyo imekwishaamua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Uchaguzi wa Vijiji na Serikali za Mitaa mwaka huu. Sasa kwa Nsimbo tuna Makazi ya Wakimbizi ya Katumba, tuombe mtoe mwongozo jinsi gani ambavyo kutokana na hadhi ya makazi ipo Katumba, Mishamo na Ulyankulu, namna gani uchaguzi wa vijiji utakwenda kufanyika na tuna sheria ya upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusiana na wakimbizi ambapo tayari bado maeneo haya yako chini yao. Kwa hiyo tuombe tupate mwongozo jinsi gani uchaguzi utakwenda kufanyika kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na madeni ya watumishi; ukiangalia hesabu za halmashauri utakuta kuna *receivable*, wanadai na kuna *payable* wanadaiwa na watumishi kutokana na maslahi yao mbalimbali, hususan uhamisho na madaraja waliyopanda. Kwa hiyo tuombe watumishi wetu katika halmashauri Serikali itoe fedha ili waweze kulipwa malimbikizo yao ambayo yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusiana na uchangiaji wa jana wa kaka yangu, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, alizungumzia *consequences* kwenye *SGR*, kwenye ndege, kwenye *Stiegler's Gorge*. Uwekezaji wowote una *return on investment; Air Tanzania ita-promote* utalii na kuanzia baada ya miaka minne ijayo itakuwa inafanya kwa faida, hizo ndiyo *positive consequences*. Kwenye *SGR*

tutakwenda kunyanya uchumi wa nchi yetu kwa kubeba mizigo toka kwenye nchi za jirani ambazo ni *landlocked*; Burundi, Rwanda, Kongo na Zaire. Kwa hiyo uchumi wa nchi utaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye umeme, umeme wa maji ndiyo umeme ambao ni nafuu kuliko umeme wowote duniani. Naibu Waziri wakati anajibu swali la gesi kaaeleza gharama ya gesi ni dola 5.1, kwa hiyo utaona jinsi gani kwamba umeme wa gesi uko juu kuliko ambavyo utakuwa umeme wa maji. Kwa hiyo *consequences* za maamuzi ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeyafanya ni *positive* kwa ajili ya wananchi wake na maendeleo ya taifa kiujuila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo, tunaendelea na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete na baadaye Mheshimiwa Mariam Kisangi na Joel Mwaka wajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama ili niweze kuchangia kwenye Wizara hizi ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichukue nafasi hii kukishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi, kikiongozwa na jemedari wake Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inafanyika katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba nitoe pongezi zangu za dharti kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wetu wa TAMISEMI kwa kazi kubwa na nzuri ambazo anazifanya, lakini sambamba na hilo kwa uwasilishaji wake ambao ni mahiri sana, pamoja na kwamba muda kwake ulikuwa ni mfupi, lakini nimpongeze kwa uwasilishaji wake na kazi nzuri ambazo anazifanya kila kona ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais mara alipochaguliwa au kabla ya kuchaguliwa aliwaahidi Watanzania kufanya kazi kwa umahiri na weledi mkubwa sana. Hii inaonesha kwamba Mheshimiwa Rais anawatumikia Watanzania. Ukiangalia kwenye kipindi ambacho kinasema tunatekeleza na kishindo cha Awamu ya Tano unaona jinsi kazi ambavyo zinafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ukiangalia tunatekeleza, unaona kila kona ya mkoa wa nchi yetu, kila wilaya, kila eneo na Mawaziri wote kwa pamoja wameshikamana kufanya hizo kazi ambazo zinaonekana katika nchi yetu; ama kweli Tanzania ya viwanda inaonekana na tunaamini itakapofika mwaka 2025 kwa kweli uchumi wa kati utafikiwa kabla ya huo mwaka ambao tunausema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa machache tu naomba niyaseme yafuatayo ambayo Mheshimiwa Rais na Serikali yetu imetekeleza; ujenzi wa *Stiegler's* ambao utatusaidia kupata umeme wa bei nafuu na sisi tunaelekea kwenye nchi ya viwanda, ni lazima tuwe na umeme wa bei nafuu. Sambamba na hilo, kuna *standard gauge*, itarahisisha usafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine, vilevile, itapunguza matatizo ya barabara kwa sababu mizigo mingi inaposafirishwa kuititia barabarani maana yake ni kwamba barabara inaharibika na kila baada ya muda mfupi inabidi tutengeneze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, sisi tunahitaji watalii. Amenunua ndege ambazo sio kwamba watatumia watalii pekee bali hata sisi wenyewe ndani ya nchi tutazitumia. Na tunashuhudia, Jumatatu asubuhi watu wengi, kila mtu anahitaji ile ndege na watu wengine wanakosa, na hizo ndege watu wote tunazipanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ameanzisha Mahakama ya Mafisadi. Hili nataka nilisemee; Mahakama ya Mafisadi ilikuwa na umuhimu kwa sababu ni agenda ambayo ilikuwa imezungumzwa kwa kasi sana lakini Rais wetu

na chama chetu ni sikivu, chama chetu kimetengeneza ilani ya kuvishughulikia hivi vitu na kweli Rais wetu kwa sababu ni msikivu vyote amevifanya, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna suala la elimu bure, elimu hii imeleta chachu ya watoto wengi wa Kitanzania kuingia shulen. Kila kwenye mafanikio hakukosi upungufu na upungufu ndiyo chachu ya maendeleo. Kwa hiyo sasa tunachotakiwa ni kujipanga juu ya watoto wengi waliopo madarasani kwetu ambao wanakosa huduma muhimu za msingi. Na zote hizi zimeelezwa na jinsi ya kutekelezwa vilevile zimeelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusiana na elimu bure naomba nijikite kwenye suala hilohilo, tunaanza elimu ya awali. Kwenye elimu ya awali ilani inasema kila kwenye shule ya msingi kuwe na darasa la awali na hii imetekelzeza kwa kiasi kikubwa. Jambo ambalo nataka nishauri, kwenye elimu ya awali ni lazima kuwe na Walimu ambao wana weledi wa kuwafundisha wale watoto wa darasa la awali kwa sababu kabla ya hapo tulikuwa hatuna hicho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake watoto walikuwa wanakwenda kwenye zile *private schools* wakitoka pale wakiingia darasa la kwanza matokeo yake wale wanaonekana kwamba wana maarifa zaidi kuliko hao kwa sababu hawakupitia elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti wanasesma hakuna mtu ambaye uwezo wa akili ni mdogo isipokuwa wanatofautiana katika kuelewa, mwingine anaalewa kwa kiwango cha chini, mwingine cha kati na mwingine kwa kiwango cha juu.

Kwa hiyo hii elimu ya awali imesaidia sana, hapa ni lazima wawepo walimu wenyewe weledi sio Walimu wapo basi anachukuliwa huyu nenda kafundishe elimu ya awali, hii sio sawa na haileti afya kwa suala zima la elimu na tukiamini kwamba elimu ndiyo msingi wa kila jambo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nizungumzie suala la elimu ya msingi; kwenye elimu ya msingi hapa ni lazima tuwaandae watoto wetu tangu mwanzo kuona kwamba hawa watoto wetu je, wanafaa kuwa akina nani, tuwaandae watoto kuwa Walimu kwa sababu kila kitu kinatengenezwa. Sasa kitu ambacho tunakiona unakuta kwamba, kwa sababu watoto hawaandaliwi kuwa Walimu ukienda ukauliza nani anataka kuwa malimu kila mtu ameshusha mkono chini, hataki kuwa Mwalimu kulingana na kutowaandaa na kulingana na mazingira yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilohilo la Walimu, wamesema kuna Walimu wengi, ajira zimetoka; je, kati ya hizi ajira zilizotoka ni Walimu wangapi? Pamoja na kwamba wanasema wengine wamepelekwa kwenye eneo la wenye ulemavu, je, kwenye ulemavu mmeangalia watoto wenye usonji? Kwa sababu watoto wenye usonji ni wenye mazingira magumu, mtoto mwenye usonji unaanza kumtambua akiwa na umri wa miaka mitatu na ni watoto ambao kukaa nao ni mtihani, naomba tufanye utaratibu tuwaandae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali haina shule hata moja yenye watoto wenye usonji. Al Muntazir wameanzisha hili darasa la watoto wenye usonji, hakuna ubaya Serikali ikashirikiana na Al Muntazir kuwasaidia watoto wenye usonji kwa sababu kila mtoto anayo haki ya kupata elimu kwa wakati muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Walimu wa sayansi. Tatizo hili ni kubwa sana hapa nchini. Ni lazima tutengeneze mkakati wa kuwaandaa Walimu wa sayansi tangu ngazi za awali, hasa kwenye shule za msingi, tuwaandae watoto tujue huyu atakuwa Mwalimu wa sayansi. Kwa hiyo tuanze maandalizi haya mapema, hatimaye tutaondoa tatizo la Walimu wa sayansi. Pamoja na kwamba wameajiriwa Walimu zaidi ya 1,900, kati ya Walimu hawa je, Walimu wangapi ni Walimu wa sayansi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kama alivyosema pale mwanzo, maandalizi ya Walimu yaanze

mapema baada tuwe na mkakati kwamba ndani ya miaka ama mitano au kumi tuwe na kazi ya kuwaandaa Walimu hawa ili tuwe na Walimu bora kuanzia elimu ya awali, elimu ya msingi mpaka elimu ya sekondari, hapa tutakuwa na matokeo mazuri na kama tunataka hayo maboresho. Tunaamini Serikali yetu ni sikuvi haya yanawezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna suala zima la ukaguzi; nimepitia sikuona kabisa eneo la ukaguzi, au labda pengine nime-*overlook*, sikuona. Suala la ukaguzi ni muhimu, ni lazima kuwepo na Wakaguzi ili waweze kufuatilia kazi za Walimu, hatimaye ndiyotutaona mafanikio ya elimu yetu. Hili kwa kuwa halipo ni lazima liwekwe kwa ajili ya ubora wa elimu ya watoto wa nchi yetu, bila ukaguzi hakuna kitu, nazungumza hayo kwa uzoefu wa kazi yangu ya ualimu niliyoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, hongereni sana. Mheshimiwa Dkt. Magufuli endelea kufanya kazi, tuko nyuma yako. Ahsante sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Salma Kikwete, tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Kisangi, baadaye Mheshimiwa Joel Mwaka na Mheshimiwa Felister Bura ajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kujadili hoja hii ya TAMISEMI. Kwanza napenda kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ilivyoweza kutekeleza llani yake ya Chama cha Mapinduzi; kwa kipindi hiki cha miaka mitatu tumefikia asilimia 90, hali ambayo inawafanya wenzetu wa upande wa kule waanze kutetemeka. Nasema Chama cha Mapinduzi kiko vizuri na Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyoko madarakani inafanya kazi nzuri na tutaona 2020 tumejipanga vizuri, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi watatawala katika Bunge hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimponeze Serikali yangu na nimponeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli kwa utendaji wake mzuri uliotukuka wa kujali wananchi wake katika maeneo mbalimbali bila kujali jimbo hili ni la nani, jimbo hili ni la Chama cha Mapinduzi, jimbo hili ni la Upinzani, Mheshimiwa Rais wetu anafanya kazi kwa ajili ya wananchi wake bila kuangalia tofauti za chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme nchi yetu, au Serikali yetu ni kweli inaendeshwa katika misingi ya utawala bora, misingi ya utawala bora inazingatiwa na ndiyo sababu tuko hapa. Utawala bora uko katika maeneo mbalimbali; uko katika viongozi lakini uko katika wale wanaoongozwa pia. Ili nchi yetu iwe vizuri, wote tunatakiwa tuendeshe nchi yetu na tuishi sisi kama viongozi kwa kuzingatia misingi, maadili, kanuni na taratibu za nchi yetu, klongozi ambaye atakwenda tofauti na maadili ya nchi, huyu hatakubalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye hoja ya TAMISEMI; kwanza napenda nimponeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, Naibu Mawaziri wote kwa kazi nzuri. Kwa kweli Serikali yetu imefanya kazi nzuri kwenye ujenzi wa hospitali za mikoa na wilaya wameweza kutoa karibu bilioni 1.5 kwa kila mkoa ambao hauna hospitali za mikoa na zile za wilaya. Pia ujenzi wa zahanati na ukarabati wa vituo vya afya Tanzania nzima, karibu vituo 325 ambavyo umegharimu bilioni 184.67, si jambo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika maboresho ya Jiji la Dar es Salaam kwa kweli Jiji la Dar es Salaam sasa hivi limefanyiwa maboresho makubwa sana, lazima tuseme, ni ukweli usiopingika. Dar es Salaam ukienda kila kona unakutana na ujenzi wa barabara, sio kazi ndogo iliyofanywa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo, sasa nakuja kwenye mchango wangu ambapo nitajikita moja kwa moja katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa

TAMISEMI, ukurasa wa 29, 83 na 87. Naanza na ukurasa wa 29 wa maboresho ya huduma za afya, kweli hospitali na vituo vya afya zimeboreshwa tena siyo vile vya Serikali tu, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wake wa llani kwa kutumia Mfuko wa Bima ya Afya umeweza kukarabari hospitali binafsi pia. Kwa kweli leo hii ukienda zahanati ya binafsi siyo ile iliyokuwa mwaka 47, utakuta ina miundombinu mizuri na iko vizuri kwa kweli zahanati za Mkoa wa Dar es Salaam zipo vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukarabati huo, niombe Serikali iiangalie kwa jicho la huruma Zahanati ya Mbagala Zakhem. Kweli Mbagala Zakhem kuna tatizo la ardhi kwamba eneo ni dogo lakini kama Halmashauri tumeboresha Hospitali ya au Zahanati ya Maji Matibu na Charame ili kusaidia wale wananchi lakini ukweli utabaki kuwa ukweli jiografia ya Mbagala na jinsi Mji wa Mbagala unavyokuwa kwa kasi Hospitali ya Zakhem iko barabarani hivyo inapotokea majeruhi anapelekwa pale baadaye anapelekwa Temeke. Huwezi ukamtoa mtu Mbagala Zakhem ukamrudisha Mbagala Maji Matitu akatokee wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali, pamoja na mambo yote mazuri tunayofanya tuiangalie hospitali ile kwani kutwa inapokea majeruhi, watu ambao wamejaa pale Mbagala, wafanyabiashara, wajasiriamali na watu wote wanaopata matatizo wanakimbilia pale. Kwa hiyo, Hospitali ile ya Mbagala Zakhem imezidiwa pamoja na kwamba kuna zingine pembezoni lakini ile bado inauhitaji wa aina yake, niombe Serikali iongeze nguvu kusaidia eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 83, Tume ya Utumishi ya Walimu, niseme ukweli kwamba bado lipo tatizo kwa walimu. Walimu wanadai hela zao za promosheni mpaka wengine wanafikia kustaafu lakini bado wanadai. Pia walimu wanateseka bado wanadai nauli zao. Ninao mfano wa walimu wa Halmashauri ya Temeke, wale ambao wamestaafu mpaka leo hawajalipwa nauli zao na

hela zao za promosheni. Walimu wale wanahangaika wakati wameitumikia nchi kwa uadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa mwalimu ambaye nimetoka kwenye elimu ya msingi, walimu wenzangu wananiuliza yaani wewe umefika huko mjengo unatusahau? Nawaambia sijawasahau na ni wajibu wangu kuwasemea. Nirombe Serikali ichukue hatua na ishuke kwenye Halmashauri iwaalize tatizo ni nini mpaka hawa walimu hata anayemaliza leo na bajeti zipo kwa nini hawalipwi? Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri ukaliangalie hilo, walimu ni walezi, wamelea watoto zetu wametulea mpaka wenye we Wabunge hapa wote tumepitia kwenye elimu, kwa hiyo naomba waendelee kuwajali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 87, mradi wa *DMDP*, nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Serikali kwa uwezeshwaji wa mradi huu. Mradi huu umeleta maendeleo makubwa katika Jiji letu kwani sasa limebadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mbagala Kijichi huwezi kudhani kama ni Mbagala ile, barabara zimetawala, soko la kisasa na miradi kadha wa kadha imejengwa. Pia katika maeneo ya Yombo Vituka, Kilakala, Tegeta, Mikocheni, Buguruni, Ilala, Upanga, Temeke, Chang'ombe, barabara ile imepanuliwa kwa mradi wa *DMDP*, ni jambo kushukuriwa. Vilevile barabara ya Ubungo, Kibamba na Gerezani, zimeshughulikiwa, kwa kweli hali za barabara zetu katika Jiji la Dar es Salaam ni nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunasimama hapa ndani mimi na Mheshimiwa Mnyika tunazungumzia barabara ya Kibwegele – Kibamba, leo hii Mnyika amenyamaza kimya anahangaika tu na mambo yake ya Mahakama. Hii yote ni kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika Jimbo la Kibamba na Mkoa mzima wa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye upande wa mabasi yaendayo kasi, kwa kweli niipongeze

Serikali sasa mabasi yaendayo kasi mradi ule unatekelezeka. Tayari fidia zimelipwa na unaanza kujengwa kwa mabasi yanayoanzia kutoka Gerezani kwenda Mbagala Rangi Tatu. Tunamshukuru sana Mungu na Serikali yetu kwa kuliwezesha hilo. Mradi ule utakapokuja pale Mbagala Rangi Tatu maeneo ya Mbagala, Charamebe, Kiburungwa, Mianzini yatapanda thamani kutokana na miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najua penye jambo jema hapakosi changamoto. Kweli mradi wa mabasi ya mwendo kasi hivi karibuni umeleta umeleta changamoto kubwa kwa hasa yale yanayotoka Mbezi, Kimara kwenda mjini, kweli kumekuwa na uhaba. Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri jinsi ambavyo unakwenda kufuatilia kwa karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nliulize Serikali ule uhaba wa mabasi unatokana na nini? Niishauri Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kama ina fedha nyingi pamoja na mabasi yake ya utalii basi yale mabasi ya utalii iongezewe nguvu Halmashauri ya Jiji waweze kununua mabasi ya akiba iwapo kutatokea tatizo lolote basi mabasi yetu wenywewe ya Serikali au Halmashauri ya Jiji yawe yanaingia kwenye miundombinu ya mwendo kasi kuwasaidia wananchi wa Dar es Salaam.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mariam.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, iendelee hivyo hivyo. Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Rais wote kwa pamoja pigeni kazi wananchi wanawaamini. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mariam Kisangi. Tunaendelea na Mheshimiwa Joel Mwaka na Mheshimiwa Felister Bura ajiandae.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kushukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba zilizotolewa na Mawaziri wa Wizara hizi mbili ambazo zipo chini ya Ofisi ya Rais.

Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Sisi wote tunaona na tunashuhudia yale yanayoendelea katika Awamu hii ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Mawaziri wetu wawili, Mheshimiwa Jafo pamoja na Naibu wake lakini pia Mheshimiwa Mkuchika pamoja na Naibu wake katika Wizara zetu hizi mbili kwa taarifa zao walizoziwasilisha hapa jana ambazo zimezihidhirisha kabisa nia na kusudi zima la Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha kwamba Tanzania hii inavuka kutoka hapa ilipo kuingia katika Tanzania ya uchumi wa katika ifikapo mwaka 2025. Nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo nianze kwa kuunga mkono hoja za Wizara zote hizi mbili kwa asilimia mia. Kwanza kabisa, niseme kwamba kupanga ni kuchagua, Serikali yetu ya Awamu ya Tano ilipanga na ikachagua kwamba tunataka kufika mwaka 2025 nchi yetu iwe imeingia kwenye uchumi wa katika njia tutakayoichukua ni hii ambayo tunaiona sasa, tunazona bajeti zetu zilivyo makini kabisa kuhakikisha kwamba tunafika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mipango mikubwa, midogo na ya katika ambayo lazima yote iende kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba tunaweza kuvuka na kufika kule tunapotaka. Tuna mipango mikubwa ambayo tunaiona, mipango ya *Stiegler's Gorge*, *SGR* na kununua ndege ni mipango mikubwa. Mipango hii wakati mwingine watu wanashindwa kuoanisha, tunahitaji macho haya ya usoni, ya kwenye ubongo na ya rohoni tuweze kuona kwa ujumla wake tukajumlisha kwamba kweli mipango hii inawalenga Watanzania wote na hasa wa kipato cha chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii ndiyo inaweza kutuwezesha sisi kutekeleza mipango mingine midogomidogo iliyo muhimu kwa ajili ya wananchi wa katil. Ukitzungumzia elimu, ili tuweze kuingia katika Tanzania ya uchumi wa katil, tunahitaji wananchi wetu wawe na elimu bora. Tunaiona mipango ya Serikali ya elimu bila malipo lakini tunaiona mipango ya Serikali hii, tumekuwa tukilia walimu lakini sasa ajira zimetoka kwa walimu elfu nne na mia saba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukatekeleza matakwa yako yote kwa wakati mmoja hata siku moja. Kila jambo ni mchakato, utaangalia kwenye elimu, afya na kadhalika, kwa hiyo, lazima twende kidogo kidogo. Walimu hawa wachache ambaao Serikali imetoea ni mpango kamili na mwaka kesho na mwaka kesho kutwa lakini mwisho wa siku tutakuwa na uwanja mzuri wa kutoa elimu iliyo bora kwa vijana wetu. Mbagala Zachiem

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu pia, tunahitaji wananchi wetu wawe na afya bora. Afya bora siyo suala la kwenda zahanati au kwenye kituo cha afya tu bali unaishi vipi nyumbani, mazingira yako yakoje? Bila maji mazingira majumbani yanakuwa ni shida tupu na tunaweza kuhatarisha afya zetu kutoka nyumbani moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi sana kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji na sisi Wabunge wenyewe kupitia Mifuko yetu ya Majimbo tumejitahidi sana. Mimi jimboni kwangu toka nimeingia 2015 hadi leo nimekwishachimba visima kumi na mbili, lakini juzi Serikali imenisaidia nimepewa visima nane. Kama watu hawayaoni haya hawataona kitu. Nachoiomba Serikali ni kuongeza kasi, visima hivi vikichimbwa basi viweze kuwekewa miundombinu ili watu waweze kuyafaidi maji hayo na yaweze kuwasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia vituo vya afya 352 katika Halmashauri zetu, katika hivyo viwili vinatoka Halmashauri ya Chamwino; kimoja Jimbo la Chilonwa na

kingine Jimbo la Mtera. Tunaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hospitali za wilaya 67, katika hizo moja ipo Halmashauri ya Chamwino, tunaipongeza sana Serikali. Kama hiyo haitoshi, nakushukuru sana Mheshimiwa Jafo na namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Hospitali ya Uhuru katika Wilaya yetu ya Chamwino. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mambo yote haya yaweze kwenda lazima kuwe na mawasiliano mazuri baina ya maeneo yetu mbalimbali. Barabara na madaraja yanaendelea kujengwa awamu kwa awamu, kama nilivyosema hatuwezi kufanya mambo yote kwa wakati mmoja. Jimboni kwangu tumetengeneza madaraja mengi, Daraja la Manyemba, daraja la kutoka Mlebe kuja Chinangali II na sasa tunashughulikia daraja la kutoka Makoja kuja Mwengamile, ni kazi kubwa inayofanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TARURA* na *TANROADS*, watu wanazungumzia kujaribu ku-*balance*, ni jambo jema lakini n kuangalia wapi kuna jukumu gani la kufanya na wapi kuna jukumu gani la kufanya.

Mimi naiomba Serikali angalau basi kutoka asilimia 30 *TARURA* iende kwenye asilimia 40 hata tusipofika 50 ili nayo iweze kuboresha kazi zake nzuri ambazo inaendelea kuzifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA ni jambo jem,a tunataka wananchi hawa wajilettee maendeleo yao wenyewe, wanyanyuke kiuchimi. Mtu mmoja mmoja ili aweze kunyanyuka kiuchumi anahitaji kuwezeshwa na Serikali na Serikali imeleta MKURABITA ili watu waweze kurasimisha maeneo yao, wakapata hati miliki za kimila, hati hizi zikatambuliwa na mabenki ili waweze kukopa na kujiletea maendeleo. Ninachokiomba Serikali isimamie kwa dhati mabenki kuhakikisha kwamba wanazitambua hizo hati na wananchi wanapata mikopo kadri inavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF* sasa tunaingia awamu ya tatu. Naiomba sana Serikali maeneo yale ambayo yalikuwa haijafika sasa ikafike maana ndiyo mpango kamili wa *TASAF III*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa ombi mahsusila maboma ya shule, nyumba za walimu, zahanati na maabara ambapo wananchi wetu wameweuka nguvu zao nydingi sana, wamejitolea kujenga na wamefika mahali wamekwamba. Sawa Serikali imeweuka nguvu lakini naiomba iongeze nguvu zaidi ili maboma haya yaweze kumalizika na wananchi waweze kuyafaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Juma Nkamia ajiandae.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai ambao ametupatia siku ya leo sisi Wabunge kwa ajili ya uwakilishi wa wananchi walituchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa mambo makubwa anayowafanya Watanzania. Kuna msemo unaosema Nabii hakubaliki kwako lakini kuna nchi wanazotamani Magufuli awe Rais wao kwa utendaji na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu tuwaombe viongozi wetu Mungu awape afya njema na waendelee kutawala kwa hekima na maarifa itokayo kwa Mungu. Wanafanya kazi nzuri, tuwa-support kwa jinsi wanavyofanya kazi nzuri. Sisi wananchi wa Dodoma tupo pamoja nao, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu lakini zaidi ya yote

tunafanya kazi. Wabunge wa Dodoma tunafanya kazi kuonyesha kwamba tunamuunga mkono Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumefanyiwa mambo mengi sana na Serikali ya Awamu ya Tano. Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mambo makubwa sana kwa Mkao wa Dodoma. Kwa hiyo, tutamuunga mkono Rais wetu, treni ile iliyokuwa ya Mwakyembe Dar es Salaam utaikuta Dodoma, barabara za mizunguko utazikuta Dodoma, soko la kimataifa na standi ya kimataifa utavikuta Dodoma. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge usipojenga Dodoma utajutia maisha yako na familia yako itakulaani kwa nini hujajenga Dodoma kwa sababu Geneva ya Tanzania inakuja kuwa Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza mji kuna mambo, kuna utwaaji wa ardhi na shughuli mbalimbali za maendeleo zinazoendeleza. Wananchi wangu wa Dodoma wa Msalato pale ambapo uwanja wa Kimataifa unajengwa kuna wanaodai fidia. Niombe Serikali iwalipe wananchi wale fidia ili wakianza kujenga kusiwepo na malalamiko ya wananchi. Eneo la Ihumwa limechukuliwa kwa ajili ya bandari kavu, niiombe Serikali sasa wale wananchi walipwe fidia ili wasiendelee kuidai Serikali. Tunajua Serikali inafanya kazi kubwa lakini pia niombe kwamba malalamiko haya madogo sasa yasiwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la watu Dodoma, shule sasa zimejaa sana watoto; shule za msingi na sekondari. Mwaka huu tumeandikisha watoto shule za awali 15,000, watoto wa darasa la kwanza tumeandikisha 11,979, hawa si wachache. Tumejkita sana kwenye ujenzi wa shule za sekondari tukasahau kwamba watoto wa shule za msingi wanahitaji pia madarasa, wanavyoongezeka madarasa hayatoshi. Utafiti ufanyike kuona kwamba hawa watoto wanaoanza shule, kwa mfano hawa 15,000 shule ya msingi watakwenda wapi, madarasa hayatoshi. Tumekazania kujenga shule za sekondari lakini za msingi je? Madarasa ya shule za msingi hatujaongeza muda mrefu, Serikali iangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi Dodoma tulitoa ardhi kwa Serikali kwa ajili wa ujenzi wa shule nydingine, shule ya kitaifa badala ya Shule ya Sekondari ya Mazengo. Tulitoa ardhi na Waziri wa Elimu alipewa ile ardhi kwa ajili kujenga shule ya kifaifa badala ya Shule ya Mazengo iliyorudishwa kwa waliokuwa wamiliki wa Kanisa la Anglikana. Sasa eneo lile tulilolitoa kwa ajili ya ujenzi wa shule ya kitaifa mpaka sasa haijajengwa mwishowe wananchi watavamia lile eneo halafu tutaanza sasa suala la ulipaji fidia. Niombe sasa Wizara ikachukue eneo lile kwa sababu shule inayojengwa pale ni ya kitaifa itachukua wanafunzi Tanzania nzima basi waanze suala la ujenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lile tulilolitoa kwa ajili ya Shule ya Kitaifa halijajengwa mpaka sasa, mwisho wananchi watavamia lile eneo halafu tutaanza sasa suala la ulipaji fidia. Naomba Wizara ikachukue lile eneo kwa sababu shule inayojengwa pale ni ya Kitaifa, itachukua wanafunzi Tanzania nzima, basi waanze suala la ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Walimu 656 wa shule za msingi kwa shule za Dodoma za pembezoni. Dodoma Jiji kuna mahali ikama ni Walimu 10 lakini utakuwa Walimu wako watatu tu. Naiomba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Serikali Sikivu, Serikali inayowajali wanyonge, Serikali iliyoamua kwamba kila mtoto apate elimu. Mtoto atapata elimu nzuri tu kama Walimu wako shulenii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba maeneo yote na siyo Dodoma tu, naombe maeneo mengine ambayo Walimu hawatoshelezi tuleteewe Walimu wa kutosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali ya viwanda, yaani tunataka kujenga viwanda; hatuwezi kujenga viwanda kama hatuna wanasyansi na Walimu wa Sayansi ndio hawatoshi katika maeneo yetu. Naiomba Serikali yangu, wako Walimu waliomaliza Elimu ya Vyuo Vikuu na walisoma masomo ya sayansi, tuombe sasa katika ugawaji wa Walimu

wa Shule za Sekondari, tupeni hao Walimu ili tuwapate watoto watakaotumika viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza suala la elimu, niombe sasa, katika Jiji letu tuna vijiji 34 ambavyo tunavihesabu kama ni mitaa. Wawekezaji wako wengi lakini hatuna umeme, vijiji hivyo vipate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Joel Mwaka amezungumzia suala la hospitali ya Uhuru na pesa za kujenga hospitali ya Uhuru ilitokana na maadhimisho ya Desemba 9, Mheshimiwa Rais akaamua hizo fedha zijenge Hospitali ya Uhuru Wilayani Chamwino. Mpaka leo fedha hizo hazijafika katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ili zijenge hiyo hospitali. Naiomba Serikali, katika bajeti hii hizo fedha zije na kama zillishatengwa na Mheshimiwa Rais alitamka, tupeni hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ina miaka zaidi ya kumi wamehamia lakini wamehamia *floor* ya chini, lile jengo halijaisha. Tumeomba shilingi milioni 900 ili tujenge jengo lile la Halmashauri. Tunawashukuru kwamba mmetupa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, hizo fedha zije sasa ili Mkuu wa Mkoa awe na ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Mariam amezungumzia suala la mabasi ya mwendokasi. Tunaishukuru Serikali na kuipongeza kwamba sasa hivi usafiri wa Dar es Salaam ni wa haraka, lakini mabasi yale mengi yameharibika, yatengenezwe sasa. Miundombinu ya mwendokasi imechukua pesa nyingi za Watanzania, Serikali ikubali kwamba yejote mwenye uwezo wa kuendesha njia ya mwendokasi, basi waweke magari pale yaweze kuwashudumia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna maboma ambayo hayajakamilishwa au kuna maeneo ambayo vituo vyta afya havijafika. Naomba Kata ya Kolo Wilayani Kondoa,

wananchi wanatembea kilometa 30 kwenda kutafuta huduma ya afya. Naomba sana, Serikali itusaidie Kituo cha Afya pale Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Posho ya Madiwani; Madiwani ni watu muhimu katika Taifa hili, wanafanya kazi kubwa. Madiwani wafikiriwe, wanafanya kazi kubwa, lakini posho inayotolewa kwa Madiwani haitoshi, kidogo mno; na wakati mwininge wanakaa hata miezi mitatu hawajapata posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu siku inayowajali wananchi wake, Posho za Madiwani zikafanyiwe ufumbuzi sasa ili Madiwani wafanye kazi kwa moyo mmoja.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Felister.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma Nkamia, baadaye Mheshimiwa Maftah ajiandae.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha salama leo, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli, pamoja na wasaidizi wake Mheshimiwa Jafo pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianzie pale alipomalizia pale Mheshimiwa Bura kwenye suala la Madiwani. Madiwani tusiwaone ni wa maana tu pale tunapokwenda kwenye uchaguzi. Nazungumza hili kwa nini?

Nataka nitoe na mifano. Madiwani wengi Tanzania, kwenye Halmashauri nyingi hata posho zao za kisheria hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visingizio vingi vimekuwa ni mifumo ime-*bust*, lakini kumbe Halmashauri nyingi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba wameshindwa kupeleka fedha za maendeleo, wamejikuta *expenditure* imekuwa kubwa na matokeo yake Madiwani toka mwezi wa Kumi mpaka tunavyozungumza, hata posho za vikao vyao nya kawaida wanakopwa. Mheshimiwa Waziri Jafo anajua, Mkuu wa Mkoa anajua na *RAS* wa Dodoma anajua. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba ipo haja ya kuangalia hili suala kwa kina sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Waziri, nitumie fursa hii kuwapongeza sana. Leo Chemba tuna Vituo nya Afya vitatu; viwili *Alhamdulillah* vimejengwa vizuri; kimoja ndiyo hivyo, tia maji tia maji, lakini tunashukuru. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri tulikwenda naye pale Hamai, na akakuta ile hali ya pale na hakuchukua hatua yoyote, japo kauli yake pale alisema hajaridhishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, nimekuwa nikiona Waheshimiwa Mawaziri wanatembea sana Tanzania hii kwenda kutatua kero za wananchi, lakini juzi nilipokuwa Kanda ya Kusini kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais, nimeona ye ye ndiyo anatatua matatizo hata yale ambayo ninyi mngeweza kuyatatua. Sasa mnazunguka kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vizuri mkachukua hatua pale mnapoona kuna kasoro. Kwa mfano, pale kwa Mtoro, mtu amepewa tenda ya kutengeneza milango akalipwa shilingi milioni 15 zote hajapeleka hata *frame* moja. Watu wa Chemba wanajua, Ofisi ya TAMISEMI inajua na Mungu anajua. Chukueni hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tukisema hapa na ninyi pale TAMISEMI kuna majungu yanaletwa sana kule, kwamba ooh, unajua Mbunge wa Chemba, Mwenyekiti wa

Halmashauri, Mwenyekiti wa CCM wanataka posho tu. Posho za nini? Watu wenu pale TAMISEMI wakishasikia hivyo, sisi tunaomba Mheshimiwa Waziri aunde tume ikachunguze matatizo ya Chemba, hatutaki kumwonea mtu. Chemba imekuwa shamba la bibi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua. Tuliomba aunde tume apeleke pale ikachunguze. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Chemba tunaomba tupatiwe pesa mwaka huu. Pia hata tukipewa hizo pesa, hata zile *1.4 billion* mlizotupatia, yule Boya ameshajenga lile jengo anadai fedha zake shilingi milioni 150, Halmashauri haina hizo fedha. Zimeenda wapi? Hata mkitupa leo, mimi sioni faida yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya. Dakika 20 zillzopita allnipigia *engineer* mmoja ambaye anajenga Hospitali ya Wilaya pale Chemba, wameingia mkataba toka mwezi wa Pili, leo walikuwa wanataka kugoma kuendelea kujenga, hawajalipwa hata senti tano na fedha mmeleta. Sasa tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, chukua hatua, hii inakusaidia kukujenga pia kwa siku zijazo. Ya Mungu mengi, huwezi kujua. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana kaka yangu, chukua hatua. Leo wanataka kugoma kujenga Hospitali ya Wilaya kwa sababu hawajalipwa, fedha mmeshaleta. Kuna tatizo gani? Mkataba toka mwezi wa Pili. Au mpaka wasikie Mheshimiwa Rais anakuja? Kwa hiyo, naomba mtusaidie juu ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye vitambulisho vya Mheshimiwa Rais. Hili ni wazo zuri sana sana, lakini huko Wilayani operesheni yake inakwenda tofauti. Baadhi ya watu wanamchukia Mheshimiwa Rais kutokana na baadhi ya Watendaji walioko huko Wilayani kulifanya hili kama vita. Wewe unawezaje kugawa vitambulisho hivi vya wajasiriamali

chini ya ulinzi wa Polisi? Nani atakuja kuchukua? Hivi wewe kiongozi unaanza kukurupushana na akina mama unabeba masufuria ya pilau, unawalazimisha wanunue vitambulisho, nani atachukua? Chukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma kwa kuzuia Polisi wa Chemba wasiende kugawa vitambulisho vyta Rais. Sasa hivi vitambulisho vinauzika sana. Yule Mkuu wangu wa Wilaya alisema, mimi na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya tunazuia. Ashindwe kwa Jina la Yesu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda mimi na Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Kakunda wakati ule, mradi wa maji wa Lahoda uliojengwa na Mkandarasi *Mrimi Construction* akalipwa shilingi milioni 451, hautoi hata tone moja na maji. Hata tone hakuna, wala kisima hakikuchimbwa na mtu kalipwa fedha zote. Tukisema sisi, kesho wanakuja watu TAMISEMI pale, aah, unajua Mbunge anataka rushwa. Nendeni mkachunguze ili mjue kuna rushwa kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapakaziana tu! Mtu anaandika taarifa huko, unajua Mbunge anataka rushwa, unaitwa TAKUKURU. Nenda kachunguze, kama kuna tone la maji, kama sio mimi na Mwenyekiti wangu kwenda kuwaomba watu wa *RIC* watusaidie pale, lakini *Mrimi Construction* amelipwa milioni 450...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Keissy, usinijaribu.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Mheshimiwa Nkamia, mzungumzaji, kwamba

kule kwangu Wakandarasi walimfuata Mheshimiwa Nkamia ili tuonane nao wanipe rushwa. Nikawaambia siwezi hilo jambo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nkamia, taarifa hiyo.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, kuna watu walinifuata hapa wanasema, bwana tusaidie kwa Mheshimiwa Keissy. Nikamtafuta Mheshimiwa Keissy mwenyewe, nikajua ndio hao hao. Nimeipokea kwa mikono 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri aunde Tume Maalum ichunguze matatizo yaliyoko Wilaya ya Chemba. Nashukuru Mheshimiwa Mkuchika upo wewe ni mtu mzima, naomba mtusaidie. Matatizo ya Chemba yanaweza kutuletea matatizo mengine makubwa. Haiwezekani Mkuu wa Wilaya anasimama saa sita barabarani anasimamisha magari kama *traffic*, yuko peke yake. Haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Mkurugenzi wa Halmashauri anajenga kwa miezi miwili na anataka kuchimba kisima cha kuuza maji pale Chemba wakati watu wanakunyuwa maji kwenye kisima nilichochimba mimi. *Where do you get money?* Halafu anakwenda TAMISEMI pale, aah unajua Mbunge anataka rushwa, unajua Mwenyekiti wa Halmashauri anataka rushwa. Rushwa gani mimi? *I have got my own investment bwana.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwaambieni ninyi, hamtaki kuchukua hatua. Mnasubiri mpaka Mheshimiwa Rais aje? Eeh, mnapokea majungu mnayaona ya maana. Tunayowaambieni, mimi nimesema, undeni Tume ikachunguze ili mjue nani mwongo? Unapiga chapa ng'ombe milioni 290 senti tano haipo. Unatuambia mfumo ume-bust, benki una shilingi milioni 40 tu, zimeenda wapi hela? Halafu Mbunge akisema hapa, aah, unajua wale wana majungu sana wale, wale wana majungu sana wale! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda mahali wako, ukaone. Mnatuambia aah, mnajua wale ni wanasiasa tu, wanasiasa tu wale. Hata hao wote wawili pale kwangu waligombea Ubunge wakashindwa; wote ni wanasiasa. Ooh, unajua tutahakikisha Nkamia uchaguzi ujao jina lake halirudi. Kwani lisiporudi, kwa Mungu haliendi? (*Kicheko/Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mwongeze dakika. Mpe dakika 10 nyingine zangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftaha Nachuma na baadaye Mheshimiwa Japhary Michael ajiandae.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu wataala* kwa sababu tangu tumemaliza kufanya Uchaguzi Mkuu ndani ya chama, uchaguzi ambao ulimweka Prof. Ibrahim Lipumba kuwa Mwenyekiti wa Chama Taifa, lakini mimi ninayezungumza hapa Maftah Nachuma kuwa Makamu Mwenyekiti Bara. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutusimamia na sasa chama chetu kimesimama imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa maneno ambayo alisema Mwanafalsafa Mtume Muhammad (S.A.W.) karne ya sita alizungumza maneno yafuatayo, kwamba *man laa yashkur kaliila, laa yashkur kathiira*. Kwamba yeoyote ambaye hashukuru kidogo alichopewa, basi hata akipewa kingi hawezi kushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa nishukuru Wizara hii ya TAMISEMI kwa bajeti ambayo mwaka

2018 tulipigania sana zikaletwa Mtwara shilingi bilioni 21 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu pale Mtwara Mjini, kujenga mifereji, kujenga *shopping mall*. Tunaishukuru sana TAMISEMI kwa sababu imeweza kutusikiliza kilio cha wana Mtwara na sasa tunajenga mifereji ya kupeleka maji baharini ili Mtwara sasa tuondokane na mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na shukrani hizo, bado kuna makandokando mengi katika zile fedha ambazo zimeletwa shilingi bilioni 21. Wale ambao walipewa dhamana ya kupitia na kusaini mikataba, kuna makandokando mengi sana. Mikataba ile ilisainiwa kwa namna ambayo haieleweki, haikuwa na uwazi. Kwamba watu waliitwa kutoka Mtwara Mjini, akaitwa Mkurugenzi, akaitwa aliyekuwa Meya kwenda Dar es Salaam, baadaye wakarudishwa pale Mtwara wakiwa wamesaini mikataba. Kwa hiyo, kuna malalamiko mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Madiwani ambao wanazungumza mambo mazito sana, kwamba mikataba yule Mkandarasi aliyepewa ule mradi wa kujenga miundombinu Mtwara Mjini mkataba wake umesainiwa kimazingara mazingara. Tunaomba Wizara ya TAMISEMI ifanye uchunguzi haraka iwezakanavyo, wale wote walilohusika kwamba wamepewa kiasi kidogo ili wampe yule Mkandarasi kutoka China, kufanyike uchunguzi wa kina, waweze kuchukuliwa hatua. Kwa sababu kiasi kinachotajwa kwamba kimetolewa ni kiasi kingi sana kitu ambacho zile fedha zingeweza kusaidia kuboresha miundombinu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza ni kwamba mpaka hivi sasa ule mradi unasuasua. Fedha zipo, Mkandarasi anasuasua kwa sababu mazingira ya ule mkataba ni mazingira ya ajabu ajabu. Tunaomba uchunguzi ufanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nizungumzie suala la Hospitali ya Mtwara. Hospitali zetu za Mtwara hasa ile Hospitali ya Wilaya lakini pia ni ya Mkoa ya Mtwara, tunaomba ipelekewe vifaa. Hospitali ile haina *X-Ray*, haina

vifaa vya kupimia, haina *CIT-Scan*. Wananchi pale wanapotaka kupimiwa au wanavyotaka kupimwa, pale ambapo wanaambiwa waende waende Hospitali ya Mkoa ambapo imezkuwa Hospitali ya Rufaa hivi sasa, wakifika pale vile vipimo vyote havipo, wanaambiwa waende Dar es Salaam. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana, tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu sana kwamba hospitali hii ipelekewe vifaa, vifaa tiba, hata dawa nayo pia hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine la ajabu sana. Ukienda kwenye hospitali hii hivi sasa kuna walinzi ambaao wamewekwa wa *SUMA JKT* wanaoangalia wagonjwa wanavyoenda pale kutibiwa. Nimepata malalamiko mengi kama Mbunge kwamba walinzi wanawapiga wagonjwa wanavyoenda kuingia hospitali pale eti kwa sababu wanapita mlango ambaao hauko sawa sawa. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali, pamoja na kwamba tunahitaji ulinzi uwepo katika hospitali zetu, lakini lazima wagonjwa waweze kuheshimiwa, Wana-Mtwara waweze kuheshimiwa, wasipigwe na hapa Mapolisi na *SUMA JKT* ambaao wamewekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuzungumza ni suala hili la demokrasia; Katiba katikalbara ya 146 inaeleza kwamba: TAMISEMI imepewa mamlaka ya kusimamia chaguzi. Mheshimiwa Waziri hapa kazungumza kwamba mwaka huu tutakuwa na uchaguzi wa mitaa, lakini kuna mambo ya ajabu sana tumekuwa tuna-experience ndani ya nchi yetu tangu chaguzi hizi zinafanyika hasa hasa hizi chaguzi za marudio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba kuelekea katika uchaguzi huu jambo la kwanza kuwe na Tume Huru ya Uchaguzi; tunahitaji kuwe na Tume Huru ya Uchaguzi ili iweze kusimamia sawasawa kwa sababu kuna mambo mengi

ambayo yamekuwa yakijitokeza katika usimamizi wa hizi chaguzi. Kwa mfano, suala hili la kutafuta wagombea vyama vya siasa vinateua wagombeakwa mujibu wa sheria lakini wakipelekwa kwa wale wanaosimamia, wale wanaoteua, wale watendaji wakata wanawaengua wagombea kutoka upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza haya tuna ushahidi sana, kwa mfano, pale Kata ya Nanguruwe kuna wagombea walishawishiwa wakahamia Chama cha Mapinduzi, lakini sisi Chama cha Wananchi - *CUF*tukasimamia uchaguzi na mchakato ndani ya chama. Wagombea wetu walivyokwenda kutakana kuteuliwa wakaenguliwa bila sababu za msingi, wakaenguliwa bila utaratibu, wakati tunasema nchi yetu niya kidemokrasia na ni nchi ya vyama vingi. Nami nilienda pale Nanguruwe kuzungumza naMtendaji wa Kata nikamwambia kwa nini unamwengua mgombea wa *CUF* akanieleza kwamba hajatimiza vigezo, hali ya kuwa kila ya kitu tumeefanya, *form* kajaza sawasawa na alivyojaza mgombea wa *CUF*,ndivyo alivyojaza mgombe wa CCM lakini mgombe wa *CUF* amaenguliwa. Sasa haya ni mambo ya ajabu sana, kwa hiyo tunaiomba TAMISEMI tunavyokwenda kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, haya mambo yaweze kufanyika sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine pia pale Kata ya Tangazo, Mtwara Vijijiini napo, pia kulikuwa na mazingira hayo hayo kwamba wagombea wa Chama cha Wananchi - *CUF* wanaenguliwa bila kufuata taratibu za kisheria na Watendaji Kata na ukimuuliza Mtendaji Kata anasema nimepata maelekezo kwamba huyu mtu hafai na kweli tumemwondoa. Kwa hiyo, mazingira hayo tunanyima demokrasia ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye hizi chaguzi, sisi tumeshiriki chaguzi zote za marudio Chama cha Wananchi - *CUF*,hasa kule kwetu Kusini kwa mfano,kuna kata moja, Kata ya Nalingu pale Mtwara Vijijiini chama cha Wananchi - *CUF* kilipambana, mgombea wetu alikuwa makini, wananchi wakampenda, wananchi wakamchagua,

tulivyokuja kwenye kuhesabu kura chama tawala kinaleta polisi ndani ya masanduku na wakawaambia kwamba bwana tunachotaka hapa sisi kama polisi, sisi ndio tunahesabu hizi kura. Kwa hiyo hiki ni kinyume kabisa cha demokrasia nchini, kwamba tunapoingia kwenye chaguzi tusiruhusu Jeshi Polisi kwenda kuhesabu, kwenda kung'ang'ania masanduku ya watu waliofanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sanakwamba, kama kweli tunahitaji amani ya kweli, ni lazima chaguzi hizi tuzisimie sawasawa tufuate sheria, tufuate Katiba namna inavyosema, Tume ya Uchaguzi iweze kuwa huru, wale askari wakae mbali kwa mujibu wa sheria inavyosema, lakini hivi sasa chaguzi zote za marudio tumeona, tumeweza kujiridhisha kabisa kwamba polisi wanaingia ndani kwenda kuhesabu kura. Je hii ni kazi ya polisi? Tunaomba sana haya mambo yaweze kuzingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Nkamia hapa ameezungumza mambo mengi yanayohusu Chemba, lakini sisi pia kama Chama cha Wananchi - CUF kule Chemba yule DC wake niliwahi kuzungumza kwenye Bunge hili, niliwahi kuzungumza hapa kwamba, balada ya kusimamia miongozo ya Serikali, badala ya kusimamia taratibu za nchi hii, ye ye kazi yake kubwa amekuwa anafanya kazi ya kuwafukuza Wenyeviti wa Mitaa wa Chama cha Wananchi - CUF. Hivi ninavyozungumza zaidi ya Wenyeviti tisa amewafukuza, yaani anaeeenda sehemu anaitisha mkuano, anawaambia hawa mimi nawafukuza. Hafukuzi Wenyeviti wa CCM, hafukuzi Wenyeviti wa chama kingine, ye ye anaefukuza Wenyeviti wa Chama cha Wananchi - CUF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili naomba kujua, utawala bora tunaozunguza hapa ni utawala bora wa aina gani, demokrasi tunayozungumza ni demokrasia ipi, kama DC yupo pale kuangalia upinzani, pale waliposhinda anawafukuza. Wakati tunasema kwamba demokrasia uwaache wananchi wafanye wanayotaka, wamchague kiongozi wanayemtaka, wananchi wamechagua viongozi, wamechagua Wenyeviti wa CUF, DC anaenda anawafukuza

Wenyeviti tisa, ni mambo ya ajabu sana. Tunaomba sana Serikali kwa kweli kama tunahitaji tuwe na amani na utulivu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunahitaji hawa Ma-DC wafanye kazi zao walizopangwiwa na mteule wao.

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnes taarifa

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampataarifa mzungumzaji kwa kifungu cha 68(7), yeye angelikuwa anaona Tanzania haina demokrasia, leo hii imekuaje yeye kutoka upinzani amekuwa Mbunge?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimusana kwa sababu anachokzungumza hakifahamu. Hapa tunachozungumza, ni kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na ipo kwenye taarifa ya Waziri wa TAMISEMI ukurasa wa 12kwamba, mwaka huu kuna uchaguzi wa Serikali za mitaa tunazungumza yanayojiri, yanayojitokeza katika chaguzi hizi ambazo tumekuwa tukifanya kwa muda wa miaka mitatuhivi sasa, kwamba Wapinzani wanaong'olewa, wapinzani wanaondolewa lakini Ma-DC waliochaguliwa kusimamia maendeleo ya wananchi wao wanafanya kazi ya kuhujumu upinzani na kuwafukuza Wenyeviti waliochaguliwa wa Chama cha Wananchi - CUF na wa vyama vingine, sasa hapa tunasema hakuna demokrasia ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze jambo moja hawa Ma-DC na Ma-RC kwa sababu wamekuwa na utamaduni, kwa mfano, pale kwangu Mtwara, juzi Mheshimiwa Rais kaja Mtwara, katika jimbo la Maftaha Nachuma ambaye ndiye, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini, RC tunamuuliza kwamba katika ratiba umemweka Mbunge wa jimbo ili aweze kusalimia wananchi wake. RC anasema wewe hatuwezi kukuweka kwa sababu wewe ni mpinzani. Sasa haya ni mambo ya ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kule kote alikopita ambapo Wabunge ni wa Chama cha Mapinduzi wamepewa nafasi Mkao ule ule lakini mimiwa Mtwara Mjini nauliza pale mbona hujaniweka kwenye ratiba, ananijibu wewe ni mpinzani. Sasa hii ni demokrasia ya wapi, lakini niwaambie, naomba niwaambie kwamba hawa Ma-*DC* na Ma-*RC* viongozi wengine wanapimwa na Mheshimiwa Rais kwa kazi wanazofanya, sio kazi ya kuwahujumu wapinzani ndani ya nchi hii. Mheshimiwa Rais atawapima atawapandisha vyeo kwa kazi wanazofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba sana Serikali, kwa sababu hawa watu wanafahamika, nilishawahi kuzungumza hapa ndani ya Bunge hili kwenye *Briefingnikamweleza* Waziri Mkuu wakati Fulani, akasema hakuna maagizo yoyote wanayotuma hawa Ma-*DC* na Ma-*RC* waweze kuwahujumu upinzani na hasa pale ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Kiongozi yoyote wa Kiserikali anavyokwenda kutembelea kwenye maeneo yetu kwamba ni Mbunge lazima upewe nafasi. *RC* anayetoka Mtwara Mjini anamnyima nafasi Maftaha eti kwa sababu ametokea Chama cha Wananchi *CUF*, anaenda Nanyumbu, anaenda kule wapi, anaenda kuwapa wale Wabunge wa CCM, Mkao mmoja ule ni ubaguzi na sisi tunasema kwamba kama tunahitaji nchi hii iwe na amani ili amani yetu iweze kuendelezwa tuheshimu msingi ya kidemokrasia, ni lazima tuheshimu msingi ya utawala bora hatuwezi kuwa na ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii tunasema inafuata *good governance* kwamba utawala bora na utawala wa kisheria na mionganoni mwa msingi ya utawala bora ni kuwa na *inclusive*, watu lazima tushirikishwe, nilichaguliwa na wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini na kwa kuthibisha hilo juzi Mheshimiwa Rais ameondoka, lakini nilivyoitisha mkutano wa hadhara mafuriko yamekuwa ni makubwa kweli kweli kwa sababu wananchi wanamwamini Mbunge wao walijemchagua. Serikali lazima ishirikiane na Mbunge husika sio kumtenga Mbunge, sio msingi ya kidemokrasia. Kwa hiyo kwa sababu Waziri ananisikia

Mheshimiwa Mkuchika alikuwepo ameshuhudia hilo na Waheshimiwa Mawaziri walikuwepo wameshuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti,jambo lingine la ajabu ambalo nasikitika sana baadhi ya Wabunge wenzetu wanashadidia Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanashadidia kwamba Mbunge wa *CUF* amenyimwa nafasi halifu. Naomba haya mambo yaweze kurekebishwa ilituweze kuwa na maendeleo sawasawa ya nchi hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhary Michael baadaye Mheshimiwa Hasna Mwilima ajindae. Mheshimiwa Japhary Michael.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kupata nafasi hili ya kuchangia. Naomba nichangie hotuba zetu mbili za Kambi ya Rasmi za Upinzani naeneo kubwa ambalo nataka nichangie la kwanza, ni kuhusu kanuni ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Katika hotuba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, ukurasa 17, kifungu cha 18, imeonesha kwamba kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zimeshakamilika lakini jambo la kushangaza ni kwamba tarehe 1, 2 na 3 Aprili, wadau wa vyama vya siasa na *NGO*'s na Asasi Zisizo za Kiserikali waliitwa kwa ajili ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anahutubia Bunge hili alisema kwamba tayari kanuni zimekamika wakati wadau waliitwa kwa ajili ya kutengeneza rasimu. Sasa tunachojuiliza hapa nikwamba wadau waliitwa kufanya nini, kwa sababu haiwezekani tarehe 1-3wadau waitwe halifu tarehe 4 Aprili, kanuni zionekane kuwa zimeshakuwa tayari wakati waliitwa kwa ajili ya kuandaa rasimu. Sasa rai yetu, tunaomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hotuba yake atusaidie kupata nakala zile za kanuni ya uchaguzi ili tuone kama mawazo na maoni ya wadau yamechukuliwa kwa kiwango gani ili kufanya uchaguzi huu uwe ni uchaguzi ambao ni huru, utakaofanya kila mtu aliyeshiriki aone ametendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kuzungumza kuhusu kujenga taasisi kuliko kujenga mtu katika nchi yetu. Tulidhani kwamba ni vizuri katika nchi yetu tuhakishe kwamba taasisi zetu zinakuwa imara kwa sababu watu wanapita, lakini taasisi zitaendelea kubaki. Lazima tuwe na taasisi ambazo zinahakikisha kwamba watendaji wanaoteuliwa katika nchi hii wanateuliwa kwa sababu ya uwezo wao na sio kwa sababu ya uswahiba wao na viongozi wa juu. Hawateuliwi kwa sababu wana mahusiano yoyote na viongozi wa juu bali kwa sababu wana maadili ya kuweza kuwasaidia Watanzania, taasisi zetu lazima zioneshe hivyo. Pia taasisi zetu lazima zioneshe kwamba kiongozi wa nchi hii ni mlinzi wa fedha za wananchi na sio mwenye fedha za wananchi. Kwa sababu hali ilivyo sasa walipakodi ni wananchi, lakini fedha inaonekana inayokusanya katika nchi ni fedha ya kiongozi wa nchi. Kwa misingi hiyo ana uwezo wakuamua anavyotaka kuipeleka, ana uwezo wa kutembea nayohata kwenye maboksi akagawa barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunadhani ni vizuri tujenge mfumo ambao utafanya kiongozi wa nchi afahamu fedha aliyonayo ni fedha ya wananchi kwa hiyo kila mwananchi katika nchi hii ana haki ya kupata maendeleo kwa kadri ya mchango wake.

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na heshima yangu kubwa kwa kaka yangu Mheshimiwa Mbunge, nataka nimpe taarifa kwamba kiongozi wa nchi yetu anatambua fedha zote ni fedha za wananchi na ndio maana bajeti ya nchi inaletwa hapa kila mwaka na ndio maana tupo hapa ndani ya miezi mitatu kujadili bajeti ya nchi. Kwa hiyo, asipotoshe umma kwamba kiongozi anasema pesani za kwake, pesa za wananchi, ndio maana Wabunge tupo hapa. Taarifa hiyo nampa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba nasema tutengeneze mfumo katika Taifa letu utakaowafanya viongozi wote watambue kwamba fedha za nchi sio za kwao ila ni za walipakodi. Kwa hiyo wana haki ya kuwapelekea wananchi maendeleo kwa kadri wanavyostahili na sio kwa kadri ya utashi wake na sijazungumzia kiongozi wa nchi aliyepo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri mifumo hii ikawepo ili iheshimu demokrasia. Ndani ya nchi yetu hii leo demokrasia haipo, na kila wakati ukisema demokrasia haipolinaonekana hili ni suala la upande mmoja,lakini leo Mungu angeweza akageuza kibao, upande huo ukawa upande huu, halafu kwa mifumo hii hii tuliyonayo, Tume za Uchaguzi tulizonazo na mazingira haya tulionayo, upande huo ungelalamika kuliko upande huu.

TAARIFA

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Nimpe Taarifa muongeaji pamoja na kwamba wenzetu wakiambiwa kwamba ipo siku moja inaweza kugeuka wanakataa, lakini katika Qurani Tukufu ipo aya inayosema hivi; *Innama amruhu idha arada shay-an an yakuula lahu kun fayakuun* (hakika Mwenyezi Mungu jambo analolitaka huliamrisha na kuwa).Sasa msijidanganyi kwamba haiwezekani ipo siku, ipo siku.

MWENYEKITI:Mheshimiwa Japhary, huyo anachanganya.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muumini mkubwa sana wa Mungu na kwa bahati mbaya wana siasa wanajitoa kwenye uelewa wa kumwamini Mungu, kwa taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge naipokea kwa mikono miwili, kwamba kilichowaweka huko mkatawala ndicho kitakachoweza kuwaweka watu hawa huko wakatawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi ambao tunatakiwa tuujenge kwenye Taifa hili ni wote tutambue kwamba

tunapaswa kuliona Taifa hili kama letu wote pamoja. Akitawala huyu aheshimu wengine anaowatawala. Sasa bahati mbaya katika Taifa hili imeonekana kwamba kuna upande ambao hili Taifa ni la kwao wengine sio Watanzania yaani tunaonekana tupo Tanzania kwa bahati mbaya tu lakini si kwamba nasi tuna haki ya kuwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachosema kwamba ni vizuri tutengeneze mfumo ambao utaheshimu haya, demokrasia iwe *part* ya maisha yetu. Haiwezekani leo Mheshimiwa katika Taifa hili CCM wanafanya mikutano ya hadhara ya ndani, wanafanya maandamo, wanalindwa lakini kila siku Wapinzani wanaandamwa ndani ya Taifa moja na Wapinzani hawajavunja sheria kwa sababu hawajawaWapinzani kwa sababu wametaka kuwa hivyo bali katiba imewaruhusu kuwa hivyo. Vyama vingi vya siasa vimeruhusiwa na Katiba ya nchi yetu. Hivyo,ni wajibu wetu sote sisi tuheshimiane kwa sababuKatiba inaruhusu kuwe kwetu sisi na kuwepo kwenu nyie.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Katiba inakuwepo ili sisi tuwakosoe nyie na sio tuwasifu nyie, hatupo hapa kwa ajili ya kuwasifu, ingekuwa kuwasifu tungekuwa upande wenu. Tupo upande huu ili tuwakosoe ili siye tuwe kioo kwenu ili mfanye vizuri, mnatulazimisha tukae Bungeni kuwasifu inaonekana *as if* kuwakosoa ni kumchukia Rais, si kweli. Hatumchukii Rais bali tunatimiza wajibu wetu wa kuwakosoa, tunam-*shape* Rais aweze kuongoza vizuri, ndio maana ya kuwa huku. Sasa ninyi mnadhani kumkosoa Rais ni kumkosea adabu Rais, si kweli na ubaya zaidi mnampanya Rais ahisi kwamba sisi tuna ugomvi na yeye, tuna chuki na yeye, baadala ya kumsaidia kwamba hawa ni wenzako wanaku-*shape* tukae vizuri. Kwa hiyo nadhani mfumo mzuri wa utawala ndani ya nchi hii utatufanya tukae vizuri. Kwa hiyo,hiyo ndio rai yangu kwaWaheshimiwa viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, nataka nizungumze suala la TARURA, Bunge lako Tukufu liliridhia kuanzishwa kwa TARURAKatika nchi hii, lakini TARURA malengo yake ya msingi kama yalivyofikiriwa hayawezi kuwa msaada

sasa kama *TARURA* haitaangaliwa vinginevyo. Sasa hivi Wakala wa Ujenzi wa Barabara Vijiji na Mjini hajawa msaada sana wa kuhakikisha barabara zetu zinakuwa kama zilivyokuwa zimetegemewa ni vizuri Mheshimiwa Waziri tuone namna gani tunahakikisha kwamba moja tunapeleka bajeti ya kutosha kwenye wakala huyu ili afanye vizuri kwenye barabara zetu, otherwise barabara ni mbaya zaidi kuliko hata wakati zikisimamiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wakati Halmashauri zikisimamia barabara zilikuwa zinauwezo wa kutenga fedha kwenye Kamati zao za dharura zikahakikisha barabara zao zinatengezwa. *TARURA* hawana hiyo fedha mpaka wasubiri fedha kutoka kwenye Mfuko Mkuu, matokeo yake wanashindwa kufanya kazi yao inayotarajiwa. Barabara nyingi zinakuwa mbovuna yaktokea majanga ya mafuriko na mambo mengine inakuwa vigumu sana barabara zetu kutengenezwa kwa hiyo hali inakuwa ni mbaya zaidi. Ni vizuri tuongeze bajeti ya kutosha nani vizuri tutafute vyanzo vingine kwa *TARURA* ili waweze kuhakikisha kwamba wanasmamia zoezi hili vizuri na malengo ya Wabunge kuomba *agency* hii iundwe yawe na maana. Kwa hiyo, nashauri sana tuangalie hili katika uzito wake wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika *TARURA*ni vizuri tuone jinsi gani Madiwani wanashirikishwa, Madiwani wanakuwa kama sio sehemu ya Halmashauri husika wala miji husika, matokeo yake maamuzi ya watendaji wa *TARURA*yanakuwa ni wao wenyewe. Sasa tuangalie sheria yetu itafanyaje Madiwani washirikishwe ndani ya *TARURA* hata kama angalau Kamati za Fedha zipewe taarifa ya namna gani *TARURA*inaendelea na pia *TARURA* iheshimu vipaumbele vya Halmashauri. Ingesaidia sana suala la kuzisaidia mamlaka hizi kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni *D by D* kumekuwa na hoja nyingi sana kwa upande huu zaidi kwamba Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wamekuwa wakigombana na Halmashauri, lakini kama mfumo huu *D by*

Dpolicy yake ingezingatiwa vizuri Wakuu wa Mikoa wakaelewa vizuri na ndio maana nikasema ni vizuri hata wanaochaguliwa, wachaguliwe kwa *ethics* zao, wachaguliwe kwa uwezo wao na sio kwa ukada wao, leo hii migogoro isingekuwa inaendelea katika Halmashauri zetu. Ipo hivi kwa sababu viongozi wetu wengi wa Mikoa na Wilaya wameshindwa kufuata maadili yao, wamekwenda kwa ukada, wamekwenda kwa ajili ya kuwaumiza Wapinzani au kuumiza watu waliopo chini yao. Matokeo yake imekuwa vurugu kila siku mpaka kila siku...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima na baadaye Mheshimiwa Ignas Malocha na Mheshimiwa Timotheo Mnzava wajiandae.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anazofanya za kutekeleza llani yetu ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020. Pia nimpongeze Waziri wa TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu. Vilevile nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Mkuchika, Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya pongezi, nitoe shukrani kwa Serikali, naishukuru Serikali kwa kutupatia shilingi milioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali yetu ya Wilaya pale Lugufu.

Naishukuru pia Wizara hii ya TAMISEMI kwa kutupatia shilingi milioni 800 kwa maana shilingi milioni 400 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kalya na shilingi milioni 400 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Uvinza. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba hilo, bado nina ombi kwenye sekta hii ya afya. Tuna ahadi alipokuja Waziri Mkuu, tarehe 29 Julai, 2019, alituahidi kwamba TAMISEMI mtatupatia shilingi milioni 800 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kazuramimba na Kituo cha Afya cha Kabeba. Mheshimiwa Waziri natambua kwamba mahitaji ni makubwa ndani ya nchi lakini unaweza ukatupatia nusu yake, unaweza ukatupa shilingi milioni 400 tukazigawanya shilingi milioni 200 zikaenda Kituo cha Afya cha Kabeba na shilingi milioni 200 nyingine zikaenda Kituo cha Afya cha Kazuramimba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru pia Serikali, nakumbuka nilichangia hapa kuhusiana na maboma, kilio chetu mmekisia kwenye zile shilingi bilioni 253 sisi kama Halmashauri ya Uvinza tumepokea shilingi milioni 375 kwenye shule kumi za sekondari. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais kwa sababu makusanyo yanakusanywa na ndiyo maana miradi ya maendeleo inaweza kutekelezeka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niende sasa kwenye ukurasa wa 125(ix) katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri umezungumzia kuhusu ununuzi wa magari kwamba magari kumi yatanunuliwa kwenda kwenye Halmashauri za Nyang'hwale, Buhigwe na nyinginezo. Mheshimiwa Waziri umefanya ziara kwenye Jimbo langu kwenye ile Timu iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais kwenda kuangalia migogoro ya ardhi na mipaka na umeona Jimbo langu ni kubwa sana na ulikuwa shahidi na Mawaziri wenzako, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Mheshimiwa Lukuvi mliona ni jinsi gani mama natawala Jimbo ambalo hata ninyi wanaume limewagusa. (*Makofî/Vigelejele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa kuona kwenye ukurasa huu wa 125, Halmashauri yangu ya Uvinza hamjatenga ipatiwe gari. Mkurugenzi na Wakuu wa Idara hawana magari na hizi Halmashauri ulizozitungumza ukurasa wa 125 ni Halmashauri mpya ambazo ndiyo mnatakiwa muwapelekee Wakurugenzi magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti kwenye *Vote 21* ya Hazina wametenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ununuzi wa haya magari, magari ya Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Nimelizungumza jambo hili na Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na yuko hapa, Katibu Mkuu (*Ndugu Doto*), Naibu Katibu Mkuu pia na mwanamke mwenzangu Kamishna wa Bajeti ili kwenye hii shilingi bilioni 20 miliyotenga ya ununuzi wa magari, naomba gari la Halmashauri ya Uvinza kaka yangu Mheshimiwa Jafo tulipate kwenye hizi pesa, usiponiletea mimi nitaona kuna upendeleo. Namtambua kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango amezaliwa kule Buhigwe lakini walianzaanza Uvinza ndiyo wakaenda kuhamia Buhigwe basi na mimi Uvinza niletewe gari la Mkurugenzi, kaka yangu Mheshimiwa Jafo naomba hilo ulipokee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 19 – 24, Mheshimiwa Waziri amezungumzia pia kuhusu majengo ya utawala ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi. Nimwombe pia kaka yangu Mheshimiwa Jafo, hivi kuna nini, mbona Uvinza haijazungumzwa na unajua fika kwamba tunayo majengo yanayosimamiwa na *TBA* lakini kwenye bajeti hii ya 2019/2020 tumeomba shilingi milioni 550 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Buhigwe, Uvinza na Kasulu lakini kwenye ukurasa huu wa 19 – 24, nasikitika Uvinza haijazungumzwa. Kaka yangu Mheshimiwa Jafo, naomba upokee, najua utanisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA*, ukurasa wa 83, nimeona kwenye bajeti ya 2018/2019 tulidhinisha shilingi bilioni 243.29 lakini hadi mwaka huu Februari *TARURA* wamepokea shilingi bilioni 136.02 sawa na asilimia 56. Kwenye hili naomba nizungumzie kwenye barabara zangu, mtandao wangu wa barabara ni Km.1230. Bajeti tuliyopangiwa mwaka jana ni shilingi milioni 490, bajeti ya ukomo tuliyopangiwa kwenye *TARURA* mwaka huu ni shilingi milioni 490, mtandao wa barabara ni Km.1230, nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Jafo hebu mtuongezee pesa *TARURA* ili tuweze kuchapa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nzungumzie kidogo mapato ya Halmashauri. Nilikuwa naangalia ukurasa wa 139, Halmashauri ya Uvinza ilipangiwa kukusanya shilingi bilioni 1.709 kwa bajeti inayoishia tarehe 30, tumekusanya shilingi milioni 850, tatizo ni nini, naomba nzungumzie kidogo vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivu vitambulisho vya wajasiriamali naviunga mkono, utaratibu ni mzuri, lakini kwenye utekelezaji kuna shida. Vitambulisho wamepewa Wakuu wa Wilaya ambao siyo Maafisa Masuuli, Maafisa Masuuli ni Wakurugenzi. Hebu sisi tushauri kama Wabunge, kule chini hivi vitambulisho tumeuliza, mimi niko Kamati ya Bajeti, tumemuuliza Waziri, hivi hizi pesa zinazokusanywa zinakwenda wapi? Tukaambiwa zinaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mapato mnayachukua kwa wale wajasiriamali wadogowadogo ndani ya Halmashauri zetu, kwa nini hizi pesa zisiingie kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri zetu? Kwa nini hizi pesa ziende kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali wakati mkitambua fika kwamba hiki ni chanzo cha mapato cha Halmashauri. Tunaomba Mheshimiwa Waziri mkae chini na Wizara ya Fedha mlizungumzie hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kidogo kwenye suala la watumishi wetu. Watumishi wengi hawajapandishwa madaraja kwa sababu wamekaimu miaka tisa, wanatakiwa wawe Wakuu wa Idara, wanashindwa kupandishwa vyeo kwa sababu wanaambiwa sio Maafisa Waandamizi. Hebu mliangalie hili, muwaruhusu wapandishwe vyeo yaani wathibitishwe kwenye nafasi za Ukuu wa Idara huku bado hawajawa Maafisa Waandamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hili, naomba nzungumzie suala la watumishi ambao walikuwa Kigoma Vijiji wakahamia Uvinza hawajalipwa pesa zao mpaka leo. Niliona kwenye Fungu la Hazina kuna kama shilingi

bilioni 350 kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi mbalimbali. Naomba na watumishi wangu wa Uvinza waweze kufikiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ndani ya nchi yetu. Leo mdogo Mheshimiwa Heche alizungumza kwamba kwenye Jimbo lake afya, elimu hali ni mbaya, lakini mimi kwa taarifa nilizonazo Serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imepeleka shilingi milioni 400 kwenye Kituo cha Afya cha Mkende kwenye Jimbo la Mheshimiwa Heche, imepeleka shilingi milioni 400 kwenye Kituo cha Sirari, imepeleka pesa za ujenzi wa jengo la Halmashauri kwenye Jimbo la mdogo wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikamsikia kaka yangu Japhary anazungumzia kwamba, unajua ninyi mnawenza mkaenda huku na sisi tukaenda huku, hivi mnazungumzia utawala bora, utawala bora kweli mnaufahamu ndugu zangu Wapinzani? Tumeona juzi Maalim Seif amehama CUF ameenda *ACT*, anaangalia tumbo lake haangalii chama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona humu ndani tulikuwa na *CUFA* na *CUFB*, leo nimemsikia Bwege anasema wote ni *CUF* moja. Sasa najiuliza huo ni utawala bora upi? Mlikuwa *CUFA* na *B*, kwa nini msiende *ACT*? Kwa hiyo, nini kinachoonekana hapa ni kwamba mmebak *CUF* hii hii ya Lipumba kwa ajili ya matumbo yenu. Sasa mnapokuwa mnaisema Serikali ya Chama cha Mapinduzi muwe mnajiangalia na ninyi. (*Makof*)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. HASNA S.K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la utawala bora...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hasna, muda wako umemalizika. (*Makofii*)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Muda wake umeisha, tunaendelea.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Sasa alitaka tukaangalie tumbo lake, ataturuhusu?

Pumbavu! [Neno Hili Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa chini nilijua umempaa taarifa.

MWENYEKITI: Hapana, umemaliza muda wako.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie dakika yangu moja.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasna, kengele ya pili ilishalia.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Ignas Malocha na baadaye Mheshimiwa Timotheo Mnzava ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba Mwongozo.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu.

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa subiri, ndiyo Mheshimiwa Stella, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 64, lugha alioitumia Mheshimiwa kabla, ametumia neno haya sana kwa Kiti, amesema pumbavu. Naomba afute, ni albu kubwa kusema neno kama hillo. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuita mpumbavu yeye?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib naomba ...

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesema, amesema tunaangalia matumbo yetu, nimeuliza tukaangalie tumbo lake yeye ataturuhusu? Yaani Mwilima ataturuhusu tuangalie tumbo lake? Amesema sisi tuko hapa kuangalia matumbo yetu, ataturuhusu tukaangalie tumbo lake yeye au Kiswahili kipi hicho? Maana ni kuangalia matumbo, sisi matumbo yetu tunayaona muda wote, sasa yeye tumbo lake anaturuhusu tukaangalie?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib, neno ambalo linazungumzwa na Mheshimiwa Stella ni pumbavu, kwa hiyo, kama umesema neno hilo naomba ulifute.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Naomba tusikilizane. Mheshimiwa Khatib, kama unajua umezungumza neno hilo naomba ulifute.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimesema hilo nafuta lakini na yeze aturuhusu tuangalie tumbo lake.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ignas Malocha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikaki za Mitaa). Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na mwenye afya njema katika siku ya leo niweze kushiriki kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nami naungana na Watanzania kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi anazozifanya, Watanzania wanaziona. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Jafo kwa kazi kubwa anayofanya, kijana huyu ni hodari, lazima tuseme ukweli, anafanya kazi vizuri sana. Niwapongeze Naibu wake; Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waitara, wanafanya kazi vizuri. Nimpongeze Katibu Mkuu, Eng. Nyamhanga na watumishi wote wa Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuanza, naomba nizungumzie barabara za vijijini. Barabara za vijijini ndiyo msingi wa maendeleo katika nchi yetu, kwa sababu huko

ndiko kunatoka chakula, kuna wananchi wanyonge na huko ndiko wananchi wanauza mazao kwa bei mbaya kutokana na hali ya barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliunda hapa chombo cha *TARURA* kwa matumaini mema tu kwamba kitaweza kutusaidia. Mimi nikiri kabisa kwamba chombo hiki ni kizuri na Watendaji wana uwezo wa kusimamia fedha vizuri kwa ajili ya kujenga barabara, shida iliyopo wanapewa pesa kidogo mno. Sasa matumaini ya Watanzania na sisi Wabunge tunashindwa kuelewa ni kwa namna gani hizi barabara zitajengwa kama tulivyokusudia. Tunaomba kwa kweli chombo hiki kiongezewe pesa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi katika Jimbo langu nina barabara sugu sana, lakini ninachokiona hata mgawanyo wa pesa hizo ndogo hauendi sawa, ni kama kuna upendeleo wa namna fulani. Nakuomba kabisa uagalie ukurasa wa 196, angalia mgao wa fedha katika Halmashauri ya *Sumbawanga DC* vilevile uende ukurasa wa 200 - 201 uone jinsi Halmashauri ya *Sumbawanga DC* iliyopata pesa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hapo twende kwa Mkoa mzima wa Rukwa, umepewa shilingi bilioni nne, mkoa wenyewe uzalishaji mkubwa na wenyewe barabara sugu na mvua nyingi ambazo zinaharibu barabara kila siku kupewa kiasi hiki siyo sawa. Kwa kweli naona jambo hili sio jema, mtafakari upya na maeneo niliyokwambia yafuatilie utaona kama ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie barabara sugu ambazo ziko katika maeneo yetu ambazo tulizipitisha kwamba walau zikitengenezwa hizi, zinaweza zikasaidia kiasi fulani. Barabara ya Kahengesa - Kitete pamoja daraja; barabara ya Kahengesa – Itela – Ntumbi – Illembu; na barabara ya Mawenzusi – Msia. Barabara hii Serikali iliwhi kutupa pesa shilingi milioni 400 lakini imeitelekeza maana yake zile pesa thamani yake itapotea kwa sababu hakuna nyongeza ilioongezeka ili barabara iweze kutengenezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ni barabara ya Mtowisa - Ng'ongo. Barabara hii ni ahadi ya Makamu wa Rais, hebu tumheshimu Makamu wa Rais, kwa huruma ya akina mama akasema hii barabara lazima itengenezwe kwa changarawe. Nashangaa mpaka sasa hivi sioni ahadi ile kama inatekelezeka na miaka inaendelea kuisha. Ni lazima tumheshimu mama huyu kwa kazi anazozifanya, walau tumpe upendeleo wa barabara hii iweze kutengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara Mihangalua - Chombe na Chombe – Kahoze. Hizi barabara nazozungumzia ni barabara sugu. Barabara zipo nyingi lakini hizi tulizitenga kwamba ni sugu, zikitengenezwa zinaweza zikapunguza kiasi fulani maumivu kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni katika ukurasa wa 5 ambapo Mheshimiwa Waziri umeelezea namna Serikali ilivyojipanga katika kujenga majengo ya utawala. Nimeangalia nikaona Sumbawanga DC ambayo ina jengo la utawala ilianza kujenga mwaka 2011 mpaka sasa hivi halijaisha, Serikali ilitupa shilingi bilioni 1.6 na mkataba wa jengo hili ni shilingi bilioni 2 na mwaka huu tuliomba shilingi millioni 700 lakini hatujapangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo limechukuwa miaka mwishowe litachakaa, watumishi watakosa pa kufanya kazi, kumbukumbu zitahifadhiwa wapi? Naomba Mheshimiwa Jafo ulione hili, jengo ni la muda mrefu, ni ghorofa moja, miaka imekuwa mingi na linachakaa na tuliomba pesa tunashangaa hamjatupangia. Tunaomba Mheshimiwa Jafo uliangalie jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la wakandarasi upande wa maji hawalipwi kwa wakati. Kama tatizo ni pesa kwa sababu tatizo la maji ni kwa nchi nzima, tulijadili kwa pamoja tutafute ufumbuzi kuliko wakandarasi wanafanya kazi muda mrefu wanadai pesa hawapati sasa tunaanza kushangaa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ahadi ya Serikali inavyosema miradi ya maji itajengeka, sijaona itajengeka kwa namna gani, kwangu mpaka sasa hivi nina wakandarasi zaidi ya wanne wanadai pesa hawajalipwa. Kwa mfano, mkandarasi wa mradi wa pale Ikosyi, alipeleka vifaa ameanza kujenga, mwishowe ameamua kuviiondoa kwa sababu hajalipwa na amedai kwa muda mrefu na nimefuatilia mara kadhaa nashangaa Serikali hajamlipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kuzungumzia upande wa afya. Kwanza kabisa, niishukuru Serikali mmetupa shilingi 1,500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, hongereni sana. Halafu mmetupa shilingi 400,000,000 kwa ajili ya upanuzi wa kituo cha afya na kwenye bajeti hii mmetupa shilingi 200,000,000 kwa ajili ya kupanua Kituo cha Afya pale Mpuli, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kuongezea Mheshimiwa Waziri uliangalie Jimbo liliyo na jiografia yake. Nashukuru kwa hiki mlichotupatia lakini hebu jaribuni kutanuka zaidi. Mimi Jimbo langu ni kubwa na jiografia ni mbaya, majimbo mengine yamepata vituo vyta afya vinne, vitatu sasa najiuliza, jimbo langu ambalo ni kubwa na Mheshimiwa Jafo umefika umeliona mpaka ukatuonea huruma, hebu jaribu huruma hiyo upeleke kwenye vitendo. Tunaamini kwa sababu utakuwa umesikia na ni kijana msikivu endelea kulingalia uweze kutuongezea kituo kingine cha afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie tatizo la gari. Jimbo langu halina gari la wagonjwa na mazingira unayajua, nimeomba gari hili karibu miaka mitatu, unaenda mwaka wa nne, naahidiwa sijapewa. Naomba na lenyewe hilo Mheshimiwa Jafo uweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni maombi ya fedha za kumalizia maboma yetu. Tuna zahanati 20 ambazo zimejengwa na wananchi kutoka usawa wa lenta na wengine wameweka na mabati, tunaomba tupewe fedha za kumalizia hizo zahanati vinginevyo wananchi watakata

tamaa. Tunavyo vituo vya afya kama vitano ambavyo wananchi wameshajenga majengo ya utawala wakaezeka tunasubiri kupewa fedha tuweze kumalizia ili yaweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile upande wa watumishi, tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi. Halmashauri ya *Sumbawanga DC* ina upungufu wa watumishi 667. Ukiangalia mgao unaotolewa unakuta sisi tumepata kidogo hata wale ambao wana nafuu wanapata watumishi zaidi. Sijajua ni vigezo gani vinatumika katika kugawa watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jamani mtuangalie maana *Sumbawanga DC* tuko vijijini, mara nyingi tukisema *Sumbawanga DC* mkija mnafikiri ni pale mjini, hapana, kuna mazingira magumu sana, Mheshimiwa Jafo umetembea umeyaona, hata Waziri Mkuu alipita akashangaa kwamba katika nchi hii kuna mazingira ya namna hii. Sasa kama hata viongozi mmeyaona si mtupendelee basi hata wa kutupa wa fedha. Kama mmekataa kugawa Halmashauri na Jimbo basi tupeni fedha za kukidhi mahitaji na shida za wananchi. Sasa kama kotekote mnatunyima wananchi watatufikiriaje? Tunaomba sana jambo hili muweze kuliangalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu, tuna maboma mengi. Kwenye Halmashauri yangu tuna maboma 259 ya madarasa na nyumba za Walimu tunaomba na hilo mfikirie. Tunashukuru mmetupa shilingi milioni 75, lakini ukilinganisha na maboma yale, kwa kweli hakuna uwiano, hazitoshi. Tunaomba na lenyewe hilo muweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni upande wa posho za Wenyeverti wa Vitongoji, Vijiji na Madiwani. Lazima tufike mahali tulitazame jambo hili. Hata miradi mikubwa tunayopeleka, ni wale ndio wanaosimamia, wanashinda kutoka asubuhi mpaka jioni bila posho. Hebu fikiria kama ungekuwa ni wewe, ungweza kufanya kazi hiyo. Tujaribu jamani kutafuta namna yoyote ya kuwafuta jasho hawa watu, angalau kama hatuwezi kuwapa mishahara, basi

tuweke hata posho, baada ya uongozi wake apate hata kiasi fulani cha kumfuta jasho, hata kama hapati mshahara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanafanya kazi kubwa sana. Kama hatuwapi posho ya kutosha hawa Madiwani basi tuwatengue posho hata mara moja baada ya miaka mitano mtu aweze kupata posho ya kufuta jasho lake kuliko kuacha kama jinsi ilivyo. Hawa watu wanafanya kazi kubwa mno. Nasi tunashuhudia tukienda tunashinda nao, unawenza ukachoka, wenyewe wanaendelea. Hebu jamani mjaribu kuangalia jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napenda kuishukuru Serikali, tulikuwa na kilio cha muda mrefu cha daraja la mto Mombasa. Nashukuru daraja hili linalekeea kukamilika, Serikali imetupa shillingi billioni 17,700,000,000/=, daraja hili linalekeea mwisho, tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tusiishie hapo, lengo la daraja ile ni kuunganisha mikoa mitatu. Kwa hiyo, tunaomba sasa Serikali ifikirie namna ya kuanza kujenga barabara ile kwa kiwango cha lami. Mkifanya hivyo, mtakuwa mmetutendea haki wananchi wa maeneo yale na ni maeneo kwa kweli yenye uzalishaji, hakuna zao linalokataa katika maeneo yale, lina rutuba nyingi sana. Mazao mengi mnayoyaona hata kule Mpanda, yanatoka Sumbawanga Vijiji; hata huko Mbeya Tunduma yanatoka Sumbawanga Vijiji. Kwa hiyo, ndiyo maeneo yenye uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali iweze kuangalia jambo hilo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. IGNAS A. MALOCHA Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Awali ya yote, nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mungu mwangi wa rehema aliyenijalia uzima na kuweza kuwepo humu ndani leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kutuletea maendeleo watu wa nchi ya Tanzania. Pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Utumishi wanafanya kazi kubwa na wasaidizi wao wote kwenye Wizara, tunaona kazi wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jambo moja kubwa ambalo amelifanya kwenye nchi yetu. Baada ya kuingia kwa Serikali ya Awamu ya Tano Mheshimiwa Rais amekuja na namna tofauti ya kuwapata Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Miji, Majiji na vile vile Makatibu Tawala wa Wilaya na watumishi wengine wa maeneo mengine, tofauti na utaratibu uliokuwa umezoleka mwanzoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limetusaidia kuondoa utendaji wa mazoea kwenye Halmashauri zetu. Kama kuna mtu ambaye analipiga vita, atakuwa na matatizo, lakini tunaojua tunaona kwamba jambo hili limetusaidia sana kupunguza urasimu na mazoea kwenye Halmashauri ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye eneo la afya. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, tunaishukuru sana Serikali sisi watu wa Korogwe. Mlichukua Hospitali ya Wilaya ya Korogwe ikaenda Halmashauri ya Mji lakini mmetupa shilingi bilioni 1.5 kutengeneza Hospitali ya Wilaya

na inajengwa pale Makuyuni na ujenzi umeanza. Tunaishukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukumbuke jambo moja, unapotoa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya au shilingi milioni 400 au 500 kwa ajili ya kituo cha afya halafu gharama za kuingiza umeme kwenye hospitali shilingi milioni 200, gharama za kuingiza maji shilingi milioni 150 na hakuna fedha nyingine nje ya hiyo inayotoka, hiyo shilingi bilioni 1.5; inatupunguzia majengo ambayo tungeweza kujenga kwenye hospitali hizi za wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba TAMISEMI itusaidie kukaa na Wizara nyingine kama ya Nishati na Wizara ya Maji. Sisi Korogwe alipokuja Mheshimiwa Waziri wa Maji nilimwomba kutusaidia kusogeza huduma ya maji kwenye hospitali ya wilaya tunayoijenga sasa hivi na alikubali. Bado tunapata shida kwenye upande wa umeme na zaidi ya shilingi milioni 190. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kuwasiliana na Wizara nyingine kuweza kutusaidia kwenye jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye kitabu humu ndani Mheshimiwa Waziri ametengea Korogwe shilingi milioni 200 kwa ajili ya kituo cha afya Kerenge, tunakushukuru sana. Wewe ulikuja Korogwe unajua shida iliyokuwa Korogwe kulingana na eneo la kujenga hospitali ile ya wilaya, pamoja na shilingi milioni 200 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kerenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo vituo vya afya vingine vitatu Korogwe. Mwaka wa fedha uliopita hatujapata fedha yoyote kwa ajili ya kituo cha afya. Kuna Vituo vya Afya vya Bungwe na Kituo cha Afya Magoma, vina hali mbaya. Ni vya muda mrefu. Mwaka 2018 aliyeokuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya TAMISEMI anayeshughulika na afya, mama yangu Zainab, alikuja Korogwe na alishaahidi watu wa Korogwe kwamba watapata shilingi milioni 500 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kituo cha Afya cha Bungu. Kwenye kitabu hiki sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana kaka yangu, Ubunge wenyewe ndiyo kwanza nimekuja juzi, namwomba, Kituo cha Afya cha Bungu chonde chonde tusaidie tupate hela tukatanue kile Kituo cha Afya. (*Makofi/Kicheko/Kigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo upande wa *TARURA*. Kwanza tuwapongeze *TARURA*, wanafanya kazi nzuri. Pamoja na changamoto za kibajeti, lakini wanajitahidi wanafanya kazi nzuri. Sisi Korogwe tuna Jimbo kubwa, jiografia yetu ni kubwa na siyo nzuri. Hela tunayotengewa ukilinganisha na maeneo mengine havilingani. Tunaomba mtupe kipaumbele watu wa Korogwe. Mwaka wa fedha uliopita tumetengeneza barabara 11 tu tena ni kwa vipande, lakini ziko barabara muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tunapojenga hospitali ya wilaya alipokuja Mheshimiwa Waziri, ukiangalia kwa upande wa juu kuna mlima, ndiyo inapatikana Tarafa ya Bungu. Ili ile hospitali ya wilaya iweze kuwa na faida kwa watu wa Tarafa ya Bungu ya mlimani, iko barabara inaitwa Makuyuni - Zege - Mpakani, Kwemchai - Makuyuni lazima itengenezwe. Bajeti ya kuitengeneza ni zaidi ya shilingi milioni 140. Kabla ya bajeti hii, nimekwenda *TARURA* zaidi ya mara tatu, nimekwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri zaidi ya mara nne nikiwaomba ili hospitali ile ya wilaya iweze kutusaidia watu wa Korogwe. Tusaidieni barabara hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kwenda Kizara; huko mahali mvua ikinyesha kuna eneo la Kizara na Foroforo ni kisiwani kwa sababu barabara ni mbovu. *TARURA* ukizungumza nao kwamba matengenezo yanahitajika; wanasema yanahitaji hela nyingi na hela tunayopewa ni ndogo, tunawaomba muwaongezee *TARURA* hela iweze kutusaidia kufanya hii kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa na shida kwenye upande wa madaraja. Ukiangalia hela wanayopewa watu wa *TARURA* kutengeneza barabara inakuwa ngumu sana kwa wao kutengeneza madaraja.

Ninalo daraja kule Korogwe linaitwa Daraja la Mswaha, ni zaidi ya shilingi milioni 180 kutengeneza lile daraja, lakini utakuta *TARURA* wanapewa shilingi milioni 400 kwa mwaka mzima wa fedha. Hawawezi kutengeneza daraja kama hilo. Wananchi wanapata shida, wanapata taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo daraja kule kwa Lukongwe, liko daraja linalotuunganisha watu wa Korogwe na wenzetu wa Bumbuli kule Mbagai, yamesimama kwa muda mrefu, wananchi wanashindwa kuvuka, wanapata shida ya kupita kwa sababu ya hela ndogo ambayo wanapata watu wa *TARURA*. Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana hebu tuangalieni, ili ile hospitali iweze kuwa na faida, tusaidie kwenye hizo barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Serikali imeweka msimamo. Yapo maelekezo kwamba hakuna kutoa maeneo mapya ya utawala; lakini kuna Halmashauri ya Mji wa Mombo imepewa Mamlaka ya Mji Mdogo tangu 2004. Miji mingine yote iliyopewa Mamlaka ya Miji Mdogo pamoja na Mji wa Mombo ilishakuwa Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwa ajili ya kupewa muda mrefu, jioghrafia ya Korogwe Vijijini ni ngumu. Mheshimiwa Waziri ndiyo maana hata kwenye eneo la kujenga hospitali tulipata shida kwa sababu ya aina ya jiografia ya Wilaya ya Korogwe. Pamoja na hayo maelekezo ya Serikali, naomba sana muangalie uhalisia wa jiografia za Wilaya zilivyo, ukubwa wa wilaya zilivyo kuweza kutafuta maeneo mapya ya utawala kwenye maeneo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa jambo hapa kuhusu Ofisi za Wakuu wa Wilaya kuingilia Ofisi za Halmashauri. Zimepigwa kelele nyingi sana. Natambua kwamba Ofisi za Wakuu wa Wilaya zimeanzishwa kwa mujibu wa sheria. Sheria ya Tawala za Mikoa, ukisoma kifungu cha 13 (1) na (2). Ukitasoma kile kifungu cha 14, kinasema Mkuu wa Wilaya ndio *principle representative* wa Serikali na wanasema

all executive functions zitafanywa na Mkuu wa Wilaya.
(*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujue tunasema Rais wetu ana sehemu tatu; kwanza, ni mkuu wa nchi; pili, ni mkuu wa Serikali; tatu, ni Amirijeshi. Mkuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ndio Wawakilishi wa Mheshimiwa Rais. Wanaonjaonja na haka kaharufu. Huwezi ukawa Mkuu wa Wilaya ukaona kwenye Halmashauri ndani ya Wilaya yako, Halmashauri inafanya vitu vya ovyo halafu ukaviacha. Ni lazima ufuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashahidi. Ziko Halmashauri ambazo Wakuu wa Mikoa walizua ziara za Madiwani za zaidi ya mamilioni ya shilingi na wakasaidia kuokoa hela za wananchi. Tunachokitaka hapa ni tuweke tu utaratibu mzuri wa namna gani hawa Wakuu wa Wilaya watashiriki kuzisimamia vizuri hizi Halmashauri zillizokuwa chini yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba TAMISEMI mlitoa Waraka Na. 2 wa 2010, unaonyesha ushirika wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya kwenye Halmashauri. Kuna mahali kuna upungufu kwenye ule waraka. Unasema Katibu Tawala wa Wilaya ambaye ndiye *technical person* kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya; naomba ni-declare interest, kabla sijawa Mbunge nilikuwa Katibu Tawala wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka unasema, ataingia kwenye vikao vya SMT, unasema ataingia kwenye Baraza la Madiwani, lakini kikao cha kila mwezi cha kufanya maamuzi ni Kamati ya Fedha. Katibu Tawala wa Wilaya haingii, anapata wapi taarifa za kumpelekea Mkuu wa Wilaya ili kujua wapi pana shida aweze kuingia hapo? Naomba sehemu hii ifanyiwe marekebisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Makatibu Tawala wa Wilaya na Makatibu Tarafa wamesahaulika. Yako maeneo Katibu Tawala wa Wilaya anakuwa *MC* wa kusherehesha kwenye shughuli wanapokuja wageni. Hii kitu siyo sawasawa.

Naomba wapewe heshima yao, naomba wakumbukwe na wasaidiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Halmashauri za Upinzani kwa mfano, ziko Halmashauri ambazo Mabaraza ya Madiwani yanataka kufanya maamuzi kinyume hata na maelekezo ya Serikali, kinyume hata na sera za nchi. Huwezi ukaacha Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa kuingilia kwenye Halmashauri za namna hiyo. Ni lazima uingie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kidogo kwenye eneo la utawala bora. Kwanza nilimsikia ndugu yangu, baba yangu Mheshimiwa Ally Saleh asubuhi alisema, ni kweli tuna uhuru, kila mtu ana uhuru na uhuru upo kwenye Katiba...

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba hii inayotoa huo uhuru, kwa mujibu wa haki za binadamu...

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu

T A A R I F A

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba siyo wajibu wa Wakuu wa Mikoa wala Wakuu wa Wilaya kuingilia Halmashauri. Ofisi za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kazi yao ni kulshauri Halmashauri. Kwa hiyo, wao hawana hiyo mamlaka wanayotaka kupewa na Bunge lako Tukufu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnzava.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnzava kwanza pokea hiyo taarifa ya mwanzo.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siipokei hiyo taarifa kwa sababu sheria iko wazi kwamba Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ndio wenye jukumu la kusimamia; na hiyo iko kwa mujibu wa sheria siyo kwa matakwa ya mtu. Huwezi kusimamia, halafu mtu unayemsimamia afanye mambo ya ovyo halafu usiingilie, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye utawala bora. Ibara ya 30(2) inaweka utaratibu wa hizo haki tunazozisema. Unaposema huna haki ya kusema, una haki ya kukusanyika; ibara hii imetoa mwanya kwa nchi kutengeneza Sheria ya Kusimamia Utaratibu huo. Huwezi ukakusanyika kama hali ya usalama inahatarishwa, huwezi ukakusanyika kama kuna jambo haliendi vizuri. Hiyo ni katiba na hakuna katiba inayovunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hoja ya mama yangu, namheshimu sana mama yangu Mheshimiwa Ruth Mollel, kuna hoja mbili kwenye ukurasa wake wa 17 na 18 kwenye hotuba yake, anasema TAKUKURU iache kupeleka watu Mahakamani...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: ...mpaka itakapoweza kupata ushahidi wa kutosha.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Pia anasema kwamba kushindwa kwa kesi nyngi za TAKUKURU mahakamani ni ishara...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa mwenyekiti, umenipa ruhusa au!

MWENYEKITI: Taarifa kuhusu nini? Kwa sababu anazungumza kitu ambacho kiko kwenye kitabu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, si kawaida kupiga taarifa!

MWENYEKITI: Ananukuu kitabu kilichoelezea. Hebu endelea Mheshimiwa Timotheo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kwenye kitabu chake kwamba kushindwa kwa kesi nyngi za TAKUKURU Mahakamani ni ishara kwamba kesi hizo siyo za haki.

Mheshimiwa Mwewayekiti, sisi tutakuwa nchi ya ajabu kweli. Hivi ni lazima kila anayeenda Mahakamani ashinde? Hilo ni swali l a kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hebu tuulizane, hivi ni nchi gani ambayo eti mpaka ushahidi wote ukipatikana ndiyo unaenda kumpeleka mtu Mahakamani. Hili ni jambo endelevu, wakati mwininge unaweza ukamkamata mtu, ukampeleka mahakamani...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Ukaendelea kuafuta ushahidi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnzava, malizia.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza TAKUKURU, nataka waendelee kufanya kazi vizuri...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: ...waimarishe Kitengo cha Uchunguzi, waimarishe Kitengo cha *Prosecution* ili wafanye kazi nzuri kwa ajili ya kutetea nchi yetu na kupingana na mafisadi wanaoifisadi nchi yetu. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Midimu, baadaye Mheshimiwa Anna Gidarya ajiandae.

MHE. ESTER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya, Mwenyezi Mungu ambariki sana. Pili, nampongeze Makamu wa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya, Mwenyezi Mungu ambariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampogeza Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya, Mwenyezi Mungu ambariki sana. Nampongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa hotuba nzuri waliyoisoma, inaridhisha, imesheheni mambo mazuri. Pia nampongeza Mheshimiwa Mkuchika, Waziri wa Utawala Bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia. Naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutujengea Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Simiyu, ambayo imezinduliwa na Mheshimiwa Rais juzi, inafanya kazi vizuri. Hata hivyo, kuna changamoto katika hospitali ya mkoa. Changamoto ya kwanza, hatuna genereta ya dharura umeme ukikatika; hospitali hiyo haina uzio na ina

upungufu wa vifaa tiba. Naiomba Serikali iliangalie hilo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inazozifanya, imetuletea shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya; Wilaya ya Itilima, Busega na *Bariadi DC* mchanganuo wake, kila Wilaya inapata shilingi bilioni 1.5. Hospitali hizo zikikamilika, nina imani matatizo yatapungua hususan katika wilaya hizo nilizozitaja; huduma itakuwa karibu; na vifo vya akina mama na watoto havitatokea tena. Vikitokea ni bahati mbaya, siyo kwamba vinatokea kwa kukosa matibabu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu katika hospitali yetu teule ya Mkoa wa Simiyu haina Madaktari Bingwa wa magonjwa ya akina mama; na hospitali hiyo ina msongamano sana. Inahudumia wilaya tatu; Busega, Bariadi na Itilima. Msongamano unakuwa mkubwa sana, akina mama wakienda pale, inachukua siku mbili au tatu kupata matibabu. Tunaiomba Serikali itusaidie kutuletea daktari wa magonjwa ya akina mama kwa vile akina mama tuna maradhi mengi. Kuna maradhi mengine yanahitaji kumwona Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Akina Mama. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuboresha Hospitali ya Wilaya ya Maswa. Imetujengea genereta nzuri, imetujengea *x-ray* nzuri, inafanya vizuri. Vilevile imetujengea wodi ya akina mama na watoto, tunapongeza sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda sasa Wizara ya Maji. Naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutuletea mradi wa maji wa Ziwa Victoria. Mradi huo ukifika utatusaidia wananchi wa Mkoa wa Simiyu hususan akina mama kwa sababu muda mwangi wanaupoteza kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo. Nina imani mradi huo ukifika, tutafanya kazi za maendeleo, tutalima mboga mboga, *tuta-supply* Dodoma na Dar es Salaam mpaka nje ya nchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kuna changamoto Wilaya ya Maswa kata ya Zanzuni. Kuna mradi wa chujio ambao umechukua muda mrefu sana. Kila kandarasi akiongezewa muda mradi huo umeshindwa kukamilika. Nashindwa kuelewa tatizo ni nini, huku wananchi wa Maswa wakiendelea kunywa maji ambayo siyo safi na salama. Fedha zipo ila mradi haukamiliki. Naiomba Serikali iangalile hilo kwa mapana yake. Kila siku nikisimama hapa hilo nalipigia kelele. Naomba sasa Serikali yangu kwa vile ni sikivu, iweze kunisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niipongeze Serikli kwa mradi mkubwa wa maji wa Busega ambao upo kata ya Ramaji. Niliuliza swalii juzi juzi hapa Bunge lililoisha. Mheshimiwa Naibu Waziri alinipa majibu mazuri sana, akasema, mradi huo utaanza kufanya kazi mwezi wa Nane. Nami nimeenda kufanya ziara, nimewaambia akina mama, mradi huo utaanza kufanya kazi mwezi wa Nane. Kwa hiyo, wananchi wa Busega wanasubiria hiyo neema ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya, Mwenyezi Mungu ambariki sana, tunamwombea, atabaki kuwa juu, atabaki kuwa mawinguni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Esther. Tunaendelea na Mheshimiwa Anna Gidarya na baadaye Justin Monko ajiandae.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hii Wizara ya TAMISEMI. Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kwa kuwapa pole viongozi wangu, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge na dada yangu Mheshimiwa Ester Matiko, kwa muda mrefu kuwepo mahabusu kwa ajili ya dhuluma ama

kutokufuata utaratibu na miongozo ya utawala bora kwa watu wanaoshikilia hayo madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitangulize kwa kusema utawala bora ni matokeo ya msingi bora wa maadili mema. Misingi hii inakubalika na inatokana na mtawaliwa na yule anayemtawala mtu mwingine. Kumekuwa na vurugu nyingi kwa baadhi ya watendaji wa Serikali hususan Wakuu wa Mikoa na ma-*DC*. Kumekuwa na mkanganyiko kati ya Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi katika halmashauri nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjambe wa Kamati ya TAMISEMI, tumekutana na kesi nyingi, mwaka jana tumeshauri, lakini bado mwaka huu hizo vurugu zinaendelea, natumai Waziri akija atatuambia hizi kero za kila siku zitakwisha lini? Utawala bora ni pamoja na kulinda wale watu unaowaongoza, lakini katika nchi yetu imekuwa ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yanayoudhi, kuna mambo mengi ambayo yanaleta hitilafu tunasema rais anafanya kazi nzuri nami nakubali ni kweli anafanya kazi, lakini wao wenyewe humu ndani ndiyo wanaomwangusha rais. Tusifurahishane hapa hata Rais mwenyewe anajua kwamba wao ndiyo wanaomwangusha, wanamwangusha vipi? Amepewa dhamana kubwa ye ye kwenda kutawala kwa ile ngazi ambayo inampasa ye ye lakini hawampelekei ripoti nzuri. Huku chini wanakuja kwa ajili ya kukamiana, kila mtu kwa nafasi yake akatekeleza wajibu wake, wanatuletea Wakurugenzi ambao hawajui hata mipaka ya kazi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Mikoa vile vile, kila mtu kwenye hizo nafasi zao amejifanya Miungu watu, tena wengine wamewaleta wanathubutu kabisa wanakwenda kwenye shughuli za ufunguzi wa miradi, ni *DED* amevaa shati ya CCM. Tukisema haya mnatuombea miongozo, kuhusu utaratibu kwamba siyo kweli, kwamba ma-*DED* na ma-*DAs* ni makada wa CCM, hata hilo mnakataa? Ushahidi tunao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na shida kubwa, kuna *issue* ya TAKUKURU, nchi hii watu wanaogopa hata kufanya biashara. TAKUKURU wakikuweka ndani leo hii utakaa miezi miwili wanasema uchunguzi bado, lakini kesi wamezibadilisha. Hivi mtu ambaye hana hata shilingi milioni 10 benki unambadilishiaje kesi kwamba ni uhujumu uchumi na utakatishaji fedha, anatakatisha makarasi? Wasaidieni watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala ni kitu cha msimu tu, tutapita, tutarudi mitaani, tutakoseana heshima, lakini *at least* ungali wewe kama unajua unaishi je, watoto wako unawabakizaje huku nyuma? Tumejenga athari, moyo ya watu inalia, wamekuwa waonevu, uchumi kama unashuka wasiende kuumiza watu kwa ajili ya kuwakamata wanatafuta pesa. Tufungiane humu ndani tutafute namna bora ya kuulinua uchumi wa nchi hii. Hivi wanavyowakamata hawa wafanyabiashara, wanafikiri kwamba hawa wafanyabiashara ndiyo wachangiaji wakuu wa mishahara. (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anna subiri taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Wenyekiti, nataka kumpa taarifa dada yangu anayezungumza kwamba, waliokuwa makada wa CCM kuwa ma-DC na Wakuu wa Mikoa wala siyo shida, kwa sababu hata yeye alikuwa kada wa CCM lakini leo hii ni Mbunge wa CHADEMA, anaamini katika kazi yake mpya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anna.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona alikuwa anataka nimwone tu, kwa sababu mdogo wangu nataka tu nimwambie katika hizo ngazi, mimi nilikuwa

CCM na najua utaratibu unaoendelea ndani ya CCM. Kwa hiyo ninachokizungumza siyo kwamba nabuni, nina juu .(Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye tume ya haki za binadamu, kumekuwa na mazuo ya mikutano ya hadhara. Hivi leo hii kama Mbunge wa Upinzani wa Jimbo ananyimwa asifanye mikutano kigezo kikuu nchi nzima kumekuwa na sababu wanasema, intelejensia, hivi intelejensia iko kwa Wabunge wa CHADEMA tu, halafu mnawatuma polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe. Naomba niendelee asinipotezee muda.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, subiri taarifa hiyo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hakuna Mbunge wa Jimbo anayezuiwa kufanya mikutano kwenye maeneo yake. (*Makof*)

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

MHE. MICH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anna umeisikia hiyo taarifa? Hakuna Mbunge anayekatazwa kufanya mkutano kwenye Jimbo lake.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa.

MHE. MCH.PETER S. MSIGWA: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Haya Kuhusu Utaratibu.

MHE. MCH.PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a) Mbunge hapaswi kutoa taarifa za uongo.

Mheshimiwa mwenyekiti, Mbunge aliyesimama sasa hivi hapa anasema Wabunge hawazuiwi kufanya mikutano kwenye maeneo yao. Mimi nimekuwa mhanga na nimelalamika mara nyingi nakataliwa, Wabunge wengi tunakataliwa kufanya mikutano kwenye maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anasimama hapa anasema uongo, kwa nini Mbunge unasema uongo na Wabunge wenzako tupo? Tunaomba afute uongo huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter Msigwa hata na mimi naelewa kwamba Mbunge hakatazwi kufanya mkutano kwenye eneo lake.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Tuendelee Mheshimiwa Anna.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ulindwe. Mimi sijazoea kujibizana na watu wenyе umri wa baba zangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu, twendeni tukajenge nchi kwa maslahi mapana ya vizazi vyetu vya baadaye, tutasifiana humu lakini ukweli wanaujua miyoni mwao na Biblia inasema, ole wako mafiki. Sasa tusinifikiane humu ndani, mikutano ni kweli wanazuia lakini kwa nini wanakimbia vivuli? Hilo wanalijua kwa nini wasituruhusu tukafanya mikutano, tukutane jukwaani kwa hoja, wasitufungie kwenye chupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie mambo machache tu kwa ajili ya Taifa hili. Huku ndani watu tunaenda na *interest* za vyama lakini hao hao wanaopiga kelele humu ndani kwenye maeneo yao hakuna kitu. Kuna halmashauri nyingi hazifanyi vizuri katika mapato ya ndani, tuache vyama twendeni kwenye halmashauri zetu, wananchi wanataka nini. Maendeleo yanaletwa sisi tumetumwa huku kwa ajili ya kutetea wananchi, tumekuja hapa tunapongezana, ni *interest* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni halmashauri kama sita hazikufanya vizuri na wamo humu wanaotetea. Mfano mzuri ni Mkoa wa Mtwara, Halmashauri ya Masasi imefanya kwa asilimia 10.95, Nanyumbu asilimia 10.44, Tandahimba asilimia 13.22, wastani ule wa mkusanyo ni 11.53. Leo tunasifiana huku wanasema wamefanya kazi nzuri, kwa nini hawakushauri huko kwenye halmashauri zenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nsimbo ni halmashauri mojawapo imetuangusha 23.5, Mlele 26.3, Tunduru 27, sasa leo hii hapa tukisema tuambizane kwa nini tunahangalka humu kupeana taarifa kusifiana tu, haiwezekani, tusemane humu ili tukajenge kule kwa wananchi. Tumekosa umoja humu kwa ajili ya hili Taifa kwa sababu kuna watu wanajipendekeza huko. Halafu wanaojipendekeza huko kwa taarifa yao jamaa mwenyewe anapiga mzigo, sasa wafanye kazi na wao wasimfurahishe furahishe humu. Bahati nzuri ye ye huwa haendi na upepo anafanya kazi, haya twendeni. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya malizia dakika moja.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ni halmashauri mojawapo pia yenye madeni makubwa. Halmashauri inadaiwa milioni 112 na *CRDB* benki, asilimia 20 ile ya vijiji haipelekwi, leo hii hapa tunasema kila kitu kimefanyika, kimefanyikaje? Halmashauri inadaiwa, makusanyo ya ndani yanaenda kulipa madeni ya mikopo ya Madiwani, mtapata wapi maendeleo. Halafu huku mnaogopana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *issue* moja ya mwisho tu dakika zangu hizo zilizobaki. Kuna *issue* ya Mfuko wa Jimbo, Wakurugenzi wamekuwa wamiliki wa Mifuko ya Jimbo, Mkurugenzi ana uwezo wa *ku-host* pesa za Mfuko wa Jimbo na kule kuna akinamama wanakufa kwa ajili ya kukosa dawa. Hawataki hizi pesa zifanye maendeleo na kazi ya Mfuko wa Jimbo siyo kwenda kumaliza miradi ni kwenda kuchochaea maendeleo. Sasa kwanini Wakurugenzi hawa wasichukuliwe hatua? Au basi kama hawajui waambiwe utaratibu na mipaka yao ya kazi, Wakurugenzi wanasingana mno na ma-*DC* na Wabunge.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anna, ahsante sana.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Monko, baadaye Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nami fursa ya kuweza kuchangia kwenye wizara zetu mbili hizi, Wizara ya TAMISEMI pamoja na Utumishi na Utawala Bora. Kwanza kabisa ningependa nianze kwa kutoa shukrani nydingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudini kubwa ambazo inafanya katika kujaribu kutatua matatizo, kero na changamoto walizonazo wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini naishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kwenye sekta ya afya ambapo tumepata jumla ya shilingi bilioni mbili na milioni 600 kwenye ujenzi wa hospitali ya wilaya pamoja na vituo viwili vya afya. Vile vile kwenye sekta ya elimu tumepata jumla ya shilingi bilioni moja milioni tisa na laki sita. Hizi zote zimekwenda kutatua changamoto mbalimbali kwenye jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia Serikali tulipata fedha za Mfuko wa Jimbo shilingi milioni hamsini na

tisa na laki moja ambazo kwa kweli zimekwenda kwa kiasi kikubwa kuchangia changamoto za ujenzi kwenye kata zetu zote 21. Kwa hiyo naishukuru sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudu kubwa ambazo Serikali yetu imefanya, ziko changamoto mbalimbali ambazo ningependa njaribu kuzisemea hasa nikianza na sekta ya elimu. Kwenye sekta ya elimu Mkao wetu wa Singida bado haufanyi vizuri sana katika masuala ya matokeo, lakini ziko changamoto kadhaa ambazo zinachangia kutokufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto hizo ni miundombinu. Kazi kubwa ya Serikali imefanyika na hasa kwenye jimbo langu nami nilipata pia shilingi milioni 300 kwenye kujenga maboma 24. Nalpongeza sana Serikali kwa hilo. Kwa shule za msingi peke yake yako maboma 68 ambayo wananchi wamekwishayaanza kwa muda mrefu na bado hayajakamilika mpaka leo. Ukienda kwenye shule za sekondari, uangalie kwenye shule za sekondari kwenye Jimbo langu pale maboma zaidi ya 69 ya maabara peke yake hapo hujagusa nyumba za Walimu, mabweni, matundu ya vyoo na vitu kama hivyo. Kwa hiyo bado tunayo changamoto kubwa kwa kweli kwenye kuwekeza, Serikali kuwekeza ili kuweza kusaidia juhudu hizi za wananchi. Maboma haya yameanzishwa mengine yana muda mrefu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya afya, ninayo maboma kwa mfano kwenye Kata ya Ngimu liko jengo ambalo lilianzishwa na wananchi kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita na mpaka leo halijaweza kukamilishwa. Ukienda pale Kata ya Makuro vile vile na sasa hivi wananchi wengi wameanza sasa kwenye kata nyingine vile vile, Kata ya Msisi wameanzisha ujenzi wa jengo la kituo cha afya, ukienda Kinyajigi pale wameanzisha. Juhudi hizi za wananchi zinahitaji kuungwa mkono na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ombi langu kwa Serikali ni kwa Serikali kuongeza bajeti hii ya kukamilisha

maboma ambayo tayari wananchi wamekwishayaanzisha kwa nyakati tofauti na wamefanya kazi kubwa ili tuisiwakatishe tama. Tukumbuke kwamba uwezo wa kuyamaliza majengo yale haupo kwa wananchi kwa sasa kwa sababu miradi mingi ya Serikali ambayo inakwenda iwe ni hospitali za wilaya, vituo vya afya, majengo ya shule wananchi wanatakiwa kuchangia asilimia 20 ya maeneo hayo. Kwa hiyo niombe sana Serikali tuongeze bajeti ya maendeleo katika kukamilisha maboma haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ambalo linatoa duni kwa kweli kwenye sekta ya elimu lakini vile vile na huduma za afya ni watumishi tulionao kwenye sekta zetu. Nitatolea mfano wa Jimbo langu la Singida Kaskazini, kwenye sekta ya shule ya msingi peke yake tunahitaji waalimu zaidi ya 1,733 hivi tunavyozungumza tuna waalimu 860 sawa sawa na asilimla 49.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye sekta nyingine ukienda kilimo unakuta watumishi wako 16, kwenye vijiji 84 na kata 21, ukienda kwenye shule za msingi upungufu wa Walimu na maeneo mengine. Ni kweli Serikali kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Serikali ilitoa ajira na kwa mwaka uliopita ajira 4,811 za Walimu. Idadi hii ya ajira iliyotoka kwenye sekta ya elimu peke yake ni ndogo sana. Ukijaribu kuangalia kwenye takwimu ambazo zipo za usajili wa wanafunzi kwa mwaka wa jana, mwaka huu ambao ndio tunaendelea nao peke yake wamesajiliwa wanafunzi wa elimu ya awali na shule za msingi kwa zaidi ya wanafunzi 2,900,000 ambao peke yake kwa idadi hiyo ilitakiwa wapatikane Walimu ambao watahudumia wanafunzi hao Walimu zaidi ya 65,550.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona karibu asilimia 36 ya Walimu wote waliojiriwa mwaka jana wanakwenda kufanya kazi tu ya kuelimisha wale wa darasa la awali na darasa la kwanza. Kwa hiyo bado tunalo tatizo kubwa, niombe sana Wizara ya Utumishi pamoja na TAMISEMI ambazo zote bahati nzuri ziko chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Rais, waangalie namna ya kuweza kuongeza ajira kwa watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo twende pamoa na maslahi ya watumishi ambao kama tulivyosema kwa zaidi ya miaka mitatu sasa bado watumishi hawajaongezewa mishahara. Idadi ya Walimu tulionao tukumbuke hawa ni wale ambao tunao kwenye takwimu, wengine wako masomoni, wengine wana mashauri mbalimbali, ninayo, naweza nikatolea mfano wa Shule moja ya Msingi Mwasauya ambayo ina Walimu saba, watatu hawapo, wako masomoni, mmoja tayari ana mashauri, wanaoingia darasani ni Walimu watatu kwa shule nzima yenye wanafunzi zaidi ya 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii hatutegemei kuwa na miujiza sana ya kufanya vizuri. Kwa hiyo, niombé sana hasa kwa mikoa hii ambayo haifanyi vizuri kama Mkoo wa Singida tupewe kipaumbele cha kupewa watumishi wa kutosha na kuwapunguzia matatizo Walimu hawa ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu. Madarasa bado hayatoshi na wengi uwiano kule kwetu unafika mpaka kwa Mwalimu mmoja wanafunzi mpaka zaidi ya 100. Kwa hiyo, naomba sana Wizara iangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la *TARURA* tunawapongeza sana. Tumeunda Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji lakini nami pia nilikuwa najaribu kuangalia katika mgawanyo wa fedha za *TARURA* ambao wamekwenda kwenye bajeti ya mwaka huu, yako maeneo mengi ambayo kwa kweli tumepata fedha kidogo. Mkoo wa Singida peke yake tumepata bilioni nne na milioni mia tano, lakini ziko halmashauri hasa kwenye majiji, manispaa moja inapata zaidi ya bilioni saba, zaidi ya bilioni sita wakati Mkoo mzima wa Singida ni bilioni nne na milioni mia tano peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana ndugu Mheshimiwa Jafo, mjaribu kuangalia, tunayo matatizo makubwa sana kwenye barabara zetu kule vijiji na tukiendelea kutoa fedha kiasi kidogo kiasi hiki kwa kweli wananchi wetu watapata matatizo sana. Mimi kwenye jimbo langu yako maeneo mengi, iko barabara ambayo tuliiomba kwa Mheshimiwa Rais kutoka Kinyeto – Kinyagigi – Meria

inakwenda mpaka Sagara kule lakini naona haijatengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatujatengewa fedha kwenye baadhi ya madaraja na maeneo mengine, kwa mfano tunalo Daraja la Songa, Kinyeto - Ilongero pale Ntambuko lakini tuna eneo la Mgori – Kikio, haya ni maeneo sugu ambayo tunayo lakini ukienda kwenye fedha ambazo sisi tumetengewa kwenye maeneo hayo ambayo ni ya matengenezo ya dharura sisi maeneo korofii hatujatengewa fedha hata senti moja lakini ukienda pia kwenye marekebisho pale hatujatengewa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana muende mkafanye *review* ili pia Halmashauri ya Singida DC waweze pia na wao kupata fedha zitakazoweza kutosheleza. Barabara hizi tunazozungumzia ni muhimu sana kwa uchumi wa Jimbo la Singida Kaskazini.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae. (*Makofi*)

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia walau maneno machache ya kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa shukurani zangu za ujumla kwa Mheshimiwa Jafo pamoja na watendaji wenzake wote kwenye Wizara kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana katika kuhudumia

Wizara hii nyeti kabisa kwenye nchi hii. Mimi nilitegemea sana kwa sababu TAMISEMI ndiyo kiini au injini ya maendeleo kwenye nchi hii hata Wabunge wenzetu wote wangeendelea kuona umuhimu wa kukupa moyo na kuendelea kukushawishi na kuendelea kukueleza maeneo ambayo wanadhani yanatakiwa kufanyiwa kazi badala ya kuendelea kulalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia sekta ya afya. Nafahamu Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa sana. Mimi natoka Jimbo la Nyamagana. Naposema Nyamagana unafahamu ndiyo kitovu cha Mkoa wa Mwanza. Tunashukuru sana kwa mgao wa vituo vingi vya afya na Nyamagana tunacho kituo kimoja cha afya chenye sifa ambacho umetupa sasa hivi kimeshakamilika. Nikushukuru tena kwa kutuongezea kituo cha pili kule Fumagira. Imani yangu ni kwamba kituo hiki kikikamilika tutakuwa tumeendelea kupunguza sana tatizo la vifo vya mama na watoto ambao kiukweli wanahitaji huduma za karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi Halmashauri peke yake, nimpongeze sana Mkurugenzi wangu pamoja na watendaji wote, Madiwani na Meya kwa kuhakikisha tunajenga zahanati sita mpya kwa fedha za mapato ya ndani. Hii ni hatua kubwa sana na tunaposema Hapa Kazi Tu, hii ndiyo tafsiri yake sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo moja kubwa ambalo Mheshimiwa Waziri inabidi sasa hivi ukimbie nalo, baada ya ujenzi wa hivi vituo vya afya vyote na hospitali za wilaya, jambo kubwa tulilonalo sasa ni upatikanaji wa vifaa. Tunafahamu vinatoka kwa awamu, sasa hivi vimeanza kwa awamu ya kwanza lakini umekwenda karibia *phase* nne ya ujenzi wa vituo vya afya. Kwa hiyo, ni jambo zuri sana tukifanya haya mambo kwa haraka ili wananchi waone matokeo tunayoyasema kwa vitendo kama ambavyo umeshaanza kupeleka vifaa kwenye vituo vingi vya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa sababu ya muda nizungumze juu ya *TARURA*. Mheshimiwa Waziri katika jambo ambalo naendelea kukupongeza sana kila siku ni uamuzi wako wa kutoa mawazo na Baraza likaazimia na Mheshimiwa Rais akaidhinisha kuwa na chombo kinachoitwa *TARURA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema mimi ni muumini mkubwa wa *TARURA* kwa sababu nimeona matokeo yake lakini najua namna ambavyo *TARURA* inaweza kuja kuwa mkombozi wa miundombinu ya barabara kwenye nchi hii hasa kwenye maeneo ya vijijiini na mjini. Juzi nimesikia wakati unazungumzia hapa ripoti ya *CAG*, *TARURA* wamepata hati safi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mkurugenzi/*CEO* wa *TARURA* Ndugu yangu Self pamoja na Mhasibu Mkuu Ndugu yangu Nyaulinga kwa namna ambavyo wamekuwa wakishirikiana vizuri na watendaji wao wote hata kupata hati safi. Endelea kuwawekea mkazo, zaidi ni kuhakikisha fedha zinapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyamagana napata shilingi billioni 3.5 lakini fedha hizi ukililinganisha ukubwa wa mji na sifa ya mji na miundombinu iliyopo hatujawahi kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami. Hatuwezi kuendelea kujenga au kuboresha barabara za vumbi. Kwa hiyo, niwaombe sana Watendaji wa *TARURA* waangalie kwenye kitengo cha barabara za lami kwenye Jiji la Mwanza tutakapoongeza barabara za lami walau kutoka Igoma - Buhongwa, kutoka Mkuyuni kwenda Mandu kuititia Mahina, kutoka Buhongwa kwenda Nyakagwe na kule Bulale tutakuwa tumefungua mji huu na sifa yake itaonekana. Mimi sishangai sana kwa sababu haya mazuri tusipoyasema leo tutayasema lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Madiwani, nimekuwa Diwani na nakubaliana na suala la posho zile za mwisho wa mwezi, Serikali inaendelea kulifanyia kazi. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri umetoka Waraka

unaosisitiza *sitting allowance*, Mheshimiwa Diwani anayetoka kilometra 18 anakuja kulipwa Sh.10,000 ya nauli, hii siyo sawa. Maelekezo kwenye Waraka yako wazi kwamba Diwani apewe malipo haya kulingana na uwezo wa Halmashauri inavyokusanya mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo kwenye Halmashauri kama ya Jiji la Mwanza na Mkurugenzi wangu hawezি kutumia nguvu kwa sababu Waraka umemuelekeza kutumia Sh.40,000 na Sh.10,000. Mheshimiwa Waziri, fungua sasa kwamba Halmashauri itoe posho ya kikao kwa siku kulingana na uwezo wake wa mapato ya ndani. Ukifanya hivi, mwanzo walikuwa wanalipwa Sh.100,000 na mimi nilikuwepo pale tunalipwa Sh.100,000 ukija kwenye kikao, nauli na kadhalika angalau unaweza kuhudumiwa hata wapiga kura wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo, najua bado nina dakika tano baada ya kengele hii, yako maneno mengi yanaenea kwenye hii nyumba. Mimi niwasihii Waheshimiwa Madiwani yako maneno yanasema ashindwaye haishi maneno lakini sote tunafahamu hapa tunapokuja kujadili bajeti na bajeti tunayokwenda kujadili tunafanya makisio. Hivi leo ukikisia kupata Sh.10,000 ukaishia kupata Sh.8, unamlamu nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishia kulaumu bajeti tunayoipata, hatuoni mambo ambayo Serikali imefanya. Kila mtu akisimama wanabeza *Stiegler's Gorge* na ndege lakini wanashahau Serikali ya Awamu ya Tano kutoka wanafunzi wa vyuo vikuu 30,000 mpaka 42,000, zaidi ya shilingi bilioni 420 zimetoka hapa. Hili siyo jambo jema la kushukuru ndugu Waheshimiwa wa upande wa kule? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize, tunasema hivi kutoka miundombinu kwenye zaidi ya shule 500, zaidi ya shilingi bilioni 100 zilizofanyiwa ukarabati na kujengwa hili siyo bora kuliko yale mengine tunayoyasema? Tumezungumza hapa tunasema, hivi leo unapozungumzia ujenzi wa vituo vya afya zaisdi ya 300, hospitali za wilaya zaidi ya 67, unabeba hata hili? Hatuoni haya? Tunajadili mipango ya kufikirika...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwakajoka kaa nitakushukia jumla jumla.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojadili habari ya bajeti, bajeti ni matarajio. Kama tulipanga kufikisha shilingi bilioni 1 tukaishia shilingi bilioni 2.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 vyama vya upinzani viliundwa, malengo yao ni kuchukua dola. Kama ingekuwa ukifikiri unatenda, leo wangekuwa wamechukua dola wale.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania siyo kijiji. Tanzania ni duara, ni nchi kubwa na wanakosea sana kuilinganisha Tanzania na vijiji. Wanakosea sana kuilinganisha Tanzania na mtaa. Hii ni nchi, ina wilaya, mikoa na ardhi kubwa na watu zaidi ya milioni 50, inataka mipango na mipango hii inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, tunaamini kuja mpaka mtukamate hapa tulipo ni kazi ya ziada sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana lakini waendelee kujifunza. Kwa mfano, kwa kumalizia, tumesema hivi toka nchi hii umeundwa kwa mara ya kwanza maamuzi ya ujenzi wa Bwawa la *Stiegler's Gorge* tunataka wananchi watoke kwenye kulipa senti 11 ya umeme tunayolipa leo waje walipe senti 5 au 6. Mtu mwingine anasema hapana, huyu mwananchi unayetaka aendelee ...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Bashe. *(Makof)*

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Heche kaa chini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wetu unamalizika, tunamalizia na Mheshimiwa Bashe.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche kaa chini, Mheshimiwa Bashe naomba uendelee.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisikilize tafadhali.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote, nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu. La pili nitumie kwa dhati kabisa kumshukuru na kumpongeza Waziri wa TAMISEMI na Naibu wake kwa kazi ambazo wamekuwa wakifanya. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mimi nianzie alipoishia Mheshimiwa Mabula. Nadhani umewadia wakati kama Bunge na kama nchi tutazame mfumo wetu wa bajeti na *budget process* kwa sababu kwa uzoefu huu mdogo nilionao ambaao tumeka a humu ndani, kila mwaka tunakuja tunalaumu kutokufikia malengo. Nadhani umewadia wakati

wa ku-reflect na kuangalia, je, mfumo wetu wa kujadili na kupanga bajeti kama nchi unatatua matatizo tunayoyataka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati wa kukaa muda mwingi kuangalia *revenue side* kuliko *expenditure side* yaani tutumie muda mwingi kuangalia ni namna gani Serikali itapata mapato ili yaweze kwenda kutatua changamoto ambazo zinatukabili. Tusipofanya namna hii tutakuja kila siku hapa kuinyooshea kidole Serikali. Sisi wenyewe ndiyo tunapitisha hiyo bajeti ambayo kila mwaka tunaiona kwamba haifkii malengo lakini hatu-*provide solution* katika matatizo ambayo tunakabiliana nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani umewadia wakati wa kuisaidia Serikali sisi kama Bunge na tuangalie kanuni zetu na sheria, je, mfumo wetu wa kujadili bajeti unajibu mahitaji yetu? Hili ni jambo la kwanza ambalo nilitaka niseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka niongelee kidogo kuhusu TAMISEMI. *Responsibility* zilizoko katika Wizara ya TAMISEMI ni kubwa sana. Mahitaji yaliyoko TAMISEMI ni makubwa sana. Mfano pale kwetu Nzega tumejenga Kituo cha Afya cha Zogoro, Serikali ilitupatia fedha kama *500 million shillings*, tumejenga nyumba za watumishi tano, tumejenga *instruction zilizoletwa theatre, OPD*, wodi ya akina mama, *theatre* ya akina mama kujifungulia na nyumba za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayotukabili leo ni vifaatiba. Wakati tuna majengo yaliyokamilika, vifaa tba hatuna. Naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri alifika pale akaiona, Naibu waziri alifika akaiona washughulikie suala hili. Mimi niwapongeze sana kwa maamuzi ya kutumia *force account* katika kujenga miundombinu katika kata zetu za vijiji vyetu, imeleta matokeo mazuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niombe, tufanye *stock taking*, majengo yaliyopo sasa hivi ambayo yameshajengwa na nguvu za wananchi na

mchango wa Serikali yana upungufu kiasi gani ili yaweze kutumika. Nzega tumejenga zahanati katika vijiji 17 ambazo ni nguvu za wananchi na tumefika katika *level* ya kuezeka. Tumetumia fedha zetu za ndani 700 *million shillings* kwa ajili ya *ku-support infrastructure* hizi lakini bado hazijakamilika. Naiomba TAMISEMI *i-deploy team* katika kila Halmashauri iende ikafanye tathmini ya miundombinu iliyopo ambayo hajjakamilika tuweze kuikamilisha halafu tuanze *phase two*. Tunajua kwamba hatuwezi kuwa tumemaliza changamoto zote lakini angalau tuwe tuna kazi ambazo zimekamilika asilimia 100. Hili ni muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nataka niongelee suala la *TARURA*. Umewadiwa wakati Wizara ya Fedha na Wizara ya TAMISEMI kukaa chini kutafuta chanzo sahihi, kwa sababu tusipokuwa na chanzo sahihi ambacho kiko *dedicated* kwa sheria ambacho kinaelekea kusalidla *TARURA* bado *TARURA* itabaki inapata *ratio* ya asilimia 30 wakati ina mzigو wa asilimia 70 mpaka 80 ya matatizo ya miundombinu. *TARURA* anachokipata ni kile ambacho kinakuwa *shared* na *TANROADS*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, umefika wakati wa *ku-evaluate*, *TARURA* inafanya kazi kubwa sana na ni muhimu upande wa *Central Government* wakaelewa, wakulima wako vijijini, wanapovuna mazao yao wanahitaji kuyatoa vijijini kuyaleta kwenye barabara za *TANROADS* kwenda sokoni. Kwa hiyo, kama kutakuwa hakuna miundombinu sahihi ya kutoa mazao vijijini, mazao haya yatabaki shambani, yatakosa soko na tathmini zipo, *post-harvest loss* ni kubwa sana katika nchi yetu na mengine ni kwa sababu tu ya miundombinu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeshauri wataalam wakae, tutafute vyanzo vya mapato. Tunaona chanzo cha mapato cha Sh.50 cha maji kinavyosaidia suala la maji, ni *reliable source* inaenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maji kutatua changamoto za maji. Umewadia wakati wa kutazama *reliable source* ya *TARURA* ambayo

itakuwa kisheria na *ring fenced*, itakayoenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Barabara wa TARURA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niombe Serikali, Mheshimiwa Waziri, Nzega tulitengeneza mradi na tukaamua kuanza kuutekeleza kwa fedha zetu za ndani kabla ya kupata *support* ya kutoka *Central Government*. Tumeamua kuanzisha a *transport hub* katika Mji wa Nzega na tumeleta maandishi Serikalini, tume-improve revenue ya stendi ya Mji wa Nzega na sasa hivi tumeanza kuitumia *temporary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshapeleka maandiko Wizara ya Fedha na wataalam wa Wizara ya Fedha wamekuja hadi Halmashauri ya Mji wa Nzega, wametembelea na wameangalia *viability* ya mradi, tunaomba hizi fedha. Tuko tayari kusaini makubaliano na Wizara ya Fedha ili turudishe hizi fedha ziwe *revolving funds* kwa sababu tuna uwezo. Mapato tutakayoyapata *we can pay back* kama *loan* kutoka sehemu nyngine na hii itatuondolea matatizo katika Halmashauri yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumzia hili kwa nguvu? Ni kwa sababu *am not a believer* wa kufukuzana na mama ntilie, bodaboda na watu wadogo wadogo kwa ajili ya kukusanya mapato katika Halmashauri. Sasa hivi *Central Government* inachukua mapato ya *Local Government* na mimi ningewashauri chukueni na *service levy* ije tu *Central Government* kwa sababu kuna *confusion* katika *Local Government*. *Service Levy* iko kwenye sheria kabisa, anayetakiwa kutathmini na kujua *turnover* ni *TRA*, ile *figure* inapelekwa Halmashauri, Halmashauri aka-compute 0.03% lakini mfanyakia shara akifika kwenye Halmashauri anakutana na kigingi. Watu wa Halmashauri wanamwambia hii tathmini hapana na sisi tuna makadirio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumeanzishwa mtindo wa *clustering*, *it is against the law*. Kama tunaona *Local Government control mechanism* ya *service levy* Mheshimiwa Jafo wakabizini *TRA* kwa sababu sasa hivi hela

zote zinaenda *Central Government*, wakabizini tu ili tupeleke kwenye *Revenue Authority* kila kitu, hii ni *opinion* yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niombe Serikali, Halmashauri ya Mji wa Nzega tumejenga shule ya wasichana, imekamilika. Tuna changamoto moja, tunaomba uongee na Wizara ya Nishati watupelekee umeme, iko porini wananchi walitoa eneo na wewe unaifahamu na Serikali naishukuru kwa *support* iliyotupa. Tunaomba ili shule hii ya watoto wa kike ya *boarding school* ya Mwanzoli mtusaidie umeme ufika ili watoto wetu wa kike waweze kwenda kusoma pale. (*Makofî*)

Jambo lingine ambalo nataka niiombe Serikali, tumejenga maabara, sisi tumekamilisha tumefikisha juu, tunaomba *support* kutoka *Central Government*. Tuna maabara 18, tunaomba mtusaidie kumalizia nyumba za walimu 10 katika Mji wa Nzega ili tuweze kutatua changamoto zinazotukabili katika *Local Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja, ahsanteni sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zetu kwa mchana huu zimeishia hapo. Kabla sijasitisha shughuli za Bunge naomba niwataje wachangiaji ambaowataanza kuchangia kwa jioni ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, tutaeendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Omary Kigua.

Baada ya kutaja majina hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi sa 11.00 Jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Namwita Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na baadaye Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ajiandae.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii. Kuna msemo unasema *Conversation rules the Nation*. Ni two ways game; ukipenda kusikilizwa, basi lazima ujue na kusikiliza pia. Leo nitajikita kwenye maeneo mawili, kupongeza na kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza CAG, Profesa Assad kwa uzalendo mkubwa aliuonesha, kwa sababu katika nchi hii watu walianza kutokwa na imani na wasomi wakiwemo maprofesa wetu, lakini kwa hatua alizochukua Prof. Assad recently kwa kweli amerudisha imani kwa wananchi kwamba kunao bado maprofesa ambao wana mapenzi na Taifa hili na wana misimamo yanapokuja masuala ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda nimpongeze Rais kwa kukubali mwaliko wa wafanyakazi Mei Mosi, kuja Mbeya kuwa mgeni rasmi. Pamoja na kwamba anakuja kwenye shughuli ya Kitaifa ya Mei Mosi, Iakini Mbeya wanamsubiri sana kwa sababu ni sehemu ambazo alikuwa hajakanyaga kabisa toka awe Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaase wanaoshughulika na ile *protocol* ya Mheshimiwa Rais wajaribu kuwazuia Chama cha Mapinduzi wasitake au kujaribu kutumia ujio wa Mheshimiwa Rais ambayo ni ziara ya kiserikali kwa maslahi ya chama chao kwa sababu wanaweza wakavuruga ziara ya Mheshimiwa Rais kwa sababu Mbeya ni *Cosmopolitan* kisiasa, imechanganyika sana. Kuna vyama vyote vinatamalaki pale na viko vyama ambavyo vinazidi idadi ya wanachama wa Chama cha Mapinduzi, hususan Jijini Mbeya.

MHE. GOOLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, kuhusu utaratibu.

MHE. GOOLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Menyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 kuhusu utaratibu, nikisoma Kanuni ya 64(1) (c) nikisoma pamoja na Kanuni ya 53(8), kuwa Mheshimiwa Mbunge hatazungumzia suala ambalo tayari Bunge lilishafanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tangu asubuhi alianza Mheshimiwa Ally Saleh kuongelea suala la *CAG*, akaja Mbunge mwingine akaongelea tena suala la *CAG* na sasa hivi Mheshimiwa Sugu. Sisi suala la huyu mtu tayari tulishaliongea kama Bunge na tulishafanya maazimio, lakini bado tu wamekuwa wakijaribu kulifukua kitu ambacho ni kinyume na kanuni zetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa umeelewaka. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kanuni aliyatumia siyo. Kanuni ya Utaratibu ni ya 64. Pili, imekuwa ni mazoea Mheshimiwa Mlinga ku-*interrupt* wasemaji wa Kambi hii kila wanapozungumza na kwa vitu vya ovyo kabisa, kupoteza muda tu. Sasa ningependa kujua, huu ndiyo utaratibu? Au Kambi hii ya Chama cha Mapinduzi imemu-*assign* ye ye ku-*interrupt* wazungumzaji wa Kambi hii kila wakati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Twende tu kwa utaratibu, kwa heshima na Bunge litatuelewa. Yote yanaweza kuwa ni mambo mema, tunataka kupata mfumo mzuri wa kujadiliana

hana ndani, lakini maneno pia anayoyatumia *Chief Whip* mwenzangu katika kueleza, umesikia sitaki kurudia lile neno alilolitamka hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria pia tutumie lugha nyepesi, ambazo ni za kibunge, zitatusaidia tu kufuata kanuni na utaratibu utaenda vizuri. Tupunguze kutumia lugha ambazo siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria lugha ya *Chief Whip* mwenzangu, hebu apunguze kidogo na ikiwezekana tuiondoe, sitaki kuirudia.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane. Mheshimiwa Mlinga alirekebisha kanuni; alianza 68 lakini baadaye akarudia 64(1); kwa hiyo, alikwenda kwenye utaratibu, lakini jambo ambalo linazungumzwa, *Chief Whips* wote wawili mko sahihi, tunatakiwa twende kwa mujibu wa utaratibu. Lugha pia tuwe nazo nzuri.

Kuhusu suala la CAG lililozungumzwa, ikiwa mtu anajadili taarifa; na ikiwa mtu anajadili jambo ambalo limeshazungumzwa Bungeni, ni jambo lingine.

Kwa hiyo, twende kwenye utaratibu. Kama tunazungumzia taarifa, tuzungumzie taarifa, lakini tusizungumzie masuala ambayo yamepita Bungeni. Kwa hiyo, tuendelee na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mbilinyi naomba uendelee.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *almost* naanza hapa, kwa sababu niliongea kwa sekunde 20, kwa hiyo, kwa kuwa nina dakika 10 na *nil-keep my watch*, nina dakika tisa kama na sekunde kama 40 hivi, ukiondoa tano hizi ambazo nimeongea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa *statement* ya ukaribisho kwa Mheshimiwa Rais Jijini Mbeya na hali ya siasa, niendelee kumpongeza na niseme kwamba leo

nimesema nitapongeza na kushauri. Masikio ya wafanyakazi na familia zao yote yatakuwa Mbeya Mei Mosi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wafanyakazi wa Mbeya ambao mimi ni Mbunge wao na Wafanyakazi wa nchi nzima, naomba sasa *with respect*, nimshauri Mheshimiwa Rais atakapokuwa Mbeya mwaka huu Mei Mosi, atangaze ongezeko la mshahara kwa wafanyakazi. Kwa sababu toka ameingia madarakani huu ni mwaka wa tatu mishahara haijaongezeka hata ndururu na wafanyakazi wana hali mbaya sana katika maeneo yote ya nchi hii na ngazi zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia aangalie suala la wastaaifu. Wako wengi sana wamestaifu, wengine mwaka wa pili sasa lakini hawajalipwa mafao yao katika Idara mbalimbali wakilwemo wastaaifu kwenye Idara za ulinzi na usalama kama Magereza, Polisi, wamestaifu miaka miwili sasa na hili nilishalisema bado wako kwenye *Police Quarter* hawaondoki, hawana hata nauhi za kubebia mizigo kurudi hata makwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama suala la mishahara haliko kwenye bajeti, Waheshimiwa Mawaziri, naomba safari hii mrudi mezani mwangalie namna gani mtafanya ili basi Mheshimiwa Rais atakapokuja Mbeya atangaze ongezeko la mishahara kwa wafanyakazi wetu nao wapate unafuu wa maisha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais kuwa Watanzania sio wajinga. Aliongea wakati anamwapisha Mheshimiwa Balozi aliyekuwa anakwenda Cuba. Ni kweli kabisa Watanzania siyo wajinga; na ukitaka kupima, angalia jinsi walivyolipokea suala la CAG baada ya CAG kufanya *Press Conference* jana Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ujinga aliousema Mheshimiwa Rais kwamba Watanzania sio wajinga, aka-*cite* suala la MO Dewji kutekwa na maelezo yake ya nini kilitokea,

Polisi, uchunguzi ulikwendaje, hewa; hivyo hivyo Watanzania wanajiuliza kuhusu Mheshimiwa Tundu Lissu, wanajiuliza kuhusu Ben Saanane, wanajiuliza kuhusu Azori na watu wengine wote waliopotea. Kwa hiyo, naungana mkono kabisa na Mheshimiwa Rais kwamba Watanzania sio wajinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na ahadi ya Mheshimiwa Rais aliposema kwamba baada ya kumaliza miaka kumi iwapo atashinda mwakani hataongeza hata saa moja lkulu. Hili namunga mkono na asiwasikilize wapotoshaji wanaoleta njaa kwenye masuala ya uongozi wa nchi kwa kumperemba na kutaka kumwingiza chaka kwa sababu Afrika hiyo imeshapita na mifano ipo, nitaisema mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itapendeza zaidi kama akiahidi kwamba atakuwa tayari kukabidhi madaraka kwa amani mwakani iwapo atashindwa kwenye uchaguzi wa 2020 mwakani. Atoe kauli na siyo tu aahidi kwa maneno, aahidi kwa vitendo kwa kutusaidia kuifumulia mbali Tume ya Uchaguzi kwa sababu Tume ya Uchaguzi iliyokuwepo haikidhi, imejaa makada wa wazi kabisa wa Chama cha Mapinduzi, chama tawala watu wanaovaa *uniform* za chama kesho wanaenda kusimamia uchaguzi. Uchaguzi huo utavurugika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila Tume Huru, tutaingiza nchi hii kwenye machafuko ya kiuchaguzi kama ilivyotokea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Kenya mwaka 2017. *Take my word, wakati tunaanza hili Bunge nilisema humu ndani kwenye briefing, I was worried about the future; I was scared of the future, mkacheka cheka hapa lakini leo everybody sees future imetukaliaje.* Sasa tunayo nafasi ya kujirekebisha kuokoa mambo mabaya yanayokwenda kutokea yasitokee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi wa mwaka 2020 itakuwa siyo mchezo, kwa sababu wananchi wanakwenda kuchagua kati ya taabu na nafuu. Sasa watu wanaochagua

kati ya taabu na nafuu, huwezi kuwaletea mchezo. Maisha yamekuwa magumu; wafanyabiashara hoi, wafanyakazi hoi. Huu ni mwaka wa tatu sasa *President Dr. Magufuli* yuko lkulu lakini bado analalamika na kutumbua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimemwangalia kwenye *tv* akiwa Namtumbo, bado mpaka leo hii nchi hii Rais anakwenda *ku-question* ujenzi wa shilingi milioni 60 wa zahanati sijui jengo gani kule wakati ameweka timu, ameweka Wakuu wa Wilaya; wote kazi yao ni kumvizia Sugu wamkamate wamweke ndani masaa 48, halafu wanashindwa kusimamia kazi ambazo Mheshimiwa Rais amewachagua wao kufanya hizo kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu ni mwaka wa tatu Mheshimiwa Rais analalamika, bado anatumbua, timu hajakaa sawa na sasa tunaenda dakika ya 85 kuelekea dakika ya 90. Msaidieni sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nishauri tubadili *approach*. Masuala ya ukali hayasaidii, turudi sasa kwenye lile suala kama aliloongea Mheshimiwa Jafari...

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHES. JOSEPH O. MBILINYI: ...Meya Mstaifu wa Arusha aliposema kwamba...

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Tunahitaji kujenga taasisi imara

Mhe. MARWA R. CHACHA: Kaa chini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, taarifa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: ...na siyo kujenga mtu imara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, Mheshimiwa Mbilinyi subiri kidogo, taarifa. Mheshimiwa Chacha.

TAARIFA

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa, mwongeaji anasema Tume ya Uchaguzi siyo huru. Liliundwa Bunge la Katiba liliokuwa linaunda Tume, wakaunda chombo kinaitwa UKAWA wakaondoka Bungeni. Leo wanataka Tume huru, ipi? (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, yule nampuuza. Ila acha niseme neno moja, kwa nini Bunge linafika hapa? Angalia hoja muhimu zinazoletwa humu Bungeni, halafu angalia Wabunge wa sasa upande wa CCM wanaochangia. Huwezi kuona Mheshimiwa Chenge kasimama au Mheshimiwa Mwinyi au hata Mheshimiwa Jenista mwenyewe hawezi kusimama kuchangia vitu vya msingi. *Wanawaachia mapoyoyo kama yule wavuruge Bunge tu kwa style ya namna hii.* (*Makofi/Kicheko*)**[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi umeyatafuta haya. Mheshimiwa Jenista.

Mheshimiwa Mbilinyi subiri, Mheshimiwa Jenista.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1) (f) na (g), inakataza kabisa kutumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine na hairuhusu kutumia lugha zinazofanana na lugha ya matusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zinatutaka humu ndani *unapom-address* Mbunge mwenzako, utatumia jina lake kwa kumwita Mheshimiwa. Mheshimiwa Mbilinyi anamwita Mbunge mwenzake poyoyo. (*Kicheko/Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista, malizia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hii siyo lugha ya Kibunge. Katika tafsiri ya lugha za Kibunge tulizonazo, hii siyo lugha ya Kibunge. Ni lugha ya kudhalilisha na kuudhi. Tunaomba lugha hiyo aifute na aiondoe kwenye *Hansard* ya leo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, hilo neno hata mimi maana yake sijui, naomba ulifute tu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uzingatie dakika zangu, bado saba hata kengele ya kwanza haijapiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kwenye shida kidogo. Angalia ma-RC na ma-DC...

MWENYEKITI: Naomba ufute lile neno.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshafuta. Poyoyo! Nimeshafuta, nitalitumia nje. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia *state* tuliyokuwepo ma-RC, ma-DC ni vituko kabisa. Angalia yule RC wa Tabora, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Namheshimu sana *my brother*; anakaa anasema, ye ye atamwomba Mungu, Mungu amshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri. Kweli! *That is blasphemy*. Hiyo ni *blasphemy* inaitwa, maana yake kwa Kiswahili ni kufuru. katika baadhi ya maeneo ambayo wako *serious* na Mungu, Mheshimiwa Aggrey Mwanry sasa hivi angekuwa mahali pabaya sana kwa kufanya *blasphemy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu ni Mkristo, tunamwona Kanisani kila siku, nashangaa hata Mheshimiwa Msigwa, mwandishi wake wa habari hajalaani kitendo kile. Tunaliingiza hili Taifa kwenye laana, namwomba Mungu alihurumie hili Taifa kwa kauli za watu kama akina Mheshimiwa Aggrey Mwanri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mko *busy* sana kuzuia maandamano. Maandamano ni haki ya Kikatiba watu *ku-express*, yatawasaidia ninyi wenye kujua joto likoje. Hamwezi kuzuia maandamano kwa kutumia Polisi. Yakifika hayazuiliki. Omar Al-Bashir saa hizi siyo Rais. Jana amelala Rais, leo siyo Rais. Amezuia shughuli za vyama vyा siasa, amezuia maandamano, amefuta vyama vyा siasa kwa miaka 30 akiwa lkulu ya Khartoum, Sudan. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakinii bei ya mkate tu, mwaka 2018 mwishoni kapandisha bei ya mkate tu, watu wameingia barabarani, vyama vyा siasa hakuna, haoni mtu wa *ku-negotiate* naye, ameishia *ku-negotiate* na Jeshi, Jeshi limemwambia kaa *barracks*, hatuwezi kupiga risasi watu, imetosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtafanya mbinu kuzuia maanadamano, mtafanya nini; yatakapofika mama! Kumbuka Algeria. Yule jamaa, yule mzee na ni wapambe tu. Mzee wa watu, Bouteflika, ana miaka 82, amechoka yuko kwenye *wheel chair*, wapambe wanalazimisha aongeze muda, agombee ili wao wabaki kwenye nafasi, kama

wanavyofanya baadhi ya watu hapa sasa hivi kuanza kumwambia *President Dr. Magufuli*, eti aongeze muda sijui aongeze miaka saba kwa maslahi yao binafsi. Hiyo Afrika imepita, tutapata taabu sana. Namwomba sana Mheshimiwa Rais asisikilize huo upuuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, baadaye Mheshimiwa Omar Kigua ajiandae.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo hotuba hizi mbili ambazo ziko mbele yetu. Sababu ya muda mdogo, naomba moja kwa moja nianze na suala la upungufu mkubwa sana wa watumishi na hasa kwenye Sekta ya Afya na Sekta ya Elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli kati ya kitu sasa hivi ambacho kinadumaza elimu, pamoja na ongezeko kuwa la watoto katika mashule yetu, ni suala la upungufu wa walimu kwenye mashule yetu. Wakati *enrollment* inaongezeka, wakati madarasa yanaongezeka, wakati shule zinaongezeka, walimu hawaongezeki kwa *speed* ile ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ya Kaliua, mwaka huu tumefungua shule nne za sekondari; mwaka huu huu tumefungua zahanati nne, mwaka huu huu tumefungua *primary school/mikondo* sita. Walimu wanahamishwa kutoka kwenye maeneno yenye upungufu, wanapelekwa kwenye shule mpya. Kwa hiyo, kwenye tatizo unaongeza tena tatizo lingine, una-create gap pale, unawapeleka kwenye shule nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka watoto wetu wapate elimu nzuri, ni lazima tuhakikishe kwamba ongezeko la watoto linakwenda sambamba na ongezeko la walimu, ni muhimu sana. (*Makofii*)

Leo shule moja ina madarasa saba inakuwa na walimu tisa, wanagawanaje hayo masomo waweze kufundishwa? Zahanati inakuwa na watumishi watatu au wanne na wakati mwagine katika maeneo mengine mpaka watumishi wawili. Mmoja akiugua, au kama ni mtu na mke wake ameugua, au amesafiri, zahanati haifanyi kazi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, lazima tuwe na mpango mkakati kabisa wa makusudi ya dhati, kuongeza watumishi na hasa kada hizi mbili, elimu na afya, ni muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengine, nilisema tena hapa, wanajifungulia kwenye zahanati, hakuna wahudumu; na mhudumu huyu anachoka. Yeye ni binadamu, anatumia damu, hatumii maji. Tunaomba suala la upungufu ya kada hizi mbili ni muhimu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mwaka 2018 wilaya yetu imepata watumishi 16; ni wachache sana sana kwenye kada ya afya kwa sababu wamekwenda kuongezwa, kwenye zahanati kulikuwa na wawili, akaongezwa mmoja. Kwa hiyo, bado tatizo liko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi bado tunakwenda kuongeza kujenga zahanati, vituo vya afya, tunaongeza shule, tunaongeza madarasa, lakini tatizo la upungufu wa walimu ni kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la walimu wa sayansi. Hivi kwa kweli, sasa hivi sijui ni *percent* ngapi, sijafanya utafiti wa kutosha; lakini shule nyingi, tumejenga maabara na ni agizo la Serikali. Maabara zile hazitumiki, hakuna walimu wa sayansi. Tunakwendaje kwenye uchumi wa viwanda wakati hatuna walimu wa sayansi, hatuna walimu wa *biology*, walimu wa *physics* na *chemistry*? Haiwezekani kwenda kwenye uchumi wa viwanda wakati hatupeleki walimu wa sayansi kwenye mashule yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine mwaka jana, mwaka juzi 2017/2018 Serikali ilipendekeza shule moja katika

kila wilaya kupokea watoto wenye mahitaji maalum kwa maana ya watoto walemavu, wenye mahitaji yote, walemavu wa viungo, viziwi wote wamepokelewa pale. Cha ajabu shule zile miundombinu ile siyo rafiki kwa watoto wale, wamepelekwa pale wanapata mazingira magumu sana, hawapati elimu kama watoto wenzao, hawajapelekewa vifaa vya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano mmoja, sisi Kaliua shule iliyopendekezwa ni *Kaliua Primary School*, ina watoto 2,295, shule moja, wale watoto wanatumia kaofisi kadogo tu kalikokuwa kakatahapo pembeni. Kwa hiyo ni tatizo. Sasa kama lengo lilikuwa ni kuwasaidia, maana yake kilio chetu hapa Bungeni ilikuwa ni kwamba, watoto wale wamesahaulika, wako majumbani, lakini ni Watanzania wanahitaji elimu kama wengine, Serikali ikaamua kuwasaidia kwa kuwa hatuna shule maalum nyingi kwenye mikoa yetu watenge shule moja. Akili yangu ilikuwa ni kwamba, Serikali ingepeleka nguvu kubwa kwenye zile shule, kujenga miundombinu, kuweka Walimu, kuweka vifaa wale watoto wapate elimu ndani ya maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli lengo lilikuwa jema, lakini leo kilichofanyika ni kuwaacha katika mazingira yale, kwa kweli hatuwatendei haki. Naiomba Serikali ihakikishe lengo lake liliokuwa la kuweka zile shule kuzitenga litimie kwa kuweka miundombinu ya kutosha, miundombinu rafiki, watoto wanatambaa chini kwenda kwenye zile mashule, wana-share vyoo na wale watoto wengine na wenyewe ni walemavu, siyo haki kabisa! Wengine walikuwa viziwi, wamekaa pale mpaka mwisho wameondoka hakuna Mwalimu wa kuwasaidia. Tuwatendee watoto hawa haki, hawakupenda kuzaliwa walemavu, ni Watanzania wenzetu, wana haki sawa kama watoto wengine ambao wamezaliwa bila kuwa na upungufu wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *TASAFnakumbuka TASAFthree ambayo tunaenda nayo sasa hivi ya kunusuru kaya maskini ilianza mwaka 2013, maeneo mengine kama Kaliua 2014*. Huu mradi ulikuwa ni miaka

mitano, tulivyokuwa tumeelezwa pamoja na upungufu kwamba kwenye hivyo vijiji ambavyo wamepewa wachache wengi pia hawapati lakini tulitegemea baada ya miaka mitano waingie wapate tena vijiji ambavyo vilikosa. Leo hakuna majibu yoyote tunayopewa na Serikali nimeuliza suala hili tangu Mheshimiwa Kairuki akiwa Waziri, hatupati majibu, ni lini vilevijiji ambavyo havijawahi kuingia kwenye *TASAF* vitaingia kwenye *TASAF*? Imekuwa ni *double standard*, kuna wazee ambao hawajiwezi kabisa, kuna walemovu hawajiwezi, wanaona kijiji jirani kuna msaada wanapata japo ni kidogo, ye ye hapo alipo kijiji hicho hicho jirani hapo pembedi hapati chochote kwa miaka yote, kwa nini Serikali isione kwamba hii ni fursa kwa wote? Kama suala la kusaidia kaya maskini zipo kote, basi baada ya miaka mitano mradi huu ueleweke kwenye vijiji tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa tupate majibu kwa Mheshimiwa Waziri atakavyokuja kujibu kwamba mradi wa *TASAF* ambao ulikuwa umalizike waweze kupeleka na kwenye vijiji ambavyo vilikosa, Kaliua tulipata vijiji 36 tu, tuna vijiji vingine kwa maana ya Jimbo la Kaliua 36 tu, bado vijiji vingine 26 hawajapata. Kwa hiyo tulikuwa tunategemea kwamba wangeweza kupata kama wengine, kwa kweli wanaumia wazee wale wanasikitika kwa sababu wanaona kwamba Serikali imewaona wenzao wa vijiji jirani wao imewasahau na ukizingatia hapa kwamba hakuna mpango wowote wa Serikali kusaidia wazee popote, hata wale ambao wana nguvu ya kufanya kazi, hakuna mfuko maalum wa kuwasaidia. Kwa hiyo tunaomba *TASAF* ihakikishe kwamba imeangalia wale wengine ambao pia hawakuingia kwenye Mfuko huu wa *TASAF* kwa awamu ile ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine na la mwisho ni suala la lishe. Suala hili ni muhimu sana, nilikuwa nasoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri; suala la lishe hapa Tanzania kwa takwimu za mwaka 2016/2017 watoto chini ya miaka mitano wenye udumavu ni watoto asilimia 34, ni wengi kweli kweli. Nilikuwa nategemea tupewe takwimu *update*, tupewe takwimu za 2017/2018, 2018/2019 tujue *current situation*, udumavu kwa sasa hivi ni asilimia ngapi. Hata kwa

takwimu za miaka mitatu iliyopita asilimia 34 kwa watoto chini ya miaka mitano suala la lishe ni muhimu kuliko maelezo, mtoto anapodumaa akiwa chini ya miaka mitano, anadumaa *totallykuanzia* fikra zake, mawazo yake, uelewa wake, darasani hafundishiki, ni tatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukiangalia bajeti iliyotengwa na Serikali bado ni kidogo sana, haiwezekani tunatengeneza Taifa la kesho, hawa ndiyo Marais wajao, ndiyo Mawaziri wajao, ndiyo Wabunge wajao, Wakurugenzi wajao, wanakua wakiwa wanaudumavu wa akili, tunawapeleka wapi. (*Makofî*/)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia niseme kwamba suala la kuangalia suala lishe siyo kutoa matone ya damu, siyo kutoa matone ya vitamini A na dawa za minyoo tu, hapana. Suala la lishe ni chakula pia na bahati mbaya ukiangalia maeneo ambako watoto wamepata utapiamlo na udumavu wa akili kwa maeneo mengi hasa utapiamlo ni mikoa ambayo wanalima vizuri sana, wanafuga vizuri, leo Mkoa wa Kilimanjaro siyo mkoa ambao tunatakiwa tuwe na udumavu wa akili wala kuwa na utapiamlo, lakini ukiangalia utapiamlo upo mwangi, kwa nini hakuna elimu. Pia ukiangalia bajeti nzima ya Mheshimiwa Waziri hakuna sehemu wamesema watawekeza kutoa elimu namna gani wazazi wawape watoto vyakula vyenye kujenga lishe yao, hawaangalii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali suala la kutoa matone ya vitamini A nakubaliana nalo, pamoja na kutoa dawa za minyoo, lakini suala kubwa kabisa ni chakula nyumbani. Ukimpa mtoto dawa ya minyoo kamanyumbani alivyokula vitaminiataendelea kudumaa tu, kwa sababu hiyo haimsaidii sana. Vile vile Mkoa wa Tabora tunalima mahindi, tunalima maharage, tunalima karanga, tunalima alizeti vyakula vyote vyenye vitamini viro, iweje watu wapate utapiamlo au udumavu wa akili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimanjaro wanalima, Kilimanjaro wanafuga watu wanakula mayai, maziwa, lakini

maziwa yanauzwa mtoto hanywi, mayai yanauzwa, mtoto hali, matokeo yake watoto wanadumaa. Tusiliangalie Mheshimiwa Waziri kama suala dogo, ni suala kubwa kwelikweli, ndio maana tunakuja kuwa na Taifa la watu ambao hawafikirii vizuri, hawawazi vizuri, hawawezi ku-deliver kwa sababu udumavu umeanzia kwenye utoto wake.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Omari Kigua na Mheshimiwa Abdallah Chikota ajiandae.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mngu kwa kuweza kusimama leo tena leo jioni hii katika Bunge lako Tukufu niweze kuchangia kwenye hotuba mbili za Waheshimiwa Mawaziri waliopo. Nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza Mawaziri wote wawili, nimpongeze Waziriwa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kaka yangu Jafo, lakini nimpongezee Mheshimiwa Mzee Mkuchika na Manaibu Waziri wote kwa kazi ambayo mnaifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwanza nianze eneo la *TARURA*, watu wamezungumza sana kuhusu *TARURA*. Natambua umuhimu wa *TARURA* na katika Bunge hilihili ndipo tulipopitisha *TARURA*, lakini wapo ambao wanasmama hapa kusema kwamba *TARURA* sasa irudi tena kwa Madiwani. Naomba niseme kwamba *TARURA* ibaki kama ilivyo; pamoja na changamoto nyingi sana kuhusu *TARURA*, lakini ni ukweli usiopingika kwamba *TARURA* ikirudi kwa Waheshimiwa Madiwani kutakuwa kuna vurugu nyingi sana. Ushauri wangu ni nini kuhusu *TARURA*, ni kwamba wanakosa usimamizi wa kutosha, Meneja wa *TARURA* anasimamia barabara za halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani anasimamia ubora wa kazi ya *TARURA*, hatuna chombo ambacho kinasimamia

kazi za *TARURA*, namshauri Mheshimiwa Waziri na timu yake waangalie namna ambavyo *TARURA* wanaweza kusimamiwa. Nalisema hili kuna changamoto nyingi sana pamoa na upungufu wa bajeti, mathalani nizungumzie katika Jimbo langu la Kilindi, ambalo lina idadi ya barabara 139, kilometra 844, pesa ambayo tumetengewa ni shilingi bilioni moja na milioni mia moja sitini na tisa. Kiasi hiki hakitoshi, hebu fikiria barabara 139 unaweza kuzigawa vipi kwa kiasi hiki cha pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wazungumzaji wa mwanzo wamezungumzia kwamba tuongeze bajeti nami niungane nao kwamba tuchukue ile asilimia kumi kwenye *TANROADS* tuiongeze kwenye asilimia 30 iwe asilimia 40. Hii itasaidia kupunguza changamoto za *TARURA*. Nalisema hili kwa sababu Wabunge wanasmama hapa wanalamika na niseme ukweli tu, kiasi hiki ambacho kimetengwa kwa ajili ya Jimbo la Kilindi hakitoshi. Tunamlaumu sana Meneja wa *TARURA*; lakini ukiangalia uhalisia wa pesa zilizotengwa ni ndogo sana. Hali halisi ya Jimbo langu la Kilindi ni mabonde na milima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyewe kusema wamesema kwamba, ni heri uone mara moja kuliko kusikia mara 20. Mheshimiwa Naibu Waziri dada yangu Dkt. Mary Mwanjelwa amefika pale Kilindi, hata Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI* amefika amelona Kilindi ilivyo, nyakati za mvua, magari hayapiti kule, mvua ni nyingi, lakini na barabara pia hazipitiki. Sasa tuone dhamira hii ya Serikali ya kuanzisha *TARURA*, basi iendane sambamba na maeneo husika, huwezi ukampa mtu mwenye barabara 139 na barabara zenyen urefu wa kilometra 844 na mtu mwenye kilometra chache unakuwa hutendi haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali sana kwenye eneo hili watazame, wanao wataalam, wasikae maofisini, tunasmama hapa Waheshimiwa Wabunge kuyazungumza haya, wawe wanawatuma Maafisa wao waje kutembelea na kuona hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo pengine nataka kulizungumzia pia ni eneo la huduma ya afya. Nimpongeze Waziri wa TAMISEMIna timu yakewamefanya kazi kubwa sana. Nitoe mfanmoja tu kwenye Jimbo langu la Kilindi, Mheshimiwa Waziri ameweza kutoa pesa ya vituo vitatu vya afya; hili ni jambo kubwa sana sana. Eneo la Kilindi ni eneo pana, tuna vijiji 102, kata 21 bado vituo vya afya hivi ambavyo tumepeata havitoshelezi; lakini wanasema asiyeshukuru kwa kidogo hata kikubwa hawezi kushukuru. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nizungumzie suala la utawala bora, mzee wangu Mheshimiwa Mzee Mkuchika, nimpongeze sana baaada ya kuchaguliwa katika eneo hilo. Kulikuwa kuna kelele sana sana juu ya ugomvi wa Wenyeviti, Wabunge na Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, lakini naona hali imetulla. Sasa naomba njielekeze kwa mtazamo wangu mimi nini maana ya utawala bora, Serikali hii imejikita kuwaleta maendeleo wananchi, imeamua kujenga vituo vya afya 352, huo ni utawala bora. Unapoamua kujenga mradi kama wa *Stiegler's Gorge* maana yake huo ni utawala bora, *SGR* ni utawala bora kwa sababu ungeweza kuchukua pesa hizo ukapeleka maeneo mengine, lakini Mheshimiwa Rais kwa sababu ana dhamira nzuri ya kuwapenda Watanzania ameamua kuwekeza kwenye miradi na hii lazima tukubaliane nao tu huu ni utawala bora, ni lazima tumsifie na tumpongeze Mheshimiwa Rais katika hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja ana mtazamo wake katika hili; lakini naamini kabisa dhamira ya Serikali hii ya kuwekeza katika miradi mikubwa, dhamira ya Serikali hii ya kupeleka umeme vijijini ni utawala bora, kwa hiyo ni lazima tuipongeze Serikali katika hili na naamini ipo siku Watanzania watakumbuka dhamira ya Mheshimiwa kwamba atakuwa ni Rais anayesimamia utawala bora na sisi kama Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tuko pamoja na yeye. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwenye utawala bora ni suala la eneo la utawala. Mzee wetu Mkuchika ameshawahi kuwa

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Tanga ni mkoa pekee ambao una halmashauri 11, Mkoa wa Tanga una shule za msingi 1028, lakini ipo baadhi ya mikoa ina halmashauri chache sana. Nimemskia Mheshimiwa Rais juzi akisema kwamba hawesi kuongeza maeneo ya utawala, lakini sasa lazima tutazame,kama hatuongezi eneo la utawala, tufanye nini ili kwenda sambamba na maeneo makubwa kama haya? Lazima tuhakikishe kwamba *resources* zile ambazo ni chache tupeleke kwenye maeneo haya ambayo ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu leo tuchukulie mfano, Afisa Elimu wa Mkoa wa Tanga ambaye shule za msingi tu ni 1,022, lakini baadhi ya Mkoa wana shule za msingi 177, unawezaje kufanya tathmini kwa watu hawa wawili, hapo hakuna usawa hata kidogo. Nashauri tuangalie namna ambavyo maeneo ambayo ni mapana kwa utawala tuhakikishe kwamba *resources* inakuwa za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kusema nikuhusu watumishi kukaimu. Hili kwa kweli halijakaa vizuri sana. Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya PAC mara nyingi tumekutana na Wakurugenzi, wanakaimu mwaka mzima, miezi sita, hivi unawezaje kufanya upekuzi kwa miezi sita, nchi hii hii, Tanzania hii hii. Namwomba Mheshimiwa Waziri, najua watu hawa wako chini ya Ofisi yake Mheshimiwa Mzee Mkuchika, hebu tuangalie kamahawana weledi katika hili, tuangalie namna ya kuwapa mafunzo ili suala la kukaimu lisichukue muda mrefu sana. Kuna umuhimu wa mtu kukaimu kwa muda mfupi, unapomkaimisha mtu kwa muda mrefu, kwanza unampotezea *confidence*, uwezo wa kufanya kazi unakuwa haupo kwa sababu hana uhakika na nafasi aliyopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti,nishauri katika dhana ya utawala bora ni pamoja na mtu kutokaimu muda mrefu. Hii nadhani nilikwishazungumza awali kwamba zamani tulikuwa na utaratibu wa *succession plan*, yaani leo Mkurugenzi anastaafu tayari tunajua nani atachukua nafasi yake. Sasa haiwezekani unastaafu leo, miezi sita ijayo ndiyo unaanza

kumtafuta mbadala wake. Ningependa kusema kwamba hebu tuliangalie hili kwa sura nyingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja zote za Waheshimiwa Mawaziri wawili. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Omary Kigua. Tunaendelea na Mheshimiwa Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Dunstan Kitandula, ajiandae.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni Wizara mbili, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwanza nipende kuchukua nafasi hili kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hizi mbili, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika hongereni sana. Pili, nichukue nafsi kuwapongeza Manaibu wa Wazara hiyo, Ofisi ya TAMISEMI kuna Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Kandege, lakini Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuna dada yetu Dkt. Mwanjelwa, hongereni sana kwa kazi mnazozifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanza kupongeza kwa kazi nzuri ambazo TAMISEMI wamefanya na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambazo ziko wazi kwa sababu si vyema kuanza kulaumu bila kupongeza, mnyonge mnyongeeni lakini haki yake mpeni. Kuna ujenzi mkubwa wa vituo vya afya 352 ambavyo vimesimamiwa vizuri na vingi vimeshakamiliaka na Mheshimiwa Rais wiki iliyopita alifanya uzinduzi Mkoani Mtwara katika kituo cha afya, Mbonde, Wilayani Masasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ujenzi wa hospitali za Wilaya 67 ikiwemo na ya Jimbo langu la Nanyamba na kwenye vituo vya afya 352 Mheshimiwa Jafo na TAMISEMI nawapongeza sana kwa sababu katika Jimbo langu tulikuwa hatuna kituo hata kimoja lakini wametuona

na tumepewa vituo vitatu na vimeshakamilika na vimeshaanza kutoa huduma, kilichobaki sasa tunasubiri mashine na vifaa vingine ili huduma ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu kuna fedha zaidi bilioni 29 zimetolewa kwa ajili ya kukamilisha maboma. Kila siku tulikuwa tunaimba hapa kwamba kuna nguvu za wananchi zimetumika, lakini Serikali haijaunga mkono. Kwa hiyo naipongeza sana TAMISEMlkwa kuliona hili nakupeleka bilioni 29 na kunusuru hayo maboma 2,392 ambayo fedha hizo zimeenda katika Mikoa yote Tanzania Bara. Si hivyo tu kuna kimiradi ya *TASA*Fna MKURABITA tumeona jinsi inavyotekelawa katika maeneo yetu. Kwa hiyo nawapa hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa rai na ushauri kwa Wizara hizi nataka niweke *record* vizuri kuhusu mambo mawili ambayo wachangiaji waliopita wamezungumzia. Kwanza kuna mzungumzaji jana alisema maamuzi mabaya ya Serikali imepelekea Mheshimiwa Rais kusema kwamba *kangomba* hawana makosa. Mheshimiwa Rais kwenye ziara yake ya Mtwara hakusema hivyo, alichosema Mheshimiwa Rais ni kutoa msamaha kwa *kangomba* na hakusema kwamba *kangomba* siyo makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Sheria ilioanzisha Bodi ya Korosho, Sura 203, kifungu cha 4(1), kinatoa majukumu ya Bodi ya Korosho, jukumu la kwanza ni kuhakikisha linasimamia suala la soko la korosho, lakini la pili kutoa leseni kwa mnunuzi na muuzaji wa korosho, *kangomba* hana leseni. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais hakusema hivyo, Mheshimiwa Rais ametoa msamaha na hiyo ni sifa ya viongozi ambao wanasiliza watu wao, hongera sana Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tusimwekee maneno Mheshimiwa Rais wetu, hakusema hivyo Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka tuweke rekodi sawa, kaka yangu hapa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha CUFTAifa, Mheshimiwa Maftaha amesema Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kazi yake ni kuwanyima wapinzani

nafasi kwenye mikutano. Hiyo siyo sahihi, Mkuu wetu wa Mtwara anajua majukumu yake, ni mtu ambaye anaafuata taratibu lakini sisi Wabunge kama viongozi tufahamu itifaki ya ugeni wa Rais. Siku ya ugeni wa Rais kuna itifaki zake na mgeni pale ni mmoja tu Mheshimiwa Rais. Tulikuwa na Mawaziri wengi hawakupewa nafasi ya kuongea.

T A A R I F A

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Tulikuwa na Wabunge wengi walipewa nafasi ya kuongea.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftah taafifa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Chikota namheshimu sana kwa yale ambayo anayozungumza kwa sababu alivyokuja Mheshimiwa Rais siku ya tarehe 2 tulipewa ratiba siku moja kabla ya ziara yake katika Jimbo langu la Mtwara Mjini ilikuwa ni pale Uwanja wa Ndege (*Airport*) na pale Naliendele na ratiba imepangwa, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini ambaye ndiyo mimi ninayezungumza sikuwepo kwenye ratiba hiyo. Sasa asijaribu kupotosha Bunge, kile nilichokizungumza ni kitu sahihi kabisa kwamba Mkuu wa Mkoa anakiuka taratibu za utawala bora.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdallah Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa hiyo, nilikuwa naendelea kusema kwamba siku ya pili, siku ya uzinduzi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara - Newala - Masasi kilometra 50, Mheshimiwa Rais alimuita Mbunge wa Jimbo husika na Mheshimiwa Maftah hakuwepo na ndiyo maana

Mheshimiwa Rais akasema Mbunge wa Viti Maalum, akampa nafasi Mheshimiwa Wambura. Kwa hiyo, angekuwepo siku ile angepewa nafasi ya kuongea.

TAARIFA

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Taarifa.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na mchango wangu.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na mchango wangu na kuweka *record* sawa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Bwege, taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anayeongea sasa hivi asipotoshe. Mimi nilikuwepo katika msafara na Mheshimiwa Maftaha ni Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini na Mkutano wa kwanza ulifanyika Mtwara Mjini, Mheshimiwa Maftaha hakupewa nafasi lakini tulipofika pale...

MWENYEKITI: Sasa unachangia au taarifa? Si umeshasema taarifa tayari?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Tulipofika katika Kiwanda cha Korosho akaitwa Mheshimiwa Hawa Ghasia akapewa nafasi akahutubia. Kwa hiyo, kuna ubaguzi mkubwa katika jambo hili, kwa taarifa yako. Mlipotambua Mheshimiwa Maftaha hakuwepo siku ya pili ndio mkamuita, kwa hiyo, ubaguzi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sipoeki taarifa hiyo, Mheshimiwa mzungumzaji aliyejita sasa hivi hakuwepo siku ya pili alikimbilia Chuo cha Ualimu Kitangali kwa ajili ya ufunguzi wa Chuo cha Ualimu Kitangali, kwa hiyo, hajui kilichotokea pale Naliendele asilipotoshe Bunge.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwege, naomba unyamaze tu, endelea.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na mchango wangu na sasa nataka nitoe rai kwenye mambo matatu kuhusu Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Suala la kwanza ni kuhusu fedha za mchango wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Wale mavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha kwa sababu sasa hivi Wizara inaandaa Kanuni, naomba tuzingatie ushauri ambao tumepokea katika maeneo mbalimbali. Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya LAAC tumepita maeneo mbalimbali, ushauri unaotolewa tusizingatie kutoa fedha hizi kwenye vikundi tu, tufikirie wazo la kutoa fedha hizi za mkopo kwa mtu mmoja mmoja, mlema vu mmoja, kijana ambaye ana mradi wake ambao unawezekana kupewa mkopo akiwa peke yake apewe na mwana mama ambaye ana mradi wake ambao ni *viable* kupewa mkopo siyo lazima awe kwenye vikundi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaweza kwenda mbali tukajifunze Mkoa wa Shinyanga hasa Wilaya ya Kahama, wameamua kutenga eneo maalum kwa ajili ya vijana. Tunaweza kuchukua mfano ule tukapeleka kwenye mikoa mingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili ni kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao unakuja. Naomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia uchaguzi huu. Tuna uzoefu kwenye

chaguzi zilizopita zinatengwa fedha ndogo na kuwaambia Halmashauri wachangie kiasi kinachobaki. Halmashauri zetu uwezo wake tunaufahamu, kwa hiyo, tusiwape mzigo, tutenge fedha za kutosha ili uchaguzi huu uende kama ulivyopangwa, tukamilishe bila ya kuwa na dosari zozote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu ni kuhusu *TARURA*. Kama walivyosema Wajumbe waliopita; *TARURA* kwa kipindi kifupi imeonyesha mafanikio makubwa sana, imefanya kazi nzuri sana lakini ina changamoto mbili. Changamoto ya kwanza bado fedha wanazopewa ni chache lakini changamoto ya pili ni watumishi. Walipewa watumishi wachache kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutengeneza pengo la uhaba wa Wahandisi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, nashauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma watoe kibali maalum ili *TARURA* waweze kupata wafanyakazi wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwagine ni kuhusu Ofisi ya Rais, TAMISEMI; kuna changamoto ya Wakuu wa Idara wengi kuwa makaimu na hii naomba mshirikiane na kaka yangu Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa sababu malalamiko mengi ambayo wanatoa Wakurugenzi kwamba suala la upekuzi kwa wale watarajiwa linachukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, hili suala la upekuzi kama walivyosema Wajumbe wengine tuliwekee mkakati ili upekuzi ufanyike kwa muda mfupi na wale wenye sifa waweze kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chikota. Tunaendelea na Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Mollel ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema ambaye ametuwezesha kuiona siku hii ya leo. Pili, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zote zenye hoja hii na kwa bahati nzuri sana wote wamefika Mkinga, wanaifahamu Mkinga, wanajua changamoto za Mkinga, nawapongeza kwa jitihada mnazozifanya za kutusaidia watu wa Mkinga tuweze kupiga hatua, ahsanteni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali kwa jitihada ambazo imefanya kuhakikisha kwamba sekta ya afya katika Wilaya yetu inapiga hatua. Mwaka jana tulipata fedha za vituo viwili vya afya takribani Sh.1,100,000,000. Vituo vile vimekamilika na nimepata taarifa tumepata vifaa vya takribani shillingi millioni 300, kwa hiyo, vituo vile vitaanza kufanyakazi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia bajeti ya mwaka huu unaokuja nimeona kilio chetu kimesikilizwa. Moja ya kilio ambacho nimekuwa nakipigia kelele sana kila mwaka ilikuwa ni ujenzi wa hospitali ya wilaya. Waziri alipokuwa akiniahidi nilikuwa naona kama vile ananidanganya lakini leo nimeona tumetengewa milioni 500 tuanze ujenzi wa hospitali ya wilaya, nashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mmeweka *benchmark* kwenye ujenzi wa hospitali za wilaya, tumezoea tukisikia Sh.1,500,000,000 sasa sisi mmetuanzia na Sh.500,000,000 tunajua hizo billioni zinifuata. Kwa hiyo, tunaomba muemnde kuweka nguvu ili tuweze kupata fedha hizi. Jambo hili litawasaidia sana watu wa Mkinga lakini litatusaidia vilevile kwenye hospitali yetu ya Mkoa ya Bombo ambayo imekuwa na msongamano mkubwa wa kupata wagonjwa kutoka Mkinga, jambo hili sasa linakwenda kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikipitia hotuba ya Waziri ukurasa wa 32 mpaka 34 nimefarjika kwa sababu

mwaka jana kwenye eneo la lishe nilishangaa kwamba hakukuwa na neno lolote kuhusu lishe. Waziri akaniambia ilikuwa ni kupitiwa na kweli kwa sababu mwaka huu naona ameweka *page* maalum kwa ajili ya lishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Sakaya amezungumzia jambo hili la lishe. Mimi kama Mwenyekiti wa kikundi cha lishe napokuwa na Wajumbe makini namna hii wanaoweza kuzielezea *issue* tunazozijadili kwa umahiri nafarijika sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusikilizane kidogo, kama Taifa tuna tatizo kubwa la lishe. Utafiti wa Hali ya Afya Nchini wa mwaka 2015/2016 unatuambia kwamba watoto wetu chini ya miaka mitano asilimia 30 wana udumavu. Hii maana yake ni kwamba watoto milioni 2,700,000 wamedumaa katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Maana yake watoto hawa hawawezi kufundishika vizuri, makuzi yao ni tatizo na fursa huko mbele ya safari za kuijiondoa kwenye umasikini ni giza. Kwa kuwa na watoto hawa ambao wa udumavu maana yake watazalisha vilevile kizazi chenye udumavu, kwa hiyo, hili ni janga kwa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bunge hapa tulipitisha shilingi billioni 15 kwa ajili ya lishe. Kinachonisikitisha ni kwamba mpaka Desemba, fedha zilizotoka kwa ajili ya jambo hili ni asilimia 40 tu. Takribani Hal mashauri 31 zilikuwa hazijatenga fedha kwa ajili ya jambo hili, hii haikubaliki. Najua kazi kubwa mnayoifanya Wizara lakini hebu tuwabane hawa ambao hawaoni kwamba tuna changamoto na tuna janga kubwa kama hili kwenye Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mikoa ambayo utapiamlo ni zaidi ya asilimia 40. Mikoa hiyo ni Dodoma, Ruvuma, Rukwa, Kigoma, Katavi na Geita. Cha kusikitisha katika Mikoa hiyo ni Dodoma peke yake ndiyo ilikuwa imetenga fedha zile na zimetumika, mikoa mingine utumikaji wa fedha zile ni kwa kiasi kidogo sana. Niwaombe Serikali

muwabane watendaji katika maeneo haya ili waone umuhimu wa kutenga fedha hizi na kutumika ili tuweze kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie elimu. Tunashukuru Serikali kwa kutupatia fedha wka ajili ya ujenzi wa madarasa, mabweni na mabwalo katika shule zetu mbili za Maramba Sekondari na Mkingaleo Sekondari ambazo hivi sasa zinakwenda kuwa za kidato cha tano na cha sita. Mkingaleo tayari imeanza, imani yangu ni kwamba tukikamilisha kutoa fedha za haraka, Maramba Sekondari nayo mwaka huu inaweza kupokea vijana wa kidato cha tano na cha sita. Nawasihi sana tupeleke fedha hizi ili tumalizie ile kazi ndogo iliyobaki pale ili Maramba Sekondari na yenewe iweze kupokea vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya maboma kwenye shule zetu. Tuna maboma karibu 40 ya shule za msingi lakini hatujapata fedha. Tuna upungufu wa walimu ambapo mahitaji yetu ni walimu 883 waliopo ni 481, karibu asilimia 50 upungufu, naomba tulitupie macho jambo hili. Hata kwenye sekondari walimu wa sayansi tuna upungufu karibu walimu 60, walimu 38 kwenye masomo ya baiolojia, fizikia na *chemistry* lakini walimu 22 kwenye somo la hisabati, tunaomba mtuangalie kwa jicho pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maombi mahsus, shule yetu ya Kigongoi wiki mbili zilizopita tumepata balaa, madarasa matatu yameezuliwa na upepo. Tunaomba jitihada za haraka zifanyike ili tuweze kupata fedha za kurejesha madarasa yale kwenye hali yake ya kawaida ili wanafunzi wasipate shida ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumzia Shule yetu ya Lanzoni kwamba shule ile ya sekondari hatuna maji. Watoto wanazimika kwenda kuchota maji mtoni, mto ule umejaa mamba. Hebu tuwaondolee balaa hili ili watoto wale wasije wakajeruhiwa au wakauawa na mamba. Tunahitaji fedha pale karibu shilingi milioni nane ili tuweze

kupeleka maji kwenye shule ile, tusaidieni tuondokane na kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mheshimiwa Waziri unajua kwa muda mrefu nimeduwa nikizungumzia suala la upungufu wa fedha za kiinua mgongo cha Madiwani. Shilingi milioni 11 zisisababishe kilio hiki bila sababu. Mheshimiwa Waziri ukiamua najua ndani ya wiki mbili zijazo hili litakuwa limeondoka, tusaidie kelele zimezidi.

Mheshimiwa Mwenyeiiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana, ahsanteni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kitandula. Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mungu kwa kunijalia kusimama hapa nami niweze kutoa mchango wangu. Kwa kuanza, kwa masikitiko makubwa sana nami naungana na Wabunge wenzangu wote kwa lile suala wanadolilia la vyanzo vyatya mapato vyatya Halmashauri vyote kuchukuliwa na Serikali Kuu, jambo ambalo litapeleka Halmashauri zetu kuendelea kudorora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umekuja mpango huu wa vitambulisho vyatya wajasiriamali, ile ni sehemu moja muhimu ambapo Halmashauri zilikuwa zinajikusanya mapato yake. Yalianza mabango, yakaja majengo na sasa wamemalizia kwenye wafanyabiashara au wajasiriamali wadogo wadogo. Nami naungana na wenzangu kulitaka jambo hili liangaliwe upya kwa sababu Halmashauri zina majukumu makubwa na lazima zijiendeshe kwa kuwa na vyanzo hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mimi leo nashukuru sana, kwanza nilisahau hapo mwanzo nilitaka kusema kwamba nilishukuru Bunge letu kwa kukubali kuipokea ile ripoti ya CAG. Nashukuru sana kwa sababu jambo hili tayari lilikuwa limeleta mjadala mkubwa huko lakini kwa umahiri imepokelewa na nashukuru ina *sign* ya

mwenyewe Profesa Assad, kwa hiyo, ni jambo la kufurahisha.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yaliyopita, iko methali ya Kiswahili inasema: "Funika kombe mwanaharamu apite. Hata hivyo, katika hili la CAG tutafunika kombe lakini mwanaharamu hapiti. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie utawala bora. Hii dhana ya utawala bora ni pana sana na Mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika amepewa Wizara hii kwa umahiri wake, nampongeza sana. Hata hivyo, mambo yanayotendeka ndani ya hchi hii yanakwenda kinyume kabisa na utawala bora. Nataka niseme wazi, Mheshimiwa Waziri umepewaa jukumu la kuhakikisha utawala bora unaendelea ndani ya nchi lakini kuna mambo yanayofanyika hayaendani kabisa na dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupiga marufuku mikutano ya vyama vyaa siasa ni moja kati ya jambo ambalo mnakiuka masharti ya utawala bora. Tanzania imesaini mikataba mbalimbali ya dunia kusimamia haki za raia wake lakini leo sheria, Katiba na vitu vyote vinasema wazi haki ya vyama vyaa siasa ya kufanya mikutano ya hadhara lakini mmezuia. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnajua kuna vyama zaidi ya 20 ndani ya nchi hii na mnajua kuna Wenyeviti wa vyama vingine hawana Mbunge hata mmoja, vyama hivyo vitawezaje kujitangaza kwa wananchi kama mmewazuia wasifanye mikutano ya hadhara? Lengo lenu ni nini? *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Jeshi la Polisi limejipa mamlaka hata vikao vyaa ndani ya vyama vyaa siasa wanazuia, kitu ambacho hakihitaji kibali wala ruhusa ya mtu ye yoyote vyama vyaa siasa kufanya vikao vyaa ndani. Hebu hili liangalieni kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linaumiza watu, tunakwenda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hivi

karibuni tu leo vyama ambavyo vinatikiwa kushiriki katika chaguzi hizo haviruhuswi kufanya siasa ndani ya nchi hii lakini mshindani wetu mkuu Chama cha Mapinduzi mnipa jaramba mtakavyo. Ndugu Humphrey Polepole anafanya mikutano anavyojisikia yeye lakini Makatibu Wenezi na Makatibu Wakuu wa vyama vingine hilo ni haramu, mnatenda dhambi Mungu anawaona, si haki. Zuo hili linahusu *opposition* lakini ninyi kwenu hakuna marufuku yoyote (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe tahadhari yangu, tunapokwenda mbele, ziko lugha zinasemwa na wenzangu wametangulia kusema kwamba kwenye Uchaguzi Mkoo Wapinzani hawatarudi. Sawa, hakuna tatizo. Tusiporudi kwa maamuzi ya wananchi, hiyo hakuna kesi; lakini msitarajie ule upuuzi uliofanyika Korogwe na uliofanyika Majimbo mengine; Msimamizi wa Uchaguzi anachukua fomu anakwenda kujificha halafu anatangaza kwamba Mgombea wa Upinzani katika eneo hili hakurudisha fomu. Huo ni upuuzi, hatutakubali, lazima tutahadharishane mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako huku Waheshimiwa Wabunge wameingia kwa njia hizo, wamejificha na ushahidi uko, kwamba Wagombea wa Upinzani wanarejesha fomu, Wakurugenzi wa Halmashauri wanajificha kukataa kupokea fomu za Wapinzani. Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaotegemea kurudi kwa njia ya mkato ya aina hiyo, wale wanaotegemea mteremko wa aina ile, mwaka 2020 tutapeana tahadhari kabisa. Tanzania ni yetu sote, Vyama vyta Siasa viro kwa mujibu wa sheria na tutasimamia sheria mpaka tone la mwisho la damu yetu. Hatutakubali Mkurugenzi ye yote au msimamizi wa uchaguzi apokee amri haramu kusimamia uharamu wa kuwabatilisha Wagombea wa Upinzani. Hilo never, never never. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea tena kwenye Utawala Bora. Kwenye Magereza wamejaa watu wengi sana.

Wamejaa watu ambao hawastahili kuwepo kwenye Magereza kwa sasa. Kuna watu kesi zao zimechukua zaidi ya miaka sita. Kosa moja tu, upelelezi haujakamilika. Jamani, wale walioko kule ndani ni wazee wetu, ni ndugu zetu, ni watoto zetu. Hatupiganii makosa yao wasamehewe, tunataka kesi zao siendeshwe, ushahidi utolewe, wahukumiwe kwa mujibu wa sheria. Siyo uhodari wa kuwachukua watu mkawalundika ndani halafu mkasema upelelezi haukamilika? Lini upelelezi utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema *especially* kesi ya Mashehe wa Uhamsho wa Zanzibar, hili suala linatukera sana. Wazanzibar wanakerekna na hakuna Mtanzania ye yote aliye radhi kuona kesi ile inaendelea kukaa ukiambiwa tu kwa sababu ushahidi haujakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yuko aliye radhi, mfano kwenye Bunge hili, aseme mimi niko radhi watu wale waendelee kukaa kwa kisingizio tu ushahidi haujakamilika. Leo ni miaka sita wazee wa watu wanasota ndani ya Magereza. Aliye radhi asimamie Mbunge mmoja aseme mimi niko radhi dhuluma ile iendelee. Asimame humu ndani ya Bunge!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina sheria. Kama kesi zinaonekana hazina ushahidi, ziko sheria za kuyaahirisha mashauri ili ushahidi mwaka wowote ukipatikana mashauri yale yarudi tena Mahakamani. Kwa nini hazitumiki hizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananyimwa fursa. Wako wale walioshitakiwa kwa kesi za ubakaji, wakahukumiwa jela wakafungwa. Wamefaidika na fursa ya Mheshimiwa Rais ya kutoa msamaha kwa wafungwa. Leo wazee wale yalaiti wangekuwa wamehukumiwa kwa makosa yao, nina hakika Mheshimiwa Rais hawezikusamehe wabakaji akaacha kuwasamehe Mashehe Wana wa Zuoni. Nina hakika wangehurumiwa na leo wangekuwa huru wakaendelea kulea familia zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Menyekiti, tuna hasira sana na tunajisikia uchungu sana kwa Mashehe wa Uhamsho na Watanzania wengine wowote wanaoendelea kulundikwa Magerezani kwa kisingizio tu cha ushahidi haujakamilika. Ushahidi utapatikana lini? Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, nakuomba sana, wewe ni mzazi, wewe ni mzee, yafikirieni tena haya, Serikali liangalieni, viambieni vyombo vyenu vya upelelezi; suala la Mashehe wa Uamsho wa Zanzibar lifikie mwisho. (*Makofii*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Taarifa.

Hiki kidonda kinachotutonesha, naomba sana suala hili lifikie mwisho.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khatib. Tunaendelea na Mheshimiwa Anatropia Theonest.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Hata Mungu hamjui ninyi! Waachieni Mashehe hao! (*Kicheko*)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa hii kuchangia katika hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI halikadhalika Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa mara nyingine kutoa pole kwa viongozi wangu wa chama hususan Kamanda wa anga, tunamwita Kamanda Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe na dada yetu mpendwa Mheshimiwa Esther Matiko kwa kukaa gerezani kwa dhuluma. Huu ni ushahidi mwingine wa uwepo wa hila. Ni ushahidi mwingine wa kutokuwepo au kwa upungufu ya Utawala Bora, watu wanakaa ndani kwa zaidi ya siku 104 kwa sababu ambazo zilionekana ni nyepesi na Mahakama Kuu ilitoa maamuzi inasema Mahakama ya Hakimu Mkazi ilikiuka kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo tunaanza kuangalia ni kwa kiwango gani katika nchi yetu tunasimamia Utawala Bora? Naendelea kumwambia Mheshimiwa Mbewe tunampenda sana, atabaki kuwa juu, juu, yuko mawinguni. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuna mwanazuoni mmoja anaitwa Twain Mark, aliwahi kusema kwamba uzalendo ni kui-*support* nchi yako, uzalendo ni kuipigania nchi yako kwa kila hali, uzalendo ni kuhakikisha muda wote unaangalia maslahi ya nchi yako na ikiwezekana au ikuridhisha unaweza kui-*support* hata Serikali yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anamaanisha nini? Kwa lugha ya kizungu alisema *patriotism is supporting your country all the time and your government if it deserve it*. Anasema ui-*support* nchi yako wakati wote, ui-*support* nchi yako kwa gharama na damu yoyote, lakini siyo lazima ui-*support* nchi yako kama hai- *deserve* hiyo aina ya *support* inayohitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema haya? Kumekuwepo na malalamiko mengi ya mambo yanavyoenda ndivyo sivyo yanayofanywa na Serikali. Kumekuwepo na malalamiko mengi hasa kutoka kwa Vyama vya Upinzani, kuonekana tunatendewa ndivyo sivyo. Nikiongea haya, kuna watu hawawezi kunielewa kwa sababu wako tayari kui-*support* Serikali yao kwa jasho na damu na siyo nchi yao, kwa sababu wanaangalia kipi wanapata kutoka kwenye Serikali na siyo kwenye nchi husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TWAWEZA walifanya utafiti na moja kati ya matokeo waliyoyapata wakasema, raia wa Tanzania wanasema hawako huru kukosoa kauli za watawala. Kwamba raia wa Tanzania wanaogopa kusema ukweli kuhusu nchi yao inavyoendeshwa hiyo ni hatari sana kwa mustakabali mzima wa uendeshaji bora wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Utawala Bora, kumekuwepo na marufuku mbalimbali, wamesema wenzangu na hasa kuzuia kazi na shughuli za Vyama vyaa Siasa. Nataka kujua, Mheshimiwa Rais kama anaafuata Katiba na Sheria, kama anaafuata utawala bora alipata wapi mamlaka ya kuzuia kazi za kisiasa ambazo zipo kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Mheshimiwa Rais alipata wapi mamlaka; alipata wapi *moral stand* ya kutamka hadharani na kusema watoto wa kike wakipata ujauzito wasiendelee na shule, wakati ni haki yao ya msingi ya kwenda shule *regardless* ya mambo mengine tunayoyasema. Uthubutu wa kutaja maneno ambayo yanakiuka hata Katiba yenye aliyoapa kuilinda anaupata wapi? Hiyo ni swali langu la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tumekuwa tunalalamika vyombo vyaa dola kushiriki mambo yanayoonekana ni ya kisiasa, kuonekana vimeegemea kwenye mlango fulani wa chama. Tuliona kwenye vyombo vyaa habari, mmoja kati ya Polisi Tarime huko akitaja hadharani kidumu Chama cha Mapinduzi na wenzake wakaitikia na hakuchukuliwa hatua zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tumeona kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano lbara ya 74(14) kinachozuia Watendaji wa Tume kuwa wanachama wa Vyama vyaa Siasa, tumeona wiki iliopita, *somebody* Mhagama Katibu wa Mkoa wa CCM anateuliwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Hiyo tunaongelea utawala bora upi katika nchi yetu? Tunathamini utawala bora upi? Tunataka tuwasifu Serikali ya Awamu ya Tano kwa lipi? Kwa nini tuwe ma-patriot wa Serikali kama mnafanya mambo ambayo tunayaona yanaenda kinyume na utawala bora tunaousemea? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tumeona *impurity* ya vyombo vyaa dola, *impurity* ya Polisi. Akwilina alipigwa risasi katika mukutano wa hadhara, yeye akipita

kwenye daladala. Tuambiwe leo, uchunguzi umefikia wapi? Tukaambiwa faili limefungwa, huyo Askari *specific* aliyehusika, alichukuliwa hatua gani? Hiyo ni lazima mtuambie kama tuna-deal na suala linaloitwa utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, kumekuwapo na tuhuma ya vyombo vya dola kuteka, kutesa na wakati mwingine kuua raia wema. Wananchi wamekuwa wakilalamika, watu wamekuwa wakipotea na hatusikii kauli yoyote kutoka Serikalini na hata Wizara inayohusika. Sasa nataka tujue ukweli: Je, ni kweli hao Usalama wa Taifa wanahuksika na hayo matendo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yanatupa maswali kwa kile kilichomkuta Mohamed Dewji. Alitekwa katika filamu ambayo inaonekana haikuchezwa vizuri. Anatekwa katika mazingira yenye *CCTV camera*, anapelekwa kusikojullikana na anapatikana katika mazingira ambayo hayaeleweki. Hiyo inatupa shaka; je, tuko salama kiwango gani? Kama kweli vyombo vya dola vilifanya au havijafanya, mbona ule mchezo ulifanya wepesi na hatupewi majibu? Kwa nini majibu hayapatikani katika suala zima la kutekwa kwa Mohamed? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, nini kilitokea kwa Zacharia? Maana yake ilisemekana amekamata watu, amewapiga risasi, lakini inakuja kujulikana ni vyombo vya dola. Mnatushawishi kuamini hilo kwamba tunaowaamini tumewapa madaraka, wanayatumia vibaya. Kama ndivyo ilivyo, tunaiweka hii Serikali au tunaiweka nchi yetu katika mazingira yanayotia shaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaingia kwenye suala zima la uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Natambua mwaka huu tunaenda kuingia kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa. Haijabiswa kokote kwamba Mheshimiwa Rais alitoa kauli kwamba Wakurugenzi watakaowatangaza Wapinzani kushinda uchaguzi kama wataendelea kulipwa mishahara au kupanda magari ya Umma. Haijapingwa kokote baada

ya kusikia. Kama ndivyo ilivyo, haijapingwa kokote, tunaamini inabaki imesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami natoa wito, Mkurugenzi anayedhani anaweza kupora haki ya mamilioni ya Watanzania watakaokaa kwenye foleni na kupiga kura, mimi namwambia ahakikishe ukoo wake, ndugu zake, jamaa zake hawapo katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni gharama kubwa. Demokrasia ina maumivu makali sana. Watu wanaweka matumaini yao makubwa katika mifumo ya kubadilisha uongozi. Kama kuna mtu mmoja mjinga anaweza kuamua kupora haki kwa maslahi ya tumbo, ninakuhakikishia hapatatosha mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, tumeambiwa kanuni ziko wazi na ninasema kanuni ni lazima ziwe rafiki. Kanuni zisiwepo kwa lengo la kulinda chama kimoja, tumezisoma kanuni na tunaona zinatoa mwanya wa watu wetu kurubuniwa na kununuliwa, zinatoa mwanya wa kubambikiziwa kesi na kama ndivyo ilivyo, mtaelewa nini maana ya nguvu ya Umma. Demokrasia ikishindwa kufanya kazi, mjue kwamba watatrafuta namna nyingine ya kujitetea na kujilinda. Nawatahadharisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kwenye suala lingine dogo kabisa wakati namalizia. Naomba tuambwi, hivyo vitambulisho vya ujasiliamali vilitoka katika mchakato upi? Ni makampuni gani yalishirikishwa na akina nani walipata tenda? Kwa sababu inaonekana kuna kitu kipo nyuma ya pazia hakijulikani. Sisi kama Wabunge watunga sera, hatujui mchakato uliohusika katika kupata Mkandarasi, hivyo vitambulisho vinaendaje? Mpaka sasa kimekusanywa kiasi gani cha fedha kwa vitambulisho vilivyogawiwa? (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia. Tunaendelea na Mheshimiwa Lusinde, baadaye Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Amina Mollel wajandae.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuzawadia tena pumzi yake leo bure ili tuweze kukaa kwenye Bunge lako Tukufu na tuweze kuchangia hoja za Wizara mbili; ile ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na ile ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema juu ya Waheshimiwa Watendaji Wakuu wa Wizara hizi; nami nachukua fursa hii kuwapongea sana ndugu yangu Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri; pamoja na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri; pamoja na Waheshimiwa Manaibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa; pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Waitara na Naibu Waziri mwenzake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri hawa wanafanya kazi kubwa sana. Tunaona namna wanavyopambana na shida za watu wetu, siyo vizuri sana kuwavunja moyo, wakati mwingine tuwapongeze kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mheshimiwa Jafo pamoja na timu yake ya Watendaji wametusaidia sana sisi wa Jimbo la Mtera kutuletea pesa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mpwayungu. Wametupa shilingi milioni 700 pale, wakatupa shilingi bilioni 1,500,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya; vilevile wametusaidia miradi ya maji yenye thamani karibu ya shilingi bilioni mbili hivi na ushee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawashukuru sana ingawa nina ombi maalum kwa ajili ya *ambulance* ya Tarafa ya Mpwayungu, ilipata ajali na ikachakaa kabisa, lakini tunamshukuru Mungu haikuua. Tunaomba tusaidiwe kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Tarafa ya Mvumi, kile Kituo cha Handali ili kwa kushirikiana na Kituo cha Mpwayungu, hospitali ya wilaya iweze kupumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile timu ya ukaguzi wa zahanati, naomba Mheshimiwa Jafo hii aitilie maanani sana. Huko vijijini kuna zahanati nyingine hazina sifa hata za kung'oa meno, lakini wanang'oa meno. Hatujui vile vifaa kama viko katika hali ya ubora. Kuna magonjwa mengi sana ya kuambukiza ambayo ni hatari sana kama zahanati zile hazikugaliwa sawasawa hasa kwenye upande wa tiba ya kinywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno mengi yemezungumzwa, nami bahati nzuri nimepewa kazi ya kupiga *penalty* ya mwisho. Unapopiga *penalty* ya mwisho lazima uwe umetulia.

Ndugu zangu tunapozungumzia habari ya utawala bora kwanza tukubaliane mambo ya msingi. Utawala Bora, vyama vyta siasa vinashindana kwa sera. Kila chama kinapeleke sera kwa wananchi kwenda kuomba kichaguliwe. Uchaguzi Mkuu umepita, chama kilichochaguliwa ni CCM, ndiyo kimechaguliwa kwa wingi. Chama hiki hakichaguliwi kwa rangi zake tu, kinachaguliwa pamoja na ubora wa sera zake. CCM ndiyo inapewa nafasi Serikali itafsiri ilani yake kwa miaka mitano bila kujali kwamba Jimbo hili la CHADEMA wala Jimbo hili la *NSSR*, wala Jimbo hili la chama gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilani inayotekeliza pale ni ilani ya mshindi wa ujumla. Wapinzani wanapewa kazi ya *ku-oppose*, kuleta sera mbadala kama wanazo, lakini wetu hawa kwa sababu hawana, ndiyo maana mnasikia madudu haya. Kama wangekuwa na sera mbadala, wangekuwa wanaeleza kwa hoja. Unasikia hoja, hivi ni Serikali gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namwombea sana Mheshimiwa Rais, Mungu ambariki aendeleee kutumia hekima. Nyie Mawaziri, mwendelee kutumia hekima. Hivi ni Waziri gani anatukanwa, anasemwa vibaya halafu tena anatakiwa apeleke maendeleo kwenye Jimbo la huyo anayemtukana? Hii iko Tanzania tu. Ndiyo maana mnaona tunapata tatizo kwa sababu uchaguzi ukiisha, wale walio shinda ndio

wanakuwa na kazi ya kutafsiri ilani yao ya uchaguzi kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo upinzani wa Tanzania mnaona wanapiga kelele, wanataka kufaidi kwenye kushindwa. Mimi sijawahi kuona. Ninyi mmeshindwa, mnataka kufaidi nini? Mmeshindwa, lazima m-face problem, lazima m-face utulivu, lazima mkae muwaache walioshinda watekeleze ilani ya uchaguzi. Sasa leo eti timu imefungwa bao tatu bila, hiyo hiyo inataka ishangilie. Nyie mbona mnachekesha! Mimi sijawahi kuiona hii. Hii naiona Tanzania tu. Mtu anasimama anasema, ohoo, tunanyimwa hiki, tunanyimwa hiki. Si mmeshindwa, mtulie. Lazima... (*Makofi*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwege kaa chini, Mheshimiwa Lusinde endelea.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ndiyo maana unaona kunaundwa Kambi ya Serikali na Kambi Rasmi ya Upinzani na wanaundwa Mawaziri wa Serikali na Mawaziri Kivuli. Leo wanaona aibu hata kutaja Wizara zao, kwamba huyu ni Waziri Kivuli. Hawasemi, kwa sababu wanajua kivuli hakiaminiki. Nani ataamini kivuli? Wanajua kivuli saa sita kiko sawa na mtu, saa saba kinaanza kuwa kirefu, saa 12 kivuli ni kirefu kuliko mtu, wanajua. Wewe uliwahi kuona wapi Mbunge unasimama unampangia Mheshimiwa Rais kitu cha kufanya? (*Kicheko/Makofi*)

Jamani hii nchi mbona hatuna heshima, unampangia Rais kwamba akija kwangu afanye moja, mbili, tatu, hivi nyumbani kwako hata baba yako mzazi unaweza kumpangia wewe kwamba, leo baba tule hiki, inawezekana? Haiwezekani, kwanza hamjasoma vizuri Katiba ya nchi, Rais wa nchi ni mkuu wa nchi, Rais wa nchi ana madaraka makubwa ambayo hata kikatiba hajayatumia, mnapiga

kelele; Rais hayo madaraka yake akiyatumbia hamponi ninyi.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana mimi sasa naawaomba Watanzania hebu mwakani tukubaliane, unajua wakati mwingine kuwahi sana nalo ni tatizo, kuwahi sana nayo ni shida.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba, kuwahi sana ni tatizo. Tunaambiwa hata mtoto wa kike wakati mwingine asubiri akomae via vyake vya uzazi ndio abebe ujauzito, kinyume cha hapo ataugua. Upinzani wa Tanzania uliwahi sana, kwa hiyo, nahisi umepata matatizo, uliwahi sana. Kwa hiyo, sisangai kuwaona Kambi nzima ya Upinzani badala ya kujenga hoja za kisiasa zenye muelekeo wa kusimua Serikali mnaleta hoja za udumavu; angalia upinzani ulivyodumaa kwa sababu ya kuwahi, wamewahi sana kabla ya wakati wao wamejikuta wamedumaa. *(Makof/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natangaza kwenye Bunge hili, tatizo tulilonalo tuna upinzani mdumavu. Wamedumaa kisiasa, wamefika mahali hawawezi kujenga hoja mbadala, kazi yao ni kulalamika na kupiga kelele kama unavyowasikia. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri nchi yetu Mheshimiwa George Mkuchika kwenye utawala bora ashikilie hapohapo. Hakuna nchi yenye utawala bora usio na mipaka, haipo duniani. Wameng'ang'ana wanataka kufanya maandamano ya nini? Mbona mazoezi asubuhi hawaendi sembuse maandamano? *(Makof/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Serikali ya namna hiyo duniani, uruhusu watu wafanye fujo tu. Eti mtu anasema ooh, mimi nataka niende nikahutubie mkutano, wewe jimbo lile umeshindwa ukahutubie kitu gani? Utaeleza nini? Huna sera, huna ilani, huna kazi unayoifanya pale unataka

ukahutubie ueleze nini? Kama sio kufanya kampeni kabla ya wakati? Ninyi mnataka mpate ruhusa ya kwenda kufanya kampeni kabla ya wakati, sisi ndio washindi jamani tunashindwa hata na *Miss Tanzania*? Kachaguliwa mrembo mmoja, wengine wote wamekaa kimya, wamekaa kimya, lakini hawa wanashindwa; sisi ndio washindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakasikia kadada kamoja kanasema Lusinde nakupenda, tulia dawa iingie. Mimi nina mke na watoto watano, tukikutana nao kwenye chai wanaongea maneno ya unafiki kabisa, ooh tunaunga mkono, mnachapa kazi vizuri, tunaunga mkono. Tukija humu ndani wanajifanya ooh, Mwenyekiti patachimbika, pachimbike kwa hawa? Hakuna kitu cha kuchimbika hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali ishikilie hapohapo. Angalia kuna watoto wanawaona wanavyozomea, wanawaona ni watu wamechanganyikiwa kabisa. Humu ndani ya Bunge kuna watu wanakuja kujifunza uendeshaji bora wa Bunge, wao wameongea sisi tumenyamaza...

MBUNGE FULANI: Umechanganyikiwa wewe.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: ...sisi tunawapa dawa, ooh, ooh. Watoto wadogo hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakusihi, tunaomba Serikali kwenye kusimamia sheria isiangalie huyu mpinzani, isiangalie huyu CCM, wote kula kichwa, wakivuruga amani weka ndani, hizo siku 120 walizosema ni kidogo. Kwa hiyo, nataka nikwambie dawa yake ukitaka nchi inyoke, sheria zifanye kazi asiwepo mtu wa kubembelezwa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hiyo dawa kuingia naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Emmanuel Papian wajiandae. (*Makofii*)

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa kupata nafasi ya kuongea jioni hii ya leo. Kwanza naomba nianze na kumpongeza kabisa Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa jinsi ambavyo anachapa kazi na kuwalettea maendeleo wananchi wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sijampongeza na kuwapongeza hasa Mawaziri ambaao kimsingi leo tunajadili hotuba zao. Mheshimiwa Waziri Jafo nampongeza sana kwa kufanya kazi kubwa ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lakini pia nampongeza sasa baba yangu Mheshimiwa Mkuchika, ambaye alishakuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbulu kwa miaka kadhaa, hongera sana mzee wangu, chapa kazi, akazie uzi hapohapo; lakini nawapongeza pia, Naibu Mawaziri katika Wizara zote mbili, ili kuokoa muda, pia na Makatibu Wakuu kwenye Wizara zote hizi mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani pia, kwa kututengea fedha za kujenga Kituo cha Afya cha Dongobesh, Mheshimiwa Waziri nampa hongera sana. Wakati naingia jimboni nilikuwa sina kituo kabisa cha afya, lakini leo tunajenga kituo cha afya ametupatia milioni 700, Mungu awabariki sana, lakini pia wametupatia bilioni moja na milioni 500 tukajenga Hospitali ya Wilaya pale Dongobesh. Mheshimiwa Waziri namshukuru sana na nashukuru sana kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nashukuru juzi wametupatia fedha za maboma. Tumepata milioni 230 kwa kujenga maboma kwenye shule za sekondari tisa. Biblia inasema ni bora kushukuru nami naishukuru sana Serikali yangu kwa kweli, kwa kutujalia na kutupatia fedha nyingi kiasi hiki, hizi ni pongezi kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biblia inasema kwa Waefeso 5:4, naomba niwakumbushe wachangiaji wenzangu. Waefeso 5:4 anasema: "*Wala aibu wala maneno ya upuuzi si vema na hata ubishi hayampendezi Mungu, ni afadhali kushukuru.*" (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetazama bajeti hii. Nimetazama na kusoma Wizara zote mbili, kuna mahali pa kupongeza Serikali na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyofanya kazi usiku na mchana. Kwa nini? Ukiangalia leo hospitali za wilaya zimejengwa na maeneo mengi tunapata huduma. Vituo vya afya viko vingi na sasahivi naona 57 vinakwenda kujengwa. Tusiposhukuru tutakuwa na hali ya kutorudisha fadhila na shukrani. Mimi nashukuru sana Serikali na niko kifua mbele nimetumwa humu kuwashukuru kwa ajili ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili ninao ushauri, ukiangalia *TARURA* bajeti yake kwa miaka miwili iliyopita imeanza kupungua. Mwaka 2017/2018 imepungua kwa asilimia nane, lakini mwaka jana kwa asilimia 16 na mwaka huu imezidi kupungua. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, tumeanzisha *TARURA* ili ikasaidie kujenga barabara za vijijini na mijini, lakini ukiangalia kwa jinsi ambavyo bajeti ya *TARURA* inapungua, tutashindwa kujenga barabara ambazo amesema mwenyewe hapa kuna kilometra 108,000; kwa kweli kwa pesa hii itakuwa shida sana kuisaldia *TARURA*. Hivyo, naungana na Wabunge wenzangu waliosema kwamba, *TARURA* iongezewe fedha. Hii asilimia ya kugawana, mgawanyo wa kwake *TARURA* na *TANROADS* kwa kweli uangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *TARURA* inakwenda mbali na mzunguko wake ni mkubwa na vijijini, niombe basi tuone namna ya kufanya, tuongezee fedha na fedha hizi tupange asilimia. Sasa hivi inaonekana ni asilimia 30, ni ndogo sana, tuongeze basi asilimia hizi angalau ziende 40 au 50. Nashukuru *TARURA* kwa mwaka huu wamenisaidia, wamejenga madaraja mawili na nimeona kwenye bajeti hapa kuna Daraja la Qambasiro na *calvat* ya Gidimadoy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe, kuna barabara mbili ambazo kwa kweli, hazipitiki sasa hivi. Barabara ya Masieda kwenda Mongo wa Mono kufika mpaka Yaeda Chini, wako Wahdzabe kule sijawahi kuwafikia, barabara haipitiki kabisa. Niombe Ndugu yangu aangalie kwenye bajeti hii tupate barabara ile, lakini kuna barabara nyingine kutoka Masieda kupitia Laghangesh kwenda Yaeda Chini, naomba barabara ile aiangalie vizuri, iwekewe fedha ili walau hata sisi tuwe na namna ya kutembea. Nami napigania na ku-support uongezaji wa asilimia za barabara katika *TARURA* ili basi barabara hizi ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimeangalia, ndugu zangu wapinzani au upande wa Gaza wanasema, kwa nini nimesoma mstari wa Biblia, nimetaka hata washukuru. Nimeangalia kuna mzungumzaji mmoja hapa kabla yangu ame-quote maneno ya mtu anayeltwa mwanazuoni na amesema yeye mwenyewe uzalendo kwanza na nini maana ya uzalendo ku-support nchi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeangalia kwenye mpango wa bajeti ya mwaka huu, ukiangalia Rombo kwa Mheshimiwa Selasini pale, kapewa hospitali. Sasa sijaona kwa nini watu hawa hawashukuru mara nyingi? Nami nawaza humu kwa nini shukrani zisitokee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukienda Kilombero kumepewa milioni 500, lakini ukienda *Arusha A/CC* pale kumepewa milioni 500, ukienda Ubungo wana fedha pale, ukienda Kigoma wanayo. Sasa huwa nawaza humu ndani, jamani hata shukrani kidogo tu hakuna? Nadhani wakati fulani yako mambo ambayo hayaendi vizuri tuseme, lakini mambo ambayo yanaenda vizuri tushukuru, hata kwa jambo moja tu. Ndio maana mara nyingi ni lazima kushukuru, tusiposhukuru ndugu zangu hata Mheshimiwa Waziri na wanaofanya kazi chini yao wataona kama vile hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa pamoja na shukurani hizi naomba nielezee ahadi za Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa

Rais wakati anapita aliahidi kilometa tano pale Hydom na kilometa mbili Dongobesh na Mheshimiwa Waziri nina hakika amefika Dongobesh na Hydom, ili Rais wetu asionekane kwamba, ameahidi na hajatekeleza, niombe basi katika bajeti ya mwaka huu atenge hata kilometa tatu au mbili, ili walau tuonekane tunaanza kujenga barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli barabara zetu hazina lami, nami nashukuru Mungu walau naona mpango wa Serikali wa kuweka lami katika wakati ujao, lakini naomba basi kipindi hiki cha mwaka huu wa 2019 kwenda 2020 kwa kweli, tuione lami ya Hydom ikiwekwa kwenye bajeti hii. Mheshimiwa Waziri nimempelekea maombi na naomba maombi haya ayachukue, aniwekee lami kilometa zile zilizoahidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaIDI naomba kuna shule ya sekondari ambayo wananchi wanaijenga kule Maretadu, wanajenga kidato cha tano na cha sita kwa fedha zao. Tumejenga madarasa manne na tumejenga bwalo, sasa naomba tu fedha za kumalizia ili mambo yaende vizuri. Kwa nini nashukuru? *Principle* ya kushukuru ni hivi unaposhukuru maana yake unaomba mara ya pili. Niombe ndugu yangu fedha atuwekee pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu pia katika ugawaji wa vijiji na kata. Inawezekana kweli kukawa hakuna bajeti ya namna hii, lakini waangalie kuna vijiji ambavyo vimeshakuwa vikubwa na vingine vitongoji vina shule ya msingi na wanahitaji kuona kwamba, wanapata uongozi wao. Katika hili wafikirie, nina kata mbili za Maretadu kule na Haidereri wameanza kujenga shule zao za vitongoji na wako vizuri na wanaendelea kufanya kazi hii ya kui-support Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga hoja mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Massay. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Mollel, baadaye Mheshimiwa Emmanuel Papian ajiandae.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na hatimaye kusimama mbele yako kuweza kuchangia bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya. Vilevile nawashukuru sana Makamu wa Rais, Waziri wetu Mkuu ambaye amekuwa ni kiongozi wetu na mshauri wetu kwa kazi kubwa anayofanya na katika kumshauri pia Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri, nampongeza sana Mheshimiwa Mkuchika na siku zote wanasema penye wazee hapaharibiki neno; amedhihirisha ye ye ni baba, amedhihirisha pamoja na yote hayo na kama wanavyosema Waswahili kwamba, mkubwa aktivuliwa nguo basi anachutama. Yeye ni jalala, lakini tunaona, tunamkubali na tunaona yale yote anayoyafanya. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri kwa ushauri mzuri na kazi nzuri anayomsaidia Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Jafo. Ameonesha umahiri mkubwa sana hasa katika kutatua changamoto nydingi zinazowakabili wanawake. Ameweza kumsaidia na kumshauri Rais na hatimaye sasa tunaona matunda mazuri yanayofanyika, nampongeza sana na namwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumtia nguvu, kumpa ujasiri na afya aendelee kuwatumikia Watanzania. Waheshimiwa Manaibu Waziri pia na wao tuwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kuchangia kuhusiana na asilimia mbili ambayo katika Bunge la Bajeti mwaka jana tulipitisha. Asilimia hii mbili tumeona ni kwa jinsi gani ambavyo imekuwa na mafanikio katika kusaidia makundi maalum na hasa kundi la watu wenye ulemavu. Niombe tu kwamba, kuna baadhi ya Halmashauri ambazo bado hazijatimiza matakwa ya Sheria hii ya Fedha (*Finance*

Act); naomba sana azisimamie ili basi ziweze kutoa hiyo asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nishauri kwamba, kumekuwepo na changamoto baadhi ya watu wenye ulemavu ambao wako maeneo tofautitofauti, naomba kwamba, busara itumike tuangalie ni kwa jinsi gani ikibidi basi kama ni mmoja mmoja basi tuwakopeshe kwa sababu, wapo ambao tumeona wamefanya vizuri sana. Kwa hiyo, kusiwe na kigezo kwamba, lazima wajunge kwenye vikundi naomba sana ofisi iweze kuangalia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayofanya hasa katika kutoa elimu bure. Nami nimekuwa siku zote nikithhibitisha kwamba, elimu hii bure imesaidia baadhi ya watoto wenye ulemavu kupelekwa shule ambao walifichwa majumbani, lakini kwa sababu elimu ni bure wametolewa na sasa hivi wako kule. Changamoto iliyopo ni miundombinu, bado ni tatizo. Naomba sana Serikali kuona ni kwa jinsi gani watasaidia katika kutatua changamoto hii ya miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika shule zote za sekondari tumeona na nashukuru sana wananchi kwa ujumla wamejitoa sana, Wabunge wamejitoa sana katika kuiunga mkono Serikali. Naomba kuona kwamba, ni kwa jinsi gani sasa katika shule hizi za sekondari, zile shule ambazo zina mabweni basi watoto wenye ulemavu waweze kupelekwa kule ili wasipate shida wakasome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia watoto wenye ulemavu ambao wanakwenda katika shule ambazo ni maalum na Serikali ilikuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba, inatoa fedha wakati shule zinapofungwa, lakini hivi sasa watoto wale imekuwa ni shida kwa sababu wengine wanalaazimika kukaa muda wote shule mpaka inapofika Disemba. Namshauri Mheshimiwa Jafo, ameonesha umahiri mkubwa, naomba awaangalie watoto hawa kwa jicho la

pekee, wapewe nauli ili unapofika wakati wa kurudi nyumbani basi waweze kurudi nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *hostel*/zitasaidia sana kwa sababu, kwa mfano kule kwetu jamii ya Wamasai, kama mnavyofahamu, mtoto wa kike akiwepo nyumbani ni rahisi sana kuolewa. Naomba sana *hostel*/kwa ajili ya shule ambazo zipo kwa mfano Shule ya Sekondari ya Oldonyowasi ambayo ni mpya imejengwa hivi karibuni na ndio wameanza kidato cha kwanza. Naomba ujenzi wa *hostel* katika Shule hii ya Oldonyowasi, ili basi waweze wanafunzi wale ambao wengi wao ni kutoka katika jamii yetu hii ya wafugaji waweze basi kukaa *hostel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naenda haraka haraka, vilevile naomba nizungumzie suala la Walimu; Walimu kwa kweli, kukopa kunasaidia na asiyekopa hafahamu nini maana ya kukopa, lakini baadhi ya taasisi za kifedha zinawaumiza Walimu na baadhi ya Walimu wamekwishaacha shule. Naomba niitaje *Baypot* imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa Walimu ambao kwa kweli, wengine wamelazimika kuacha shule na kukimbia ili kukwepa hiyo mikopo ambayo imekuwa ni kero kubwa kwao. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha uko hapa, alitazame hilli ili kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana *TARURA* na kipekee kabisa kwa sababu, natoka Mkoa wa Arusha, nampongeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Arusha, nampongeza Meneja wa *TARURA* katika Halmashauri ya *Arusha DC*. Niombe tu sasa kwamba, kweli wanahitaji kuangaliwa ni kwa jinsi gani tunawaongezea bajeti ili waweze kutimiza yale malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilli ni jambo ambalo kwa kweli ni la kutolewa mfano. Ni jambo ambalo kwa kweli, la kushukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imeweza kujenga vituo vyta afya na vituo hivi vyta afya vinakwenda kutatua changamoto ya vifo vyta wanawake na watoto. Haijawahi kutokea, tuna kila sababu ya kujivunia Rais wetu Mheshimiwa

Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ambaye, tumeona fedha zinazopatikana zinatumika katika kuhakikisha kwamba, zinafanya yale ambayo yamekusudiwa. Vituo hivi pamoja na hospitali za wilaya zinazokwenda kujengwa haya ni mapinduzi makubwa ya maendeleo, naipongeza sana Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu pia tumeona ni kwa jinsi gani Rais wetu kutokana na utawala bora amedhihirisha miradi hii mikubwa kama kusingekuwa na utawala bora, basi isingewezezana; leo hii kuna *Stieglers Gorge*, tunaona kwamba, nikwa jinsi gani tatizo changamoto ya umeme itakwenda kutatuliwa. Tumeona Mradi wa REA, lakini sio hilo tu, ujenzi wa reli ya kisasa, vyote hivi ni maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuangalie pia katika Jiji la Dar es Salaam, tuangalie Ji la Dodoma jinsi ambavyo unapendeza na majengo yale ya Serikali. Hii yote ni kutokana na utawala bora na matumizi sahihi kabisa ya fedha katika kuhakikisha kwamba tunasimamia na kuleta maendeleo ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa, mimi naipongeza sana Serikali na Mawaziri kwa vifua walivyonavyo vya kuweza kuhimili yote hayo na msivunjike moyo. Kama ndani ya miaka mitatu ambapo sasa hivi tupo mwaka wa nne, Rais Magufuli ameweza kufanya yote hayo, wapo wengine ambao ndani ya miongo zaidi ya miwili mpaka leo hii hawana hata ofisi ya chama, kwa nini tusimpongeze Rais wetu Magufuli kwa kazi kubwa aliyofanya. Nampongeza sana, tunamtia moyo Rais wetu ili kuhakikisha kwamba anzidi kuwaleta Watanzania maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Watanzania wanaona na 2020 siyo mbali mwakani tutaona Watanzania watakachoenda kufanya na nina uhakika kwamba CCM itaendelea kutawala. Upinzani bado upo nyuma sana kwa hiyo sisi tutaendelea kutawala kwa sababu ya sera nzuri na utawala bora tulionao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Waheshimiwa Mawaziri hongereni sana, msivunjike moyo tuendelee kufanya kazi na sisi Wabunge kumbukeni ni askari miamvuli wenu humu ndani kwa hiyo kabla hamjafikiwa nyie sisi tutakuwa wa kwanza. *Alluta continua*, mapambano yanaendelea CCM iendelee kutawala. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Amina. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Papian, na Mheshimiwa Innocent Bilakwate ajiandae.

MHE. EMMANUEL P. JOHN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nipongeze Mawaziri ambao wametuletea bajeti yetu hii, Mawaziri wote wawili kwa ushirikiano mkubwa na bajeti nzuri ambayo imeweza kutusaidia kutupa malengo na mwelekeo wa 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa kazi nzuri na bajeti ambayo mmetutengea Kiteto kwa maana ya *TARURA* kutupa shilingi bilioni 1.6, *secondary school* shilingi bilioni 1.4, *primary school* shilingi bilioni 1.2, Kituo cha Afya cha Engusero shilingi milioni 200 na maboma yanaendelea kumaliziwa. Hongereni sana kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki ambacho tunaelekea mwishoni mwa bajeti ya 2019 naomba tupate pesa za kumalizia jengo letu la Halmashauri ambalo limesimama muda mrefu. Mheshimiwa Waziri Jafo unajua kabisa hili jengo lipo ukingoni tunahitaji mtutengene pesa kwa haraka ili angalau katika hii miezi miwili mitatu tuweze kufanya kazi ambayo tunadhani kwamba ingeweza kutusaidia kumalizia hilo jengo ili tukafanyie uchaguzi mahali ambapo pako safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi hii ya kimkakati ambayo tumeomba pesa na miradi mingi ambayo inaendelea, naomba na kushauri Serikali kwamba kwenye miradi hii ya kimkakati Serikali ingeweza kuainisha maeneo

ambayo yanaweza kuwa na miradi ambayo ni *highly paying* ili iweze kui-*fund* mapema inaweza kusaidia zile Halmashauri kutengeneza ile *internal income* yake na kusaidia kupunguza utegemezi Serikali Kuu, jambo hili linaweza kusaidia sana Halmashauri. Zile Halmashauri ambazo hazina miradi mikubwa wala vyanzo vya mapato, inaweza kuhamisha ile pesa ambayo ingeweza kuwa inaenda kwenye zile Halmashauri ikapunguza zile pesa zikaenda kwenye zile Halmashauri na kuhakikisha kwamba tunatengeneza uwiano wa mapato kwenye Halmashauri zetu na kuhakikisha kwamba tunasukuma gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora. Kwenye utawala bora pale Kiteto tuna nyumba yetu ya TAKUKURU imeharibika na imekwisha. Nilitaka kumwomba Waziri, Mheshimiwa Mkuchika ikikupendeza tuondoke hapa wakati wowote baada ya maswali na majibu ukaangalie hilo jengo, ikikupendeza ukitutengea shilingi milioni 15 tukitumia *force account* ile jengo tutalikarabati na litakuwa salama. Mimi nikuombe kwa hilo ukubaliane na mimi kabla hujaamua lolote twende kule uone halafu turudi tuweze kuamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo la *TASAF*. Katika kusaidia kaya maskini tuli-*form* mfumo ambao uliweza kusaidia watu kukatiwa bima ya afya. Watu wamekuwa wanakatwa pesa zao, bima za afya zinachelewa kuja, watu hawapati matibabu, pesa zinakwenda na mwaka unaisha halafu wanaendelea kupoteza hela zao. Naomba Mheshimiwa Waziri ujitalidi ulione hili na ni namna gani tunaweza kufanya kwa ajili ya kupata bima ya afya basi hizo pesa zinapokatwa bima ya afya iwahi na watu waweze kupata matibabu katika mwaka husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumza juu ya suala la Madiwani. Madiwani wetu sasa hivi ni viungo muhimu sana na wanafanya kazi sana kwenye maeneo yetu. Madiwani hawa sasa hivi ndiyo wanaoweka *pressure* ya kusimamia kwenye Baraza la Madiwani na *WDC* zao kwa ajili ya kusukuma shughuli za maendeleo ya ujenzi wa hivi vituo vya afya vinavyojengwa kote nchini. Madiwani hawa ndiyo

tunaowabana kwa ajili ya kujenga maboma na kusimamia pesa kwa kutumia *force account* ili waweze ku-manage zile fedha vizuri. Madiwani hawa ndio wanaosimamia miradi ya maji, ukusanyaji wa kodi, mapato na ushuru wa Halmashauri kwenye vyanzo vyetu ili kuona ni namna gani ya ku-push maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali na Mheshimiwa Jafo mlione. Nilikuwa naangalia tuna Madiwani zaidi ya 3000 nchi nzima, Madiwani hawa tungewapa pikipiki. Mimi Diwani mmoja anatembea kilomita 120 kwenda na kurudi ni 240, huyo Diwani atakwenda wapi na wapi? Haiwezekani! Nina Diwani ambaye lazima akienda kwenye eneo lake la kijiji fulani lazima alale huko na kesho yake arudi, anapita maporini kuna *incidence* nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Waziri liangalle suala hili tupate pikipiki kwa sababu tume-afford kuwapa wataalam wa elimu kwenye kata zetu, tuone ni namna gani tunaweza ku-support hawa Madiwani wapate vyombo vya usafiri mafuta watajitegemea lakini tuone namna gani wanaweza kuwa *motivated* na kusukuma gurudumu la maendeleo kwenye maeneo yetu na maagizo mengi ambayo Wakurugenzi wetu wanawaagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la maboma; Kiteto tuna maboma 92 ya *primary schools, secondary schools* tumeshamaliza kwa kutumia mapato yetu ya ndani. Niombe tusaidiwe pesa haya maboma yaweze kumalizwa kwa wakati kwa sababu watoto wetu kutoka *point* moja kwenda nyingine anakwenda kilomita 56; hatuwezi kupeleka wale watoto kwenye hayo maeneo kwa kuanza *primary school*. Tuna watoto ambaao hawawezi kusafiri umbali mrefu na kurudi nyumbani kwa jiografia ya Wilaya yetu maeneo ya kifugaji ya Ndido, Makame, Rolela, Sunya na kuna maeneo mengi ambayo ni makubwa na mapana ambayo watoto hawawezi kwenda shule na kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha shule sikizi, zinawasaidia wale watoto kujuua kusoma na kuandika,

vinginevyo tusipofanya hivyo tuta-create mfumo wa kuwa na watu ambaio hawajui kusoma na kuandika na mwisho wa siku wataogopa kwenda shuleni kwa kusubiri hizi shule zikafunguliwe. Niombe *review programme* yenu ya kuangalia ni namna gani ya kusajili hizi shule, muangalie madarasa yanayofikiwa, mfumo upi utumike ili watoto wetu waweze kuanza shule na zile shule ziweze kufunguliwa, mpunguze aina ya vigezo ambavyo mnaona kwamba vinaweza kusaidia kuhakikisha kwamba hizi shule zinaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumalizia kwa kusema yafuatayo. Nimeona wenzetu watani zetu na wengine wanalamikia Serikali na Rais kwamba hakuna utawala bora. Watu wanasema kwamba hapatatosha, patachimbika, naomba niwaambie Rais Magufuli ukimwambia kwamba kesho hapatachimbika patatokea fujo, anataka hapohapo. Ogopa Rais ambaye hawezikurudi nyumba *ana-change gear* angani kukabiliana na mapambano, huyo ndiyo Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishaona una kiongozi huyo hapo juu, wewe unachofanya *always* unakuja mezani *mn-debate* hoja yako, mnatatua mgogoro mnamatiza, *ana-solve* matatizo yako akimaliza mnapeana mikono kwaheri. Ukitangaza msuli kwa namna Rais wetu Magufuli alivyo na namna anavyotekeleza shughuli, bora akufyatue mambo mengine mtajadili baadaye. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape mfano maana tunazungumza kwa mifano, Kibiti hapa juzi walisumbua mbele nyuma, amefyatua mapolisi waliokuwa wanalinda na ule upuuzi uliokuwa unafanyika pale. Amegeuza viongozi pale, amehakikisha amepeleka mtu mmoja tu amecheza vizuri sembuse mahali ambapo panawaka taa. Niwaombe tukae mezani, tujenje Tanzania kwa kushauriana, *tu-debate* wote, tutafute *solution* ya *issues* zinazoikabili nchi kwa pamoja bila kutishiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe niwaambie Tanzania ina demokrasia ya kutosha, nchi nyingine

zinazotuzunguka, wapinzani na wabishi wote wanazungumzia ughaibuni na nje ya nchi. Unatoka hapa unazungumza mtaani na unarudi nyumbani unalala; unatoka hapo unatukana unarudi unalala, huyo Rais leo *East and Central Africa*, utampata wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niwaambieni hapa ndiyo tunaagana, tunatafuta nani anaenda kibra kazaneni na sisi tunakazana, kesho kutwa 2020 mechi uwanjani biashara imekwisha, huko ni CCM, huku ni CCM kazi imeisha. CCM hoyee, Mungu awabariki sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Papian. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Mahawe na baadaye Mheshimiwa Maryam Msabaha ajiandae.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nimshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja zilizopo mbele yetu za Wizara zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pale alipoishia kaka yangu Papian na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano ambaye ndiye aliyependwa na Watanzania kuinadi llani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 - 2020. Huwezi kusimama katika Bunge hili ukashindwa kusema habari za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, vinginevyo wewe hautakuwa mzalendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanyika katika nchi hii. Kabla sijaenda mbali, nielekeze pia pongezi hizo kwa Waziri wa TAMISEMI, kaka yangu Mheshimiwa Jafo na Naibu wako, nielekeze pongezi hizi kwa ndugu yetu Mheshimiwa Mkuchika na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, Mungu awabariki sana kwa utendaji wenu uliotukuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na nukuu hii inasema: "*A good leader is not measured by how long he/she stayed in a particular position, it is measured by how*

many positive changes you brought over there." Tangu Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli mambo makubwa yamefanyika katika nchi hii na ni kazi yetu sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kuzitafsiri kazi hizo kwa wananchi wetu kupitia Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye suala zima la afya, niipongeze Wizara ya Afya pamoja na hii Wizara ya TAMISEMI kwa upande wa miundombinu. Tangu mwaka 1961 mpaka leo tulikuwa na vituo vya afya visivyozidi 695 lakini ndani ya miaka mitatu kutokana na utendaji uliotukuka wa Serikali ya Awamu ya Tano tumejengewa vituo vya afya zaidi ya 300. Unaanzaje kubeza juhudhi kama hizi? Msema kweli ni mpenzi wa Mungu, wanasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais na Wizara ya TAMISEMI, hongereni sana, kazi yenu ni nzuri sana, mnaokoa vifo vya akina mama na huduma za afya zinapatikana. Ni kweli changamoto ndogo ndogo bado zipo, wanasema hata Roma haikujengwa siku moja, hatuwezi kumaliza changamoto kwa siku moja. Hii nchi ni kubwa, wananchi wake ni wengi na mambo yanayotakiwa kufanyika ni mengi lakini lazima *tu-recognize* juhudhi zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano tangu 2015 *to date*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie na suala la elimu. Ni kweli kwamba kuna changamoto lakini lazima tuseme yale mazuri makubwa yaliyofanyika. Changamoto ya ukosefu wa miundombinu ni kwa sababu ya elimu bure ambayo imetolewa katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano. Usajili umekuwa ni mkubwa sana katika shule zetu ambao umepelekea kupungua kwa matundu ya vyoo, madarasa na kadhalika lakini bado kazi kubwa imefanywa na maboma mengi yamejengwa. Sisi tu Mkoa wa Manyara tumeletewa fedha za EPforR zaidi ya shilingi bilioni saba kwa ajili ya kumalizia maboma katika Mkoa wa Manyara, naishukuru sana Serikali hii ya CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamejengwa matundu mengi ya vyoo lakini bado kuna changamoto. Niendelee kuomba Wizara ya TAMISEMI waweze kuzingatia hitaji hili kwa sababu kwa asilimia kubwa lina-affect watoto wa kike wanapokuwa kwenye mizunguko yao ile ya mwezi wanashindwa kuhudhuria shule kwa sababu ya mazingira mazuri ya maeneo hayo ya kujisitiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masula mazima ya upungufu wa walimu wa sayansi ni kilio kikubwa. Tumejenga maabara za kutosha na tunatengeneza nchi ya viwanda, ni lazima tuwekeze kwenye elimu na walimu wa sayansi. Upungufu wa walimu wa sayansi ni mkubwa, upungufu huu ni janga la kitaifa. Tuwa-motivate watoto wetu kuanzia kwenye *level* za primary school kupenda sayansi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli walimu wa sayansi huwa ni wakali na wakati mwininge watoto wasipoelewa ukali unapozidi basi unakuta wanatoa adhabu mbalimbali na watoto hao wanajikuta wamechukia masomo hayo ya sayansi na hisabati. Niwaombe walimu wenzangu twende taratibu, tunahitaji kuwajenga wanasayansi ili nchi yetu iweze kupata wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwa uchache suala zima...

TAARIFA

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Ester subiri.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwasihi Wabunge wamsikilize kwa makini Mbunge ajaye wa Jimbo wa Babati Mjini. Ahsante. (*Kicheko/Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Mahawe, naomba uendelee.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa ruhusa hii ya kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu, mimi natokea Mkao wa Manyara ambako wenyeji wetu wengi ni wafugaji na shule zetu nydingi za sekondari hazina mabweni na hosteli za kutosha. Nishukuru tumepeata hosteli kadhaa, siyo chini ya 10 katika Mkao wetu wa Manyara lakini hazitoshi hasa Wilaya ya Kiteto na Simanjiro, wale watoto wanatembea umbali mrefu mno. Kama unavyofahamu sisi wafugaji watoto wa kike wanaolewa haraka sana, naomba ili ku-rescue watoto hawa, shule hizi ziweze kupata *hostels* ili watoto wale waweze kumaliza masomo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la afya. Nishukuru sana kwa ajili ya mambo mengi yanayoendelea kufanywa na Serikali hii lakini nina ombi la dhati kabisa kwa ajili ya magari ya wagonjwa katika maeneo mbalimbali katika Mkao wa Manyara. Hospitali ya Mbulu haina gari la wagonjwa, liliopo ni chakavu na Kituo cha Afya cha Ngusero hakina gari la wagonjwa, tunaomba sana kusaidiwa. Niliiwahi kuomba gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Orkesmet mbele ya Makamu wa Rais, nina hakika ombi hili linaendelea kufanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkao wa Manyara, jiografia za Kiteto na Simanjiro zimekaa vibaya kuliko mahali pengine popote nchi hii. Akina mama wakati mwingine wanapata tabu wanapopelekwa hospitali kujifungua. Naomba tena gari kwa ajili ya Orkesmet na Kituo cha Afya cha Ngusero, Kiteto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba gari kwa ajili ya Hospitali ya Mrara, Babati Mjini, gari ni moja na ni chakavu. Kama hiyo haitoshi, Hospitali ya Wilaya ya Babati Mjini ilianza kama zahanati miaka ya 1956, imeongezwa jengo moja moja baadaye ikawa kituo cha afya, leo imekuwa Hospitali ya Wilaya, majengo yapo *scattered* hayana mpangilio, wodi ya wazazi ipo mita 100 kutoka *theatre*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unafahamu ukiingia kwenye kile chumba ama miguu itangulie kaburini au wewe mwenyewe mzima mzima. Sasa *imagine theatre* ipo 100 metreskutoka kwenye *labor ward*. Hili jambo nakuomba sana Mheshimiwa Jafo ultazame kwa macho ya huruma. Naomba sana suala la Hospitali ya Mrara litazwamwe vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu wa watumishi wa kada ya afya katika Mkao mzima. Tunajua juzi TAMISEMI wamejitätahidi sana, wameachilia ajira lakini bado tuna upungufu kadhaa. Kada ya afya ni muhimu sana, ndio inayo-save maisha ya wananchi wetu. Ikitokea tu bajeti kidogo ya kuweza kuruhusu kuongeza watumishi wa kada ya afya tunaomba Manyara tukumbukwe kwa namna ya tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza nilikuwa naomba nizungumzie suala la lishe. Ni kweli kwamba tuna tatizo la lishe...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester malizia, muda wako umeisha.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niseme tu udumavu ulipo Mkao wa Manyara ni asilimia 36 na hili linachagizwa na ukosefu mkubwa wa maji; akina mama wengi wanatoka asubuhi wanarudi usiku hawana hata muda wa kuwaandalia watoto wao chakula kizuri hata kama kipo. Naiomba sana Serikali yangu, Ofisi hii ya TAMISEMI itusaidie kutazama namna ambavyo tutamalizana na changamoto ya miundombinu ya maji ili hatimaye tuweze kupata vijana wazuri watakaolilea taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, Mungu akubariki sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Mahawe. Tunaendelea na Mheshimiwa Maryam Msabaha, baadaye Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Tauhida Gallos wajandae.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na kwa pumzi hii. Pia naishukuru Ofisi ya Spika na Katibu wa Bunge na wafanyakazi kwa kuhakikisha napata matibabu na kurudi katika hali yangu ya kawaida; na Wabunge wenzangu wote walioniombea. Sasa hivi nimeimarika na nimesimama katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napongeza hotuba hizi mbili zote zilizowasilishwa na Mawaziri Kivuli kwa upande wa pili. Naiomba Serikali yale yote mazuri wayachukue wayafanyie kazi. Kuna mambo mazuri sana yamezungumzwa humu ndani na yataleta tija na changamoto kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye haki za binadamu. Haki za binadamu kwa kweli zinakiukwa. Tuangalie msongamano ulivyojaa kwenye magereza. Nenda Keko, Segerea, Tanzania nzima; zunguka mpaka Korogwe uende mpaka Arusha, kuna mahabusu wengi sana ambaao wako magerezani. Kesi zinachukua muda mrefu. Kibaya zaidi, wengine wanaumwa, wengine wamepata majeraha, wengine wamepigwa labda wamevunjwa vunjwa miguu, miguu inaoza mpaka wengine wanafika hata karibia kukatwa miguu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie hii kweli ni haki au ni utawala bora? Tuangalie sasa hizi kesi ni kwa nini zinachukua muda mrefu? Kwanza wale wanachanganywa; kuna watoto mle ndani, kuna wendawazimu na kila mchanganyiko ndani ya mahabusu. Sasa kuna haki au kuna utawala bora katika haki za binadamu? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sasa zile kesi ambazo ni ndogo ndogo au ni kwa nini zinachukua muda

mrefu? Zifanyiwe maamuzi ili wapate kutoka mle ndani na mzigo utoke kwa Serikali. Kwa sababu mnayvolundika watu kule, kwanza wale wanataka kula, miundombinu siyo rafiki, wamejazana, wengine wanaumwa *TB*, wengine wanaumwa maradhi ya UKIMWI, wengine wanaumwa maradhi nyemelezi. Kwa hiyo, sasa tunatafuta matatizo na tunaipa Serikali mzigo mbiti sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe Mahakama nayo inafanya kazi kwa kufuata sheria na haki. Pia tuhakikishe vyombo vya ulinzi na usalama vinavyowakamata raia wasiokuwa na hatia wasiwapige wakawaumiza wakawavunja vunja miguu, kwa sababu huwezi kumvunja vunja raia, ukawa ulishamuumiza halafu tena unamweka mahabusu huku hajapata huduma za huduma za afya. Kwa hiyo, pale kutakuwa hakuna utawala bora. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye utawala huu kuna watu wengi sana, sijui tunaambiwa wahujumu uchumi, tunaambiwa TAKUKURU wamewachukua, lakini vielelezo viko wapi? Vile vielelezo vinatakiwa vifuatiliwe sasa, kama kweli wamefanya makosa wasikae muda mrefu bila kuhukumiwa. Unakuta mtu anakaa hata miaka sita hata miaka kumi yupo tu mahabusu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tuangalie sheria ambazo tunazipitisha humu ndani. Hizi sheria, kwa mfano, Sheria za Vyama vya Siasa. Vyama vya Siasa, Waasisi wa Taifa hili walivyoleta vyama vingi hawakuwa wagonjwa. Hawakukurupuka! Hivi vyama vimeletwa kwa mujibu wa sheria. Chama ni mtu kuwa na uhuru wako binafsi, unaamua mimi niende chama gani? Chama siyo ugomvi, siyo kuhasimiana. Tumeletewa vyama ili tupate siasa bora, tupate maendeleo, tuosoane pale mnapokosea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta sasa hivi tumeleta sheria ya kukandamiza vyama vya siasa. Ninyi mnacheka, lakini msichekelee. Mwalimu Nyerere hakuwa mjinga, wala Mwasisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naye hakuwa mjinga. Ni kwa nini alileta vyama vingi? Wengi

ambao walikuja kutengeneza hivi vyama vingi pia walitoka upande wa pili wakaja huku tukatengeneza vyama. Sasa mbona mnakandamiza hivi vyama? Kwa nini mnaogopa kivuli chenu wenyewe mlichokitengeneza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vipewe uhuru, vitangaze sera zao. Upinzani siyo ugomvi, sio chuki, kwa hiyo, Wapinzani wapewe fursa kama Chama Tawala kinavyopewa fursa ya kufanya mikutano, kujieleza, kutoa sera zao, hata pale panapokuwa na uchaguzi, kuwe na uchaguzi wa haki bila kudhulumiana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnachekelea, mnaona hii mipasuko ya vyama vyaa siasa, lakini tunajenga matabaka yasiyokuwa na sababu. Tunajenga matabaka kwa baadaye ambayo tutapelekea nchi yetu kutokusikilizana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msome *history*, kwa mfano, vyama vyaa siasa kwa upande wa Zanzibar. Tuseme ile *CUF* ya Zanzibar na Chama cha Mapinduzi, mmetoka mbali. Kulikuwa na migogoro mpaka mkaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Serikali ile iliundwa ili msikilizane, mfanye kazi kwa pamoja turudi kwa pamoja na tupate muungano safi ili anayetoka Tanzania Bara anakwenda kule anakuwa yuko huru, anayetoka visiwani anakuja huku anakuwa yuko huru. Kujenga ni kazi, lakini kubomoa tunabomoa kwa siku moja.. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie, hawa washauri wa Mheshimiwa Rais, mshaurini na mpeleke taarifa za ukweli, msipeleke taarifa za uongo za kujipendekeza. Mumpe mustakabali wa siasa inavyokwenda, hasa siasa ya Zanzibar. Mumpe ukweli siasa ya Zanzibar iko vipi? Msione Wazanzibari wamenyamaza, wananyamaza lakini siasa ya Zanzibar ina wenyewe. Siasa ya Zanzibar siyo kama siasa ya Tanzania Bara. Ni kwa nini mnajenga chuki zisizokuwa na sababu? Ni kwa nini wengine mnafanya kazi kwa utashi wenu, kwa kujipendekeza ili kumgombanisha Mheshimiwa Rais na wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyie kama ni wateuliwa wa Mheshimiwa Rais, mfanye kazi kwa mujibu wa sheria, pale penye haki mfanye haki. Leo unakuta hata wengine mnabambikia watu kesi za kisiasa, mnawaweka ndani ili kutaka kupandishwa vyeo. Hiyo haitakiwi, mnamharibia Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, mnatakiwa kila mtu anayepewa nafasi yake, aisimamie na kila mtu anayeteuliwa aisimamie ile nafasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipaka yetu tuangalie sasa tumeingiza migogoro ya kisiasa isiyokuwa na maana. Mipaka yetu, usalama wa raia uko vipi? Kwa sababu tunajenga chuki, tunajenga makundi yasiyokuwa na sababu. Tuangalie haya makundi tunayoyajenga tutanufaika na nini? Tuangalie hizi chuki za kuchukua wapinzani tukawasweka ndani tutafaidika na nini? Tuangalie wawekezaji kwa nini wanakimbia? Tuangalie kwa nini watu hawataki tena kuja Tanzania? Sekta ya Utalii, kwa nini watalii wanapungua? Hii yote ni kwa kuwa tunajenga siasa ni ya chuki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Zanzibar ni kisiwa. Kuna visiwa viwili; Kisiwa cha Pemba na Kisiwa cha Unguja, vimezungukwa na bahari. Hii mipaka mmeilinda vipi? Hizi chuki mnazozipalilia, mnajjlinda vipi? Kwa hiyo, naomba mrudi mezani, make, msifanye siasa za ubabe. Fanyeni siasa za mustakabali wa nchi hii, tuangalie Muungano unakuwa vipi? Tuangalie vyama vya siasa vinapata uhuru wa kutosha wa kujieleza na wagombea wanakwenda kwenye kugombea bila bughudha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge wengine wanakuja hapa hata hawasaidii wananchi wao wale waliowapigia kura. Mtu anaweza kukaa hapa Bungeni miaka mitano hajawahi kuuliza swali, hajawahi kufika Jimboni, hajawahi kufanya kitu chochote. Kwa hiyo, mwananchi ana uhuru wa kumchagua mtu anayemtaka. Kwa hiyo, sasa Serikali ijitafakari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwa watumishi. Mlikuwa na zoezi lile la kuondoa watumishi hewa. Watumishi

hewa waliondolewa, lakini kuna taasisi ambazo sasa hivi zinafanya vizuri. Hata Taasisi ya Bunge, Watumishi wa Bunge wanafanya kazi vizuri tu, mishahara iko wapi? Wapeni stahiki zao za mishahara. Mkienda Muhimbili, pia huko Madaktari sasa hivi wanafanya kazi vizuri. Wapeni mishahara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesema mmeboresha shule kongwe. Zile shule kongwe mlizoziboresha, bado kuna changamoto ya Walimu wa Sayansi. Kwa hiyo, sasa tuhakikishe shule zile nazo zinapata Walimu wa Sayansi na wale Walimu wapandishwe madaraja. Hata wale walimu wengine wanaostahili kupandishwa madaraja wapandishwe, wale wanaostahili kupandishiwa mishahara wapandishiwe. Kuongezwa vyeo... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maryam.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na mjadala, naomba tutambue uwepo wa wanafunzi 126 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma amba ni wageni wa Wabunge kutoka Mkoa wa Manyara, wakiongozwa na Ndugu Nikomedi Josephati. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. (*Makofi*)

Tunaendelea na mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, baadaye Mheshimiwa Tauhida Gallos na Mheshimiwa Josephine Chagula wajialdae.

MHE. LOLESLIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti muhimu kabisa ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli,

kwa usimamizi mzuri ambao anaufanya kila wakati. Ameweza kusimamia, kwa kweli tunaona matokeo makubwa kwa kipindi kifupi tunaona mambo yanaendelea vizuri. Ni Serikali inaendelea kusimamia vizuri na kutekeleza sera kwa vitendo ambazo zipo katika nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora na Naibu Mawaziri wote, watumishi wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanazozifanya. Wote tunafahamu TAMISEMI imebeba wananchi wa nchi hii ya Tanzania. Inashughulika na changamoto nydingi katika Taifa hili. Masuala ya elimu, afya, barabara na kwa kweli TAMISEMI ni kila kitu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nikianza katika Sekta ya Afya, nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ya ujenzi wa vituo zaidi ya 352 Tanzania nzima. Kwa kweli ni kazi kubwa iliyotukuka. Napongeza kazi hii kubwa ambayo imeifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia pia katika mkoa wangu, hasa katika Halmashauri ya Wilaya yangu, nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kutupatia shilingi bilioni 1.5 ambazo zimejenga Hospitali ya Halmashauri katika eneo la Nzela. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutupatia shilingi milioni 400 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya Nyarugusu. Natoa shukrani hizi kwa sababu kusema ukweli kikikamilika kituo hiki kitapunguza changamoto kubwa ambayo wananchi wa Nyarugusu walikuwa wakiipata. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kunatokea mambo ya vifo pamoja na changamoto mbalimbali, lakini kwa kupewa hizi shilingi milioni 400, kwa kweli kwa niaba ya wananchi, wanashukuru sana kwa kazi kubwa na fedha nydingi ambazo mmetupatia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika Sekta ya Afya najua bado changamoto zipo. Kwa mfano hii hospitali ambayo tumepewa, inajengwa Nzela, lakini jiografia yetu katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa kweli changamoto ni kubwa sana. Haiwezekani mtu akatoka Jimbo la Busanda kwenda kutibwa Nzela, ni mbali. Afadhalii hata akatibiwe Geita Mjini. Kwa hiyo, tunaona jiografia yake ni ngumu, itawezesha wananchi watapata changamoto kubwa kabisa kwa ajili ya usafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja mwaka 2018 akatuahidi kujenga hospitali Katoro. Nimeangalia kwenye bajeti sijaweza kuona. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, tuangalie, maadam Waziri Mkuu ametuahidi, alikuja Geita akatuahidi pale pale Katoro na wananchi wakafurahi wakiamini kwamba hospitali itajengwa Katoro. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba hebu atutafutie fedha popote ili hospitali hii iweze kujengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu Katoro ni Mamlaka ya Mji Mdogo, lakini ukiangalia uhalisia ni zaidi ya Mamlaka ya Mji kamili. Kwa hali halisi ya kibashara kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini, pamoja na shughuli za uvuvi na shughuli za biashara, watu wengi sana wako mahali pale. Kwa kweli ni Mji wa kibashara, tunahitaji hospitali. Watu ni wengi, tunahitaji huduma. Ukienda kwenye kile Kituo cha Afya cha Katoro kimezidiwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli mtutazame kwa macho mawili. Ninajua kwamba wewe umeshafika Katoro, kwa hiyo, nakuomba kabisa, ikiwezekana tuma timu maalum ije iangalie changamoto ilivyo kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanahangaika sana. Mara kwa mara hata ukienda katika hospitali ya rufaa ya mkoa zaidi utakuta watu wengi wanatoka Katoro, kila dakika gari la Katoro linapeleka wagonjwa kwenye Hospitali ya Rufaa. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri

atuangalie; na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatuhahidi kwa hiyo tunaomba sasa utekelezaji uweze kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia, katika Sekta hii ya Afya tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi. Kwenye Wilaya ya Geita tu tuna upungufu wa takribani watumishi zaidi ya 150, ni wengi sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika bajeti hii tuangalie namna ya kuwekeza zaidi kuajiri watumishi katika Sekta ya Afya ili hatimaye tuweze kufikia ile azma ya kuweza kupunguza vifo kwa ajili ya akina mama pamoja na watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba kwa juhudhi ambazo zinaendelea kufanyika na Serikali ile changamoto iliyokuwepo katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa ya vifo vya akina mama tuna imani kabisa kwamba itakwenda kupungua sasa. Cha msingi, naiomba Serikali iendelee kutuongezea kipaumbele, yaani mtupe kipaumbele zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta hiyo hiyo ya Afya, kuna Kituo changu cha Afya cha Bukoli ambacho kwa muda mrefu sana kimekuwa na changamoto kubwa sana. Hatuna gari la wagonjwa katika eneo hilo, tarafa nzima haina gari la wagonjwa. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri aliniahidi. Kwa hiyo naomba sana, mara magari yakipatikana, tunaomba sana ukumbuke Kituo hiki cha Afya cha Bukoli kiweza kupatiwa gari la wagonjwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara nyingine kama Wizara ya Nishati. Wizara ya Nishati kuna changamoto kubwa sana, unakuta eneo umeme umefika, lakini unakuta kwenye huduma za afya, labda kwenye elimu; shule za sekondari hakuna umeme. Hii ipo, kwa mfano, Kituo cha Afya Bukoli, pamoja na kwamba umeme umefika Bukoli mwaka 2014 lakini mpaka leo kituo cha afya hakina umeme. Kwa hiyo, upasuaji hauwezi kufanyika bila ya kuwa na umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi wamefuatilia lakini wanaambiwa ili kuweka tu umeme pale watoe shilingi milioni 10. Yaani kituo cha afya kupatiwa umeme lazima shilingi milioni 10 zitolewe zilipwe TANESCO. Kwa hiyo, ninaiona hii ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, naionba Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara nyininge; Wizara ya Nishati, hebu tuangalie namna bora ya kuweza kufanya kazi kwa ushirikiano. Hapa tutaweza kuokoa maisha ya wananchi wetu na wataweza kupata huduma zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora. Nimeangalia katika kitabu chake ukurasa wa 83 ameweza kuzungumzia jinsi ambavyo ameandaa Mpango wa MKURABITA wa kurasi misha maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini katika Mkoa wa Geita. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana kwa mpango huu. Naomba utekelezaji uweze kufanya kama ambavyo ameweza kupanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu mkoa wetu, tunategemea shughuli za uchimbaji wa madini. Kwa miaka mingi wachimbaji hawa walikuwa wadogo wadogo, walikuwa hawawezi kutambulika. Kwa mpango huu sasa wa kurasi misha wachimbaji wadogo, tuna imani kubwa kwamba tutaweza kupata mchangomkubwa sana katika pato la Taifa kwa ujumla pamoja na mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Tauhida, baadaye Mheshimiwa Josephine Chagula ajiandae.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia katika Wizara hizi mbili; Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais wetu ametukopesha Watanzania imani, ametukopesha Watanzania mapenzi, ametukopesha Watanzania utu wema, ametukopesha Watanzania kazi, ametutendea haki. Tunaahidi 2020 kulipa alichotukopesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanamna pia ya pekee nichukue fursa hii nimshukuru Rais wangu wa Zanzibar, mwongeaji aliyeppita kabla ya huyu aliyekaa alizungumzia Zanzibar naakasema kwamba hali ya kisiasa haiko vizuri. Niseme katika ukumbi huu kwamba Zanzibar hali ya kisiasa iko vizuri, Rais wa Zanzibar anaisimamia siasa ya Zanzibar vizuri hatuna mashaka usiku na mchana tunatembea bila wasiwasi na siasa inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Mawaziri wa Wizara zote mbili nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Jafo, kazi kubwa anayoifanya pamoja na wasaidizi wake, lakini pia nimpongeze Waziri wa Utawala Bora kazi kubwa wanazozifanya Mwenyezi Mungu atawalipa, maana tukisema tu kwa mdomo haitoshi lakini tuseme kwa vitendo tunaiona kazi kubwa wanayoifanya, tunasimama kutimiza wajibu na kuona maeneo gani ambayo wanahitajika kuongeza nguvu ili tuweze kwenda vizuri kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama leosuala kubwa ninalotaka kulizungumza ni suala la Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Mahitaji Maalum. Nimwambie kaka yangu, Mheshimiwa Jafo pamoja na kazi

kubwa na majukumu aliyokuwanayo na wasaidizi wake, aweke mkazo kwenye suala la Mfuko wa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Mahitaji Maalum. Sehemu hii tunahitaji mkazo wa kipekee, suala kubwa ndani ya Taifa letu, janga kubwa tulililokuwa nalo ni suala la ajira kwa vijana. Kwa maneno ya vijana wanakwambia hatuna njia ya kutokea isipokuwa kwenye Mfuko huu. Kaka yangu, Mheshimiwa Jafo mengi anayoyafanya tunampongeza na mazuri, mazuri na yakupigiwa mfano. Tunamwomba kaka, kwa vijana wanawake na watu wenye mahitaji maalum aweke mkakati mahususi wa kuusimamia Mfuko huu ambao utakwenda kuwakomboa wanawake na vijana. Mfuko huu upo na unafanya kazi, lakini unasuasua, haupo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa ndani ya Kamati ya *LAAC* miaka mitano Mwenyezi Mungu aliyonipa kibali cha kuingia Bungeni kuititia nafasi za vijana, nilikaa ndani ya Kamati ya *LAAC*, Mfuko huu haufiki kwa vijana kama ipasavyo, haufiki kwa wanawake kama ipasavyo na kwa sasa tumeongeza kufika kwa watu wenye mahitaji maalumu. Mpaka sasa ninavyoongea namshukuru Mheshimiwa Spika kwa kunirudisha tena kwenye Kamati ya *LAAC*, kwahiyo napata kujua tathmini mambo yanakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo halmashauri zinaendelea vizuri, hatusemi kwa asilimia mia moja, lakini zinaendelea vizuri, jitihada zake zinafanya kazi, aweke mkazo kwenye Mfuko huu ili vijana wapate kutoka, akiwapa fursa vijana kutoka kuititia Mfuko huu, namwambia kaka, Mheshimiwa Jafo hatuna wasiwasi na yeye, Mwenyezi Mungu aendelee kumbariki maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu waVijana, Wanawake na Watu Wenye Mahitaji Maalum ndiyo kwenye kilio, labda kaka, Mheshimiwa Jafo ifike wakati nikutolee mfano, kuna halmashauri ya mwisho wakati tupo kwenye Kamati, tulikwenda Halmashauri ya Kahama kama sikosei. Halmashauri ya Kahama wana mradi unahitwa unaitwa Mradi wa Dodoma. Kaka, Mheshimiwa Jafo mradi ule umetoa ajira kuititia huo huo Mfuko, ajira elfu moja mia tano

na sabini na tisa, lakini hapo hapo wamepatiwa viwanja wanawake, vijana na watu wenye ulemavu watu738.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama nimwombe jambo moja tu kaka, Mheshimiwa Jafo, aendeakakague kama itamridhisha, kama ule mradi umefanywa upo sana salama ashawishi na halmashauri nyingine ziige. Ni mfano wa kuigwa, leo kijana wa Tanzania aliyekuwa akiuza karanga, aliyekuwa akipanga mananasi matatu, manne, Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wetu anapata hati miliki ya kiwanja bure. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kamakaka, Mheshimiwa Jafo utamridhisha, atauhisi uko salama, hautakuwa na matatizo mbele ya safari akauangalie, ashawishi na halmashauri nyingine. Naamini kama utakuwa mradi mzuri, basi halmashauri nyingi zikitaka, vijana watapata mabadiliko kwa sababu leo kijana ana hati miliki kwamba ana sehemu anapamiliki, anaenda kukopa wakati wowote, saa yoyote, benki yoyote, kwa sababu hati miliki ya kumiliki anayo.

Sasa nimshauri na kumwomba Mheshimiwa Jafo kwamba, akiangalia na ukimridhisha, kama itawezekana mfumo unaotolewa fedha kwa vijana kuititia halmashauri, kwa sasa fedha hazina marejesho, vijana wakipewa fedha hawarejeshi, lakini kama tutatumia mfumo huo kwamba amepatiwa viwanja bure, wameenda kukopa huko mwenyewe, wataelekezwa utaratibu mzuri wa kukopa, watasimamiwa na mabenki basi mambo yataendelea kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimwambie kaka, Mheshimiwa Jafo kwamba tuwapongeze pamoja na Utawala Bora, zamani ukienda halmashauri, wafanyakazi wa halmashauri, Mkurugenzi kaenda leo wanasema kesho ataondoka, lakini sasa hivi mambo hayako hivyo, kila mfanyakazi aliyeuwepo kwenye halmashauri akiiona Kamati ya LAAC anatamani kuulizwa ajibu nini kinaonesha kwamba

wafanyakazi wameelimika, wamefundishwa vya kutosha, utawala bora unaonekana. Niwaombe kwamba waendelee kusimamia bila wasiwasi...

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa Mwakanyoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji, amekuwa ana tamka mara kwa mara kaka Jafo kwa mujibu wa kanuni, ni kwamba lazima aheshimu sana nafasi yake awataje kwa vyeo vyao kama ni Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aseme ili na watu wamwelewe na *hansard* ziweze kusoma vizuri. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tauhida.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake. Asiwe muungwana kwa hapa, awe muungwana na kwa mengine wanayoyaona Rais yetu anayoyafanya na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri ni Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naomba waendelee kuwasimamia wafanyakazi. Kulikuwa na tatizo sugu la mfanyakazi anaharibu halmashauri moja, ugonjwa wake unahamishiwa halmashauri ya pili, kaka Jafo...

WABUNGE FULANI: Aaa,aaa. (*Makofî/Kicheko*)

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO: Mheshimiwa Waziri sijaona kipindi hiki hilo tatizo, hilo tatizo limepungua kwa asilimia kubwa. Niseme kwamba kulikuwa na matatizo ya ma-*engineer* kutokujua wajibu wao, lakini sasa mambo yamebadilika hayajaondoka, hayajamalizika, lakini yamepungua. Kwahiyo, Mheshimiwa Waziri kwa maeneo wanayofanya vizuri lazima tumpongeze, lakini asiache kuendelea kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo pia la kukaimu, Mheshimiwa Waziri ajitahidi kwenye hili. Mtendaji waHalmashauri unapomwambia kakaimu hawajibiki ipasavyo, kwanza anawajibika kwa hofu, jambo la pili anachofanya ni kufanya kazi kwa kutokujiamini. Kwahiyo, Mheshimiwa Waziri kamahili eneo utalismamia kumaliza suala la watu wanaokaimu, litatusaidia na tutaendelea kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine linalosumbua ni suala la Wanasheria waliokuwepo ndani ya Halmashauri. Nafikiri ni muda mzuri wa kukaa na Wanasheria waliokuwemo ndani ya halmashauri na wanaotaka kuwapeleka, kwa sababu baadhi ya halmashauri bado hazina Wanasheria, mambo mengi ambayo yanaharibika ndani ya halmashauri chanzo kinachosababisha na kinachochangia pia ni kutokuwa na Wanasheria wazuri. Wapeleke Wanasheria wazuri ambaao wataweza kuisaidia halmashauri hususan kwenye suala la kuingia mikataba, halmashauri zimekuwa zikilega lega au zikiharibika kwenye suala hili au haliko vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kama maeneo haya atayakazia vizuri na kuyasimamia vizuri, nafikiri kwamba kero na matatizo ya ndani ya halmashauri yatakwisha.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwaasilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Chagula, baadaye Mheshimiwa Augustino Masele na Mheshimiwa Ibrahim Raza wajiandae.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya TAMISEMI. Kwanza nianze

kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema lakini pia kuweza kusimama hapa leo jioni hii. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa hotuba yake nzuri, lakini pia tumpongeze sana kwa kazi nzuri anazozifanya. Vile vile niwapongeze Manaibu Waziri, niwapongeze watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini vile vile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Utawala bora, hongera sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, nimpongeze Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa jinsi wanavyotekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hongera sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa jinsi ilivyojipanga kuhakikisha afya za Watanzania zinaimarika vizuri. Kwa kweli Serikali imejitahidi kwa kiasi kikubwa sana kuweza kujenga hospitali za wilaya, hospitali za mkoa lakini pia kujenga vituo vya afya, zahanati, kununua vifaa tiba vya kutosha na kikubwa zaidi kupata madawa ya kutosha kwa nchi nzima. Haya yote ni matunda mazuri ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, tunamshukuru sana, tunampongeza mno na tunamtakia kila lilio la kheri katika maisha yake hapa duniani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Geita tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi tumeweza kupata billion 5.9 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya rufaa na kwa sasa tumeshapata bilioni 3.7 na mkandarasi yupo kazini anaendelea. Tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, palipo na mafanikio lazima kuna changamoto; changamoto yangu ya kwanza ni upungufu wa Wauguzi katika zahanati zetu, kuna upungufu

mkubwa sana wa watumishi katika zahanati zetu, unaweza ukakuta zahanati moja, ina Muuguzi mmoja, anafanyaje kazi. Sasa niiombe sana Serikali iweze kuona ni namna gani itaweza kutupatia Wauguzi wa kutosha katika zahanati zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni upungufu wa Madaktari katika vituo vyetu vya afya. Hili pia ni tatizo, huko kwenye vituo vya afya tunapofanya ziara, kuna vituo vya afya vingine utakuta daktari mmoja na muuguzi mmoja. Kituo cha afya ni wananchi kata nzima, wananchi hawa ni wengi mno kuweza kupelea huduma na mtu mmoja, niiombe sana Serikali iweze kuona ni namna gani itaweza kutupatia Madaktari wa kutosha katika vituo vyetu vya afya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yangu ya tatu ni kukosekana kwa Madaktari Bigwa katika wilaya, niiombe sana Serikali yangu iweze kupeleka Madaktari Bigwa kwa watoto na akinamama katika hospitali zetu za wilaya. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu kumekuwa na msongamano mkubwa mno kwenye hospitali zetu za rufaa kwa sababu ya wagonjwa wengi kwenda kwenye rufaa, lakini Madaktari Bigwa wakiwa kwenye hospitali za wilaya tutapunguza huo msongamano na wananchi wetu watakuwa hawapati shida kama hivi sasa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kuliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tena, katika Mkao wangu wa Geita wananchi wamehamasika sana kujenga maboma kwa ajili ya vituo vya afya lakini pia, Zahanati kwa maana hiyo tunamaboma mengi sana ambayo yamesimama na nimpongeze sana Mkuu wangu wa Mkao wa Geita kwa jinsi alivyosimamia ujenzi huo, niombe sasa Serikali iweze kuunga mkono jitihada za wananchi hawa ili maboma hayo yaweze kukamilika kwa kuezekwa na wananchi hawa waweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza hayo, naomba kuunga mkono hoja. *Ahsante. (Makof!)*

MWENYEKITI:Ahsante sana Mheshimiwa Josephine Chagula. Kutokana na muda wetu tutamalizia na Mheshimiwa Augustino Masele,dakika tano na Mheshimiwa Ibrahim Raza, dakika tano.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nilikuwa naomba nimpatie bwana Raza hizo dakika zangu tano ili mimi nichangie kesho. Ahsante.

MWENYEKITI: Sawa Mheshimiwa Ibrahim Raza.

MHE.IBRAHIM HASSANALI RAZA: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante. Kwanza nimshukuru kaka yangu kwa imani yake aliyonipa hizo dakika tano nichangie, kwa hiyo zitakuwa ni kumi, Mwenyezi Mungu amzidishie. Pia nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba za Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa George Mkuchika katika hotuba zao. Kabla sijaendelea huko mbele nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi zake mie kusimama hapa na kuweza kuzungumza mambo mawili matatu ambayo yatasaidia kueleza changamoto zetu.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, nikianza na Wizara ya TAMISEMI, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Jafo kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwa kweli naweza kusema ni Waziri mwenye kiwango, nikisema Waziri mwenye kiwango kwamba ni Waziri ambaye kwa kweli ameleta matumaini mapya kwa wananchi na kwa Serikali yetu hii ya CCM. Nampongezasana Mheshimiwa Jafo pamoja na wenzake, Manaibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, nataka vilevile nizungumzie changamoto ambazo zinatokana na hii Wizara. Kwanza kabla sijakwenda huko niwapongeze Wakuu wa Mikoa, kwa sababu Wakuu wa Mikoa kwakweli kwa awamu hii wanafanya kazi nzuri na wanasmamia mapato ya halmashauri, lakini baadhi ya halmashauri hawajafanya vizuri katika *ku-collect zile ten percent* ya vijana akinamama na watu wenye ulemavu. Kwahiyoo, naomba sana Wakuu wa

Mikoa wawe kidogo wakakamavu na wawafuatilie Wakurugenzi wao kwasababu tunayo taarifa kwamba halmashauri nyingi zimekuwa hazifanyi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambazo nataka kuzungumzia hapa kwanza hii ya *ten percent* ambao kwa kweli baadhi ya Wakurugenzi wanakuwa hawazikusanyi hizi pesa zinavyotakiwa na vilevile wanazitumia kwa matumizi mengine ambapo hii *ten percent* ya vijana, akinamama na walemaavu, tumepitisha hapa Bungeni ikawa ni sheria mama kwamba zitumike katika mambo tuliyokusudia. Kwahiyio, ningeomba sanaWakurugenzi hili suala la *ten percent*, huu ndiyo uhai wa wananchi wetu maskini ambao wanategemea hii asilimia kumi kufanya miradi yao ambayo inayaendeleza mbele maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri nikija kwenye suala la usafiri wa *DART*, hili limekuwa janga katika Jiji la Dar es Salaam. Nasema janga kwa sababu nimeshuhudia na nimepata malalamiko mengi sana kwa wananchi wetu kwamba mabasi hayatoshi, mabasi mengi yameharibika na vilevile pale Kimara pamekuwa watoto na akinamama wanavyobanwa hata kuvuta pumzi wanashindwa wengine wanarudi nyumbani hawaendi makazini. Sasa hili suala la *DARTnamwomba* sanaMheshimiwa Waziri alivalienjuga, kwa kweli nikimpelekea picha ambazo ninazo kwenye simu zangu atawaonea huruma akinamama na watoto wanavyobanwa, yaani wamebanwa na wengine wanakanyangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya matatizo ya *DART*hao Wapinzani wanaidakia sana hii, kuikemea Serikali na kuitukana Serikali yetu ya CCM, hiyo ndiyo imekuwa ajenda yao wapinzani, lakini hawajui kwamba matatizo haya yanawahusu na wao vile vile siyo watu wa CCM tu. Kwahiyio, namwomba Mheshimiwa Jafo suala la *DART*ha kama huyu mwekezaji amefeli hawezi basi aniambietu Mheshimiwa Raza hebu tutafutie mwekezaji mwingine, nitamtafutia mwekezaji mzuri sana ambaye ataondoa matatizo haya ya usafiri wa mabasi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa mzee wangu Kapteni George Mkuchika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, ni kaka yangu, ni mzee wangu, nimpongeze kwa hotuba yake nzuri ambayo haina mashaka. Sisi nimashahidi wa Tanzania, utawala huu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hauna doa hata *zeropointone percent*. Nataka niwaambie Wapinzani kwamba huu utawala bora uliokuwa Tanzania, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Mungu alivyompa imani Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa mambo anayoyatenda, lakini kuna nchi huwezi ukasema jambo lolote la ubaya wa yule mfalme ambaye anaongoza katika nchi ile, utapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa leo Tanzania hii, watu wana fursa ya kuzungumza, wanafursa ya kusema, wanafursa ya kutembea, leo mwisho tunakuwa hatuthamini utawala bora ambao unaongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa kweli naweza kusema kwamba, Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa ni mfano katika Afrika na sasa hivi katika Afrika sisi tupo *post* ya juu kabisa katika nchi ambayo ipo amani katika nchi hii yaani tujipongeze sisi Wabunge wote kwamba Tanzania ipo juu katika amani. Isitoshe katika Afrika tu hata katika nchi za Afrika Mashariki na kati *we are top number one* katika amani. Kwahiylo, hii peke yake inasadikisha kwamba kweli utawala bora uliokuwepo na amani ipo, ungekuwa utawala bora si mzuri, basi na amani isingekuwepo, ingetoweka. Kwahiylo, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika, namwambia aendelee hapo hapo na kama kuna msumeno aendelee, lakini tuweke nchi katika hali ya nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niwapongeze ndugu zangu wa TAKUKURU, wameweza kufanya kazi kubwa sana ya kuwapeleka mahakamani mafisadi wakubwa ambao walikuwa wanajilikana mapapa wa nchi hii. Nataka nimwambie Mkurugenzi wa TAKUKURU, Diwani Athman kwa sababu namwamini na pale alipowekwa na Mheshimiwa Rais kwa sababu naye kamwamini, kwahiylo Ndugu Diwani Athuman apige kazi, asiogope sura ya mtu, bado kuna

mafisadi wamefichika ndani ya pazia, wamefilisi nchi hii, kwahiyo Mheshimiwa Waziri nataka ashirikiane na huyu Mkurugenzi wetu wa TAKUKURU ili aweze vile vile kuwafichua wengine ambao wamefilisi nchi hii na kutufikisha hapa tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwahiyo nampongeza sana. Kwa kweli rushwa imeondoka Tanzania sivyo kamatalivyokuwa miaka ya nyuma, sasa hivi nidhamu imerejea katika kazi. Rushwa ndogo ndogo ipo bado, lakini na hakika chini ya Wizara ya Mheshimiwa George Mkuchika na hizo rushwa ndogo ndogo nazo zitaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nafikiri nimetumia muda wangu dakika kumi kama ipasavyo, nikushukuru kwa kunipa nafasi na naiunga mkono Wizara hii *hundred percent*. Pia Wizara ya Mheshimiwa Jafo naiunga mkono *hundred percent*.Mwenyezi Mungu ampe afya na umri Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Amini. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ibrahim Razana huyo ndiyo mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo. Nawashukuru wote kwa namna ambavyo mmewajibika kufanya kazi zenu za kibunge na sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho tarehe 12 Aprili, 2019 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.43 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 12 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*